

# **FITRA**

(UMBILE)

الفطرة

**Mwandishi:**

Ustadh Sayyid Jawad Naqvi

**Kimetarjumiwa na:**

Salman Shou

**Kimehaririwa na:**

Al-Haj Ramadhani S.K. Shemahimbo

## **الفطرة**

**تأليف**

**الأستاذ السيد الجواد النقوي**

**من اللغة الإنجليزية إلى اللغة السواحلية**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**  
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 039 – 5

**Mwandishi:**  
Ustadh Sayyid Jawad Naqvi

**Kimetarjumiwa na:**  
Salman Shou

**Kimehaririwa na:**  
Al-Haj Ramadhani S.K. Shemahimbo

**Kimesomwa-Prufu na:**  
Ustadh Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepitiwa na:**  
Al-Haji Mujahid Rashid

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**  
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Aprili, 2017  
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**  
Alitrah Foundation  
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania  
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555  
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com  
**Tovuti:** www.alitrah.info

---

---

# YALIYOMO

---

Utangulizi.....	vi
Neno la Mchapishaji .....	vii
Dibaji .....	1
Msingi wa somo.....	3
Fitra (Hali ya kimaumbile) ni nini? .....	5
Barzakh .....	10
Fitran4a Khilqat (uumbaji) .....	12
Uelekeo wa binadamu kwa mintarafu ya Fitra .....	14
Kwa nini binadamu amepotoka .....	15
Kusudio la dini na mwongozo .....	16
Kuisahau Fitra.....	22
Neno “ <i>Fitra</i> ” (Hali ya kimaumbile).....	26
“ <i>Fitra</i> ’ ni mtindo wa Khilqat .....	29
Upendeleo, <i>Karamat</i> ya binadamu juu ya viumbe vingine.....	35
Mpango wa kuelimisha Fitra .....	35
Mapana ya Ulimwengu .....	37
Mwenyezi Mungu Mtukufu hubadili mtindo wa uumbaji .....	40
Falsafa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Kujipongeza Mwenyewe .....	43
Binadamu ameumbwa kwa kusudio gani?.....	47
Khalq (ni ile sehemu ya uwepo wa binadamu) na Khulq (ni ile sehemu iliyokabidhiwa kwa binadamu) .....	49
Umbo la binadamu – Mwili na Roho.....	53
Maana ya “ <i>Hanif</i> ” (kuelekea) .....	62

Maana ya “Shi’ah”(jina la Madhehebu ya Kiislamu) .....	74
Madhehebu na kurudi kwa mintarafu ya Dini Hanifa .....	70
Fitra na Sunnah .....	72
Maana ya maada katika Falsafa .....	74
Dunia Inayooonekana na Isiyoonekana iliyopo ndani ya binadamu .....	78
Upekee wa uumbwaji wa binadamu .....	81
Kwa nini Mwenyezi Mungu anasema “Nilipuliza roho yangu ndani ya binadamu? .....	85
Tofauti baina ya Fitra na Tabiyat (mambo ya kimwili).....	86
Kanuni zenyе msingi wa kuelewa dini iliyo sahihi .....	88
Uimamu-Sharti la Fitra .....	90
Binadamu wa Magharibi.....	98
Tabiyat (mambo ya kimwili).....	101
Maana halisi ya neno “ <i>Tabiyat</i> ” .....	103
“ <i>Tabiyat</i> ” ya viumbe vyote.....	108
Tabiyat ipo kwa binadamu na wanyama.....	109
Mapambano ya Fitra na matokeo yake .....	111
Binadamu-Kiumbe asiyejulikana.....	112
<i>Ghariza</i> (silika za asili).....	114
Falsafa ya starehe.....	127
Tofauti baina ya <i>Hidayat-e-Takwini na Ghariza</i> .....	132
Fitra ya mwanamume na mwanamke .....	136
Hivi Uislamu umepitwa na wakati baada ya miaka 1400? .....	147

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## UTANGULIZI

**K**itabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenyewe kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam  
Al Itrah Foundation  
Barua Pepe: [alitrah@yahoo.com](mailto:alitrah@yahoo.com)  
SMS: +255 778 300 140

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## **NENO LA MCHAPISHAJI**

**K**itabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha Kiingereza kiitwacho, *Fitrat*, kilichoandikwa na Ustadh Sayyid Jawad Naqvi na kutarjumiwa kwa Kiswahili na Ndugu Salman Shou.

Lengo kuu la muumini ni kufikia takua (*taqwa*) ya hali juu. Lakin ili kufikia hatua hii, ni lazima muumini awe amelelewa kiroho na kutayarishwa vizuri ili kufikia lengo hilo. Moja ya matayarisho hayo ni umbile (*fitrah*) lake, yaani kuielewa hali yake ya maumbile na pia ulezi (*tarbiyah*), yaani mambo yake ya kimwili, nukta ambazo zitafafanuliwa vizuri ndani ya kitabu hiki.

Kitabu hiki ni mlolongo wa mihadhara ya mwandishi aliyokuwa akiitoa mara kwa mara kwa lengo la kuzifafanua kielimu nukta hizi mbili – umbile na ulezi.

Kutokana na umuhimu wa mada hii, tumeamua kukichapisha kitabu hiki kama kilivyo kwa lugha ya Kiswahili kama ada ya Taasii yetu ya Al-Itrah kuwashudumiwa wasomaji wetu wa lugha ya Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu, sayansi na tekinolojia ambapo upotoshaji wa historia, ngano na hekaya ni vitu ambavyo havina nafasi katika vichwa vya watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki, Ustadh Sayyid Jawad Naqvi kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa ajili ya Umma huu wa

Waislamu, Allah Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru ndugu yetu Salman Shou kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na yeye Allah Azza wa Jallah amlipe kila la kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na Akhera pia.

**Mchapishaji  
Al-Itrah Foundation**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## DIBAJI

### Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

**F**itra (Hali ya kimaumbile) ni somo la msingi la mtu kujitambua mwenyewe na halafu kitabu hiki ni tafsiri ya mlolongo wa miadhara iliyotolewa na Hujjatul Islam Syed Jawad Naqvi juu ya mada hii. Mada hii sio ya kisomi lakini ni mada ambayo inagusa roho, na msomaji akilitenda haki somo hili basi linawenza kubadili utambuzi wake wa kuhusu yeye mwenyewe. Kitabu hiki anapelekewa msomaji mwenyewe. Msingi wa somo hili ni aya ya 30 ya Surah Rum, pale ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelekeza uzingativu kwenye uumbwaji wa “*Fitra* (Hali ya kimaumbile)” ya wanadamu ambayo inatoa mfano wa pekee kwa uumbaji Wake ikimtofautisha binadamu na viumbe vingine vyote. Upendeleo, ufahari na kitu cha thamani cha wanadamu kinatokana na “*Fitra*”(Hali ya kimaumbile) na “*Fitra*” hii ambayo uelekeo wake tangu mtu anapozaliwa umewekwa kwa mintarafu ya dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ambayo kituo chake cha mwisho ni asili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hutiishwa na kupotea. Matokeo ya kutokujua mada hii ya msingi ni uharibifu na imesababisha kufanyika makosa makubwa sana yanayofanywa na wanadamu katika historia yote. Msingi wa somo, kwa mara nyingine ni maelekezo ya Kiongozi Mkuu Ayatullah Syed Ali Khamenei (d.a.) yakiwa ni ujumbe kwa wahubiri wa kidini waweze kuwasilisha kwa ummah Masomo kutoka Karbala. Katika kipindi cha nyuma waliowahi kuwa wafuasi na masahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ na Imam Ali ؑ walikwenda Karbala na

wakamchinja mtoto wao; Husein bin Ali ﷺ katika namna ya kikatili sana. Hapa mwandishi anawasilisha msingi wa chimbuko la sababu na uchambuzi wa tukio la Karbala. Kwa kuelewa somo hili la “Fitra,” tukio lote la Karbala linagawika katika kundi la watu ambaao ama walikuwa wahanga wa “Fitra” iliyoharibika au wale ambao “Fitra” yao iling`aa kwelikweli na wakafanikiwa kupata furaha kuu. Kwa mara nyingine tena ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kunijaalia upendeleo huu wa kutafsiri kazi hii ya kuheshimika.

**Syed Arif Rizvi**

بسم الله الرحمن الرحيم

## MSINGI WA SOMO:

**K**iongozi Mkuu wa Mapinduzi ya Kislamu; Ayatullah Syed Ali Khamenei (d.a.) alipokuwa akiwahutubia wanafunzi wa kitheolojia miaka michache iliyopita alisema kwamba mada moja muhimu inayofaa kuwasilishwa kwa watu ni Masomo kutoka Karbala. Hasa zaidi ye ye ali kuwa na maana ya kuhusu kipimo hiki, ambacho kinatakiwa kusemwa kuhusu ni nani hao watu waliokwenda Karbala kama wakandamizaji, watu kama Shimr, Hurmula, Kholi na wengine waliofika idadi ya maelfu? Watu hawa walikuwa ni Waislamu au sio Waislamu? Hivi walikuwa wanamjua Husein ni nani? Walikuwa wanajua wanapigana na nani? Kwa kweli wali-kuwepo wachache waliokuwa wanamjua Husein bin Ali ﷺ vizuri zaidi ya wengine. Shimr ali kuwa ofisa wa cheo cha juu katika jeshi la Imam Ali ﷺ. Kwa hiyo ni vipi hawa watu wakawa wauaji? Ni kitu gani kiliwafanya washushe hadhi zao kuwa chini mno? Palikuwepo na baadhi ya sababu ambazo historia imezificha. Umari bin Saad akawa muuaji wa Husein ﷺ kwa sababu tu ya kuahidiwa Ugavana huko Rae, na vivyo hivyo Shimr naye aliahidiwa cheo cha juu. Wengine waliahidiwa rasilimali, wengine waliahidiwa mammalaka wakageuka kuwa maadui na wauaji wa Husein ﷺ. Jambo hili linafaa kufanyiwa tafakuri kwamba, kama ahadi ya namna hiyo inaweza kumfikisha Umari bin Saad na Shimr kwenye kiwango cha kufedheheka kiasi hicho, basi ahadi za namna hiyo zinawenza kufanya hivyo kwa wengine pia. Leo hii pia wapo akina Umari bin Saad na Shimr wengi, lakini Husein ni wachache sana. Leo hii hawawezi kumuona Husein. Kama wanaweza kumuona Husein basi

wapo tayari kumkata shingo Husein kwa sababu ya ulafi, tamaa ya mamlaka, utajiri, na umashuhuri. Hiki ni kipimo cha somo kutoka Karbala. Kitu ambacho kiliwashusha na kuwadhalilisha wauaji wa Karbala ni kuitelekeza Fitra (Hali ya kimaumbile). Waliitelekeza Fitra ya Utu. Kama mtu akiacha kutilia maanani njia ya Fitra na anachepuka na kuacha njia ya Fitra, basi atakuwa ameacha dini na pia atageuka kuwa muuaji wa mjukuu wa Mtukufu Mtume ﷺ kama walivyofanya Shimr na Kholi.

Fitra ambayo ni fahari ya wanadamu na sehemu ya msingi wa binadamu imesahauliwa na binadamu mwenyewe. Mtu mwenye Fitra amegeuka kuwa mtu asiye na Fitra. Maovu yote na mikengeuko yote ni matokeo ya kuchepuka na kuacha njia hii ya Fitra (maumbile) ambapo urekebishaji, mwongozo na mambo ya kimwili (*Tabiyat*) yote ni njia ya kurudi kwenye Fitra (Hali ya kimaumbile). Kama tunataka kupata dondoo za mafundisho yote ya Kidini katika sentensi moja basi inawezekana kusema kwamba Dini ya Uislamu haikuja kuwapa binadamu kitu kutoka nje, badala yake Dini ya Uislamu imekuja kuhuisha asili ya uelekeo wa binadamu ambayo tayari ipo, yaani Fitra ya Binadamu. Kama Fitra ikifufuka basi mtu huyo anakuwa ameongoka na hivyo anafanikiwa. Mitume wote waliteuliwa na Maimamu walipewa kazi kwa ajili ya kuhuisha na kuipatia uhai Fitra ya Binadamu. Mhimili wa vitabu vyote vya dini ni Fitra (Hali ya kimaumbile) ya binadamu na leo hii kama mtu amejitenga sana na kitu, basi kitu hicho ni Fitra. Leo hii binadamu ni mtu asiye na Fitra na badala ya Fitra, nafasi yake imechukuliwa na vitu fulani vingine ambavyo vitatajwa baadaye.

Wanafalsafa wote mashuhuri ambao wametangulia mbele ya haki, walikuwa wanaifuatilia *Fitra* ya Binadamu. Watakatifu wote wa Mwenyezi Mungu Mtukufu (*Awliya Allah*) na warekebishaji ambao wamefika kwenye vituo vyao walifanikisha hili baada ya kuhui-

sha Fitra yao. Watu wote wa dunia ambao wamekengeuka wameangukia kwenye maangamizi kwa sababu tu ya kutelekeza Fitra yao. Katika sentensi moja kwa yule mtu anayetaka kuwa Yazid, anachotakiwa kufanya ni kuchepuka tu na kuacha njia ya Fitra; na kuitelekeza Fitra yake. Somo ambalo linahitaji msisitizo mkubwa sana ni somo la Fitra (Hali ya kimaumbile). Katika Qur`ani Tukufu Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaja kuhusu uumbwaji wa binadamu na akamfanya binadamu awe mwangalifu kwa mintarafu ya kitu hiki cha thamani kilichopo ndani mwake. Mwenyezi Mungu Mtukufu alipeleka vitabu nya mbinguni na viongozi wa dini ili lulu hii (*Fitra - Hali ya kimaumbile*) iendelee kuwa hai.

Utamaduni ambao tumechukua leo; utamaduni huu tulionao katika zama zetu, na utamaduni ambao ndimo jamii zetu zimo, ni utamaduni unaoua Fitra. Dondoo za wanafalsafa wote, dondoo za dini zote, matokeo ya jitihada za warekebishaji wote, ni kuhuisha Fitra ya Binadamu tu. Endapo binadamu angeweza kugundua kitu hiki cha thamani na kuweza kukitambua!

### **Fitra (Hali ya kimaumbile) ni Nini?**

Tumelisikia neno hili lakini hatujui maana yake. Siku hizi watu wanapokutana kwa kawaida huulizana kuhusu afya zao za kimwili (*Tabiyat*). Binadamu anatamani na hujaribu kuweka mwili wake katika hali nzuri na afya nzuri kwa kadiri awezavyo. Kama kuna dosari kidogo katika afya yake atasema afya yake sio nzuri au mwili wake haupo salama siku hiyo. Kama mwili ukipata maradhi kidogo tu binadamu hukimbilia kwa dakitari, na kuanza kutumia fedha, na hii inaonesha binadamu anahuksika kiasi gani na usalama na afya njema ya mwili wake au upande wake wa kimaumbile. Lakini imepata kutokea binadamu kuulizana kuhusu afya ya Fitra kama vile wanavyoulizana kuhusu afya ya miili yao? Binadamu ni wazembe na hawa-

jali hadi kiwango hiki, ambapo hawajali hata kuulizana kuhusu afya ya Fitra zao.

Fitra (Hali ya kimaumbile) ambayo ni sisi au mimi, mimi mwenyewe na ni uhalisi na mhimili wa binadamu; binadamu anatakiwa kujihusisha na kitu hicho pia. Katika Surah Rum; aya ya 30 Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtaka binadamu aelekeze usikivu wake kwa mintarafu ya uhalisi huu. Hii ni aya ya Fitra. Katika aya hii binadamu ametakiwa kunyoosha uelekeo wake kwa mintarafu ya Fitra. Wito huu unaelekezwa kwetu binadamu kwa sababu mielekeo yetu ipo katika mielekeo mahususi tofauti:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّدِينِ حَنِيفًاٰ فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخُلُقِ اللَّهِ  
ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيْمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

**“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini-ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini ya sawasawa, lakini watu wengi hawajui.” (Surat ar-Rum; 30:30).**

Qur`ani Tukufu inasema kwamba watu wengi hawajui kuhusu jambo hili. Fitra hutafsiriwa kama asili na kutokea hapa ndipo inapojulikana kwamba binadamu hajui kitu kuhusu Fitra. Kiingereza ni lugha lakini katika utamaduni wa zama za leo, kama mtu anajua Kiingereza inadhaniwa kwamba anajua kila kitu. Kiarabu ni lugha lakini inapotokea mwanachuoni akisomea Kiarabu anadhani yeye amekuwa *Hujjatul-Islamu*, lakini katika hali halisi yeye ni *Hujjatu* wa Kiarabu. Kusema Fitra maana yake ni asili ni sawa na kusema juu maana yake ni mti. Kwa kuwa huwa linapotumika neno asili katika Kiingereza inakuwa ni uhakikisho (*Hujjat*) kwa wengi na huanza kusema maana ya Fitra ni asili. Hili ni kosa kubwa. Kwa kuwa hatujatafakari kuhusu vitu hivi viwili yaani, asili na Fitra. Kosa hili lin-

aendelea kufanyika. Ipo asili ndani ya binadamu lakini Fitra maana yake sio asili.

*Tabiyat* maana yake ni asili na *Tabiyat* ni neno la Kiarabu. *Tabiyat* na Fitra ni maneno mawili tofauti. Katika hali halisi binadamu anavyo vitu vitatu ndani mwake ambavyo vinakaribiana, na ipo haja ya kuvitambua vitu hivi kimoja baada ya kingine. Vitu hivi vitatu ni *Tabiyat*, *Fitra* na *Ghariza*. *Ghariza* maana yake ni silika za asili. Vitu vyote hivi vipo ndani ya binadamu, lakini utu wa binadamu haupo chini ya huruma ya *Tabiyat* na *Ghariza*. Utu wa binadamu unategemea Fitra yake. Katika Surah hii ya Rum, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema amemuumba binadamu kwa Fitra ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Binadamu wamejisahau wao wenyewe kwa hiyo Fitra wanaielewa kimakosa kama *Tabiyat*, yaani: sisi, sisi wenyewe kuwa maana yake ni Fitra. Matunzo yote yanaelekezwa kwa *Tabiyat* (mambo ya kimwili), jithhada zote za binadamu zinaelekezwa kwa mintarafu ya *Tabiyat*. Elimu, Malezi, Sayansi, Chakula na kila kitu kinatoa huduma kwa manufaa ya *Tabiyat*, uwezo wote wa Fitra unajishughulisha katika kuihudumia *Tabiyat*. Fitra imekuwa mtumishi wa kuihudumia *Tabiyat*. Juhudi zote za kisomi, kimwili, kiroho zinatumika katika kuihudumia *Tabiyat*. *Tabiyat* imeshiba na kujinenepea, lakini Fitra inaogopa na ni dhaifu. *Tabiyat* inatawala na Fitra inati.

Hatua ya kwanza ni kujua maana ya *Fitra* ni nini, na halafu yatazamwe mambo yanayohusu Fitra. Halafu zinaangaliwa bidhaa zinazozalishwa na Fitra na *Tabiyat*. Karbala ni uwanja wa mapambano ya *Tabiyat* na Fitra. Upande mmoja palikuwepo jeshi la Fitra na upande mwagine palikuwepo jeshi la *Tabiyat* (mambo ya kimwili). Kama Fitra ikipewa umbo la kuonekana, basi umbo hilo litakuwa ni Husein bin Ali ﷺ na Masahaba wake; vivyo hivyo kama *Tabiyat* ikipewa umbo la kuonekana, ambapo Fitra imelala na kutiishwa,

basi umbo hilo litakuwa ni jeshi la Umari bin Saad, Shimr, Yazid na wale wote maelfu ambao walikuwa jeshi la Tabiyat. Hiyo Tabiyat inapotanda huwa kipingamizi kwa Fitra ambapo Fitra hushinikizwa na kuzikwa.

Baada ya kuapa mara 11 katika Surah Shams, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَاللَّهُمَّ هَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا قَدْ أَفْلَحَ مِنْ زَكَاهَا

**“Akaifahamisha uovu wake na takua yake. Hakika amefaulu aliyeit-akasa,”** (as-Shams; 91:8-9)

وَقَدْ خَابَ مَنْ نَسَاهَا

**“Na amepata hasara aliyeitweza.”** (Sura no 91:10)

Wale ambao wanaitunza Tabiyat yao ndiyo hao ambao Fitra yao imezikwa.

Ni lazima watu wajue somo hili la Fitra kwa ajili yao, wato-to wao na mfumo wao wa jamii. Kwa kukengeuka na kuacha njia ya Fitra ipo haja ya watu kujiuliza wao wenyewe kwamba Tabiyat (mambo ya kimwili) hii inawaelekeza kwa mintarafu gani? Qur’ani Tukufu inawauliza na kusema;

فَأَيْنَ تَدْهِبُونَ.

**“Mnakwenda wapi?”** (Sura no 81:26)

Rudi. Hatukukuumba ukiwa hivi; tumekuumba wewe ukiwa safi kabisa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَفْوِيمٍ.

### **Hakika tumemuumba mtu katika hali nzuri mno. (Sura 95:4)**

Ewe binadamu tumekuumba wewe ukiwa mzuri sana na kupendeza, lakini umegeuka kuwa nini?

Mtu akitaka kumtuma mwanawe mahali fulani atamvisha nguo nzuri iliyopigwa pasi, atampaka manukato, atamchana nywele, na halafu mtoto anarudi baada ya kuanguka kwenye mfereji wa majitaka. Sasa mama atasema nini? Mtoto wangu mpendwa, sikukutuma ukiwa hivi, nilikuisha nguo, sasa kwa nini umekuja umechafuka namna hii? Huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inazidi sana humura ya mama.

يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ

### **Ewe Mtu! Nini kilichokughuri na Mola Wako mkarimu? (Qur’ani Sura al-Infitaar 82:6)**

Mimi nilikuwa Mola Wako mkarimu, nilikuumba ukiwa mzuri sana, lakini umegeuka na kuwa kitu gani. Unajua jinsi nilivyokuumba wewe? Tulikuumba kutokana na udongo, halafu tukakufanya upite katika safari kubwa, halafu tukakuweka katika hali kadhaa na unajua matatizo ya kiasi gani wengine walipata kwa ajili yako. Na sasa wewe umerudi kwangu ukiwa katika hali hii? Fitra yako iko wapi? Umekuja kwangu na malundo haya ya Tabiyat (mambo ya kimwili). Umepotezea wapi kile kitu cha thamani nilichokukabidhi? Sasa baada ya kifo utakuwa hapa Barzakhi. Sasa wewe ngoja hapa Barzakhi hadi wakati hiyo Fitra yako itakapotoka imeng’ara kutoka chini ya malundo ya Tabiyat (mambo ya kimwili) ili niweze kufunga milango ya Pepo kwa ajili yako.” Hayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## **Barzakhi:**

Barzakhi ni sawa na karantini. Karantini ni sehemu ya uwanja wa ndege ambapo wasafiri hukaguliwa ili kuhakikisha kwamba hawana maradhi yoyote. Na yeote akionekana na maradhi haruhusiwi ku-changanyika na watu hadi atibiwe na kupona. Kwa nini watu wanazuwa hapo Barzakhi? Kwa kuwa watu wanabeba virusi na bakteria ndani mwao, na Pepo ni mahali pa viumbe hai vilivyo vitakatifu na si mahali pa viumbe hai waliobeba dhambi. Kwa hiyo ipo haja ya watu kutakaswa hapo. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anase-ma kaa hapa hadi hapo utakapokuwa umepata kinga.

Wanadamu wanasema: “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Vipi? Tunaweza kurudi tulikotoka?” Jibu ni “Hapana.” “Sasa tunaweza kufanya chochote hapa ili tutakasike?” Jibu tena ni “Hapana, kaeni hapa tu na mngoje” Binadamu wanaendelea kulalamika; “Hatuwezi kwenda mbele, hatuwezi kurudi nyuma, hatuwezi kufanya chochote hapa pia Mola Wetu! Dhambi hizi tulizobeba zitatakaswa vipi?” Jibu: “Dhambi hizi zitatakaswa na yale mliyoyaacha nyuma. Sasa wekeni matumaini yenu juu ya hayo, labda yanaweza yakawapatia msaada.”

“Labda kama mmeacha watoto wema wanaweza wakawasaidi-eni, lakini kama watoto mliowaacha wamekengeuka na wamejaa dhambi, wao pia hawatakupeni msaada wowote. Kama mmeanzisha kituo cha elimu ya kidini na wapo watu ambao wamefuata desturi nzuri basi hayo yanaweza kuwa na msaada kwenu.”

“Kama hakuna chochote, labda wale watu ambao mliishi nao katika maisha yenu wanaweza kukumbuka kuwaombeeni ili mpate msamaha wa dhambi. Na kama mionganoni mwa watu hao yupo mmoja ambaye ametakasika na yupo karibu na Mimi, na kama aki-waombeeni, labda ninaweza kusikia dua yake na kuwapunguzieni

mizigo yenu ya Tabiyat (mambo ya kimwili), na Fitra iking`ara hapo milango ya rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu itafunguka.” Kama mtu hatataka kukaa muda mrefu katika Karantini hiyo afanye nini?

Taarifa hii ipo katika hadithi kwamba aina ya watu wawili havakai Barzakhi; aina moja ni ya mtu ambaye Fitra yake imeharibika kabisa. Mtu wa namna hii huenda Jahannam moja kwa moja. Na aina ya pili ni ya mtu ambaye Fitra yake haina hata kovu dogo; mtu wa aina hii huenda Peponi moja kwa moja. Tatizo lipo kwa watu kama sisi. Kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupatia hii mialaka sitini ya kuishi hapa duniani ambayo ni kipindi cha kung`arisha Fitra sio kuizika.

Roho huwa haizikwi kaburini, bali mwili ndiyo huzikwa kaburini. Roho huwa ipo katika dunia ya kaburi (*Qabr*) ambayo ni Barzakhi mahali ambapo usaili hufanyika. Lakini roho huusikilia mwili kwa sababu imekuwa pamoja na mwili kwa muda mrefu. *Alam-al-Qabr* ni dunia iliyosambamba ambayo inajulikana kama Barzakhi. Dunia hii sio kama hii yenye mambo ya kimaumbile, wala sio akhera. Binadamu huwekwa katika hali hii ili ajirekebishe. Wale ambao wamejikamilisha wenyewe hufika mbinguni, na wale ambao wamejiharibu kabisa watatupwa motoni moja kwa moja.

Wale ambao wamefanya uovu hapa duniani kama kujenga nyumba ya kuonesha filamu, dhambi zozote ambazo hufanywa humo, mwenye kujenga nyumba hiyo atakutana na athari zake hapo Barzakhi. Inasemekana kwamba mtu anayeanzisha desturi ovu basi wale watu wanaofuata desturi hizo dhambi zao zitawekwa kwa yule aliyeanzisha desturi hizo. Hali ileile inatumika kwa mtu ambaye ameacha kitu kizuri baada ya kifo chake, mtu huyo atapata malipo ya thawabu. Hivi ndivyo ambavyo mtu hukamilishwa katika Barzakhi.

Adhabu ya kaburini ni shinikizo ambalo roho hupata katika Barzakhi. Dunia hiyo ni pana na kubwa zaidi ya dunia hii. Imependekezwa kutembelea makaburi na kusoma Surah Fatiha lakini sio kwamba roho ipo pale kwenye kaburi linaloonekana. Roho huwa inasikiliza kwa mintarafu ya kaburi lakini hata kama mtu akifanya mema kwa niaba ya marehemu mahali popote thawabu na athari zake zitaifikia roho. Sio lazima kwamba mtu akitembelea makaburi ni kwa ajili ya kupata thawabu za marehemu tu. Falsafa ya kutembelea makaburi na kupendekezwa sana sio kwa ajili ya kupeleka Thawabu kwa marehemu tu, jambo hili lipo zaidi ya hapo. Talakini anayosomewa maiti ni kitendo cha ishara, kwa sababu hatuna uwezo wa kuiona na kuigusa roho. Talakini (ushauri) hupelekwa kwa roho na chochote kile anachosomewa maiti roho husikia.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atupatie nguvu ya kufungua sura hii ya Fitra na Yeye mwenyewe atuongoze kwa mintarafu ya Fitra, na labda kwenye mkusanyiko ambapo somo hili linazungumziwa au mionganoni mwa wale wanaosoma somo hili la Fitra kutoka kwenye kitabu hiki anatokeza mtu mmoja ambaye anaweza kung'arisha Fitra yake, anaihuisha na kutatua matatizo yake. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba hata kama mtu mmoja aliyehudhuria kwenye mkusanyiko huo akitoka humo akiwa ametakasika, basi Mwenyezi Mungu anauneemesha mkusanyiko wote na wote wale walio hudhuria kwenye mkusanyiko huo wa dini.

### **Fitra na *Khilqat* (Kuumba):**

Vipo vitu vitatu vilivyopo ndani ya binadamu; Tabiyat, Fitra na Ghariza. Shahidi Murtadha Mutahhari anacho kitabu kinachoitwa *al-Fitrat*. Neno Fitrat limekuja mara moja ndani ya Qur`ani Tukufu katika Surah Rum. Lakini familia ya neno hili; ambalo ni *Maftuur* (aliyeumbwa), *Fatara* (ameumbwa), *Faatir* (muumbaji) na *Munfatir* (aliyeumbika) yanatumika katika sehemu nyingi.

Katika majina mazuri sana ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, lipo jina moja nalo ni **Faatir**.

Tafsiri ya kawaida inayotumika kwa neno *Faatir* ni Muumbaji. Fatara maana yake ni Kuumba. Lakini *Faatir* na *Khaliq* hayana maana sawa. Lipo neno *Khalqiyat* (Uumbaji) ambalo lipo katika *Faatir*, lakini zipo sifa maalum zingine pia katika *Faatir*. Endapo Sifa hizi maalum zinaingia katika uumbaji basi inakuwa Fitra, na kama Muumbaji anazo sifa hizi maalum basi anakuwa *Faatir* (Muumbaji). *Khalaq* maana yake ni kuhuluku uwepo.

Aina moja ya Uumbaji ni kuumba kitu kipya ambacho mfano wake wa kitu cha zamani tayari upo. Aina nyingine ya *Khilqat* (Uumbaji) ni kwamba malighafi ipo na halafu kinaumbwa kitu kutokana na malighafi, kama vile vyungu kutokana na udongo na mkate kutokana na unga. Malighafi ipo, muumbaji anakipatia kitu sura na umbile. Aina ya tatu ya uumbaji ni kwamba hakuna malighafi iliyopo, na wala hakuna mfano wa kitu kile ambacho kimekuwepo kabla ya hapo, lakini ni kuumba kitu kutokana na kitu kisichokuwepo (*Adamu*) na kuwa kwenye uwepo (*Wujuud*) ni *Fatr*. Kwenye viwanda, malighafi hununuliwa, hupelekwa kiwandani na bidhaa huzalishwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu haku-fanya hivyo.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkabidhi binadamu Fitra maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu alitoa uumbaji wa kwanza kwa binadamu ambaeo haukuwa na mfano kabla yake na pia hakuna uten-ganisho wa maada hii iliyokuwepo kabla yake. Vitu vyote vile am-bavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alivikabidhi katika uumbaji wake wa kwanza vilikuwa Fitra, lakini bado hivi sio vyote ni sifa za Fitra ambazo zitazungumziwa baadaye.

## Uelekeo wa Binadamu kwa Mintarafu ya Fitra:

Katika Surah Rum, aya ya 30 Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema siri ya uumbwaji wa binadamu ambayo imepewa jina la Fitra, na dini ya sawasawa; na wanadamu wameagizwa kuelekeza usikivu wao kwa mintarafu ya dini.

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلّدِينِ حَنِيفًاٰ فِطْرَتَ اللّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَاٰ لَا تَبْدِيلَ لِخُلُقِ اللّهِ<sup>۲</sup>  
ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيْمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسَ لَا يَعْلَمُونَ

**“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini-ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndio dini ya sawasawa, lakini watu wengi hawajui.” (Surah Rum, 30:30).**

Uelekeo wa safari ya binadamu kwenda kwenye dunia isiyooone-kana, umewekwa kabla na Fitra yake, na binadamu huzaliwa akiwa amekwisha wekewa uelekeo wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba binadamu; alitunza na kuung`arisha uumbaji Wake katika namna iliyo nzuri sana (Mustawi ni neno ambalo limetumiwa na Qur`ani Tukufu).

Alama hii kwa mintarafu ya upekee na uzuri katika uumbaji huu uliofanywa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu hakumremba binadamu nje tu lakini pia alianzisha uelekeo wake (na kituo chake) ndani ya uumbwaji Wake. Binadamu hazaliwi akiwa amechanganyikiwa, pamoja na kwamba baada ya kuzaliwa binadamu hujikanganya mwenyewe, na zaidi ya hapo hukanganywa na binadamu wenzake; na sababu zingine za kuchanganyikiwa kwake pia zimekuwa ni pale anapo jitenga na Fitra yake.

Uelekeo wa Fitra ni kwa mintarafu ya Mola na lugha ya Fitra ndiyo lugha ya Qur'an. Inapotokea binadamu anajitenga na Fitra yake pia huwa ni vigumu kwake kuelewa Qur'an. Njia ya mwongozo ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamuru kwa ajili ya binadamu ni vitu ambavyo vinaendana na Fitra yake.

### Kwa Nini Binadamu Amepotoka?

Ni jambo la kustaajabisha kwamba pamoja na kwamba zipo njia kadhaa ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameziumba na kuzianzisha kwa ajili ya binadamu katika namna ya ufunuo, Mitume, Maimamu ambao walikuwa taa ya kandili na jua la mwongozo, bado binadamu amekengeuka na amepotoka. Swali hili huja kwenye akili za watu: kwa nini binadamu yupo gizani, amepotoka na kudhalilika? Pale ambapo jua la mwongozo lipo kileleni lakini binadamu bado yupo kwenye upotofu? Sababu ni kwamba jua ambalo lipo kileleni na kutupa miale yake kwenye Fitra ya binadamu lakini wale ambao Fitra zao zimezikwa hawapati chochote kutoka kwenye miale hii. Yaani pale ambapo jua lipo kwenye kilele wakati wa mchana na ambapo kila kitu hunufaika kutokana na nuru hii na mng'aro wake, wapo viumbe ambao hupendelea kukaa kwenye giza. Viumbe hawa ni popo ambao hukubali kila kitu isipokuwa mwanga na jua. Hii ni kwa sababu popo hawana uwezo unaohitajika kufyonza mwanga wa jua.

Ama iwe Qur'an Tukufu, Mitume, Maimamu, Watakatifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu (*Awliya Allah*) wote hao ni viwango mbalimbali vya mwongozo. Fitra ni uwezo ambao ndio humwezesha binadamu kupokea mwongozo kutoka kwenye vyanzo hivi vya mwongozo. Mahubiri yote ya Qur'an Tukufu ni kwa ajili ya Fitra; Enyi watu! Enyi waumini! Uelekeo wa Fitra ni kwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجُونَ

**Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake tutarejea.**  
**(Qur'ani Sura al-Baqarah 2:156)**

Pale ambapo Fitra itakapopata ulimi na kuzungumza itatongoa aya za Qur'ani Tukufu. Zama za leo tunazo lugha na maneno mbalimbali, ambayo mionganoni mwao mojawapo ni lugha ya Fitra. Wale ambao bado wanaishi na Fitra au Fitra bado hai na hajatiishwa, ukitaka kuandika wasifu wao, basi wasifu huo utageuka kuwa aya za Qur'ani Tukufu. Unapotaka kuzipatia aya za Qur'ani Tukufu umbo na sura zitatokeza kuwa Mtu Mkamilifu, (*Insaa-e-Kaamil*), yaani Fitra iliyotakasika. Mifadhaiko ya kila aina na matatizo ya kila aina ni vitu ambavyo vipo ndani ya binadamu katika zama za leo ama viwe vya kibinagsi, kijamii, kielimu, kisiasa; vyote hivi ni kwa sabbu ya kujitenga na Fitra na kuacha njia ya Fitra (Hali ya kimaumbile).

### **Kusudio la Dini na Mwongozo:**

Kusudio la Dini na Mwongozo ni kumgeuza binadamu arudi kwenye mintarafu ya njia ya Fitra. Viongozi wa Fitra wametoa wito kwa usikivu wa binadamu kwa mintarafu ya Fitra. Hotuba ya kwanza ya *Nahjul-Balaghah* ni hotuba nzuri kiasi kwamba mwanafalsafa Mulla Sadri baada ya kusoma hotuba hii akatekwa na shauku. Ni sawa tu na wale ambao wana mazoea ya muziki ambao baada ya kusikiliza muziki hutekwa na hisia kali. Muziki huathiri mfumo wa mishipa ya fahamu ya binadamu na hisi hugonganishwa na muziki na watu hutekwa na shauku. Shauku inapotawala hekima, Fitra na moyo basi mtu hutekwa na hisia kali kwa urahisi kupitia kila kitu kinachoamsha hisia kali. Na pale ambapo mgongano unafika kileleni, hali hiyo huitwa *Wajd*. Vivyo hivyo pale ambapo nyoyo zilizotakasika ziki-

soma hotuba hizi za *Najul-Balaghah* nazo hupata ile hali ya *Wajd*. Hizi ni hotuba za hisia kali almuradi Fitra ya mhusika iwe imetakasi-ka. Wapo watu ambao hawajajifunza taratibu zinazoonekana laki-ni wameziweka Fitra zao katika hali iliyotakasika. Ukimwangalia George Jordac, anatoa kilio cha nguvu kwa dunia nzima “kwa Sauti ya Kuwataka Binadamu kuwa Waadilifu.” Anasema; “Enyi Watu! Sikilizeni! Mwenyezi Mungu Mtukufu ameleta zawadi hapa duniani kwa jina la Ali.” Mtu huyu ni Mkristo lakini ameiweka Fitra yake katika hali ya utakaso; huyu sio Mkristo aliyechakachuliwa, bali ni Mkristo aliye safi. Anawaambia Waislamu kwamba wamesikia jina la Ali lakini hawapendezewi na maneno ya Ali. Tunapojitenga na Fitra inakuwa ndiyo sababu ya shida, matatizo na mikengeuko yetu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba ameumba mbingu iwe kama paa na ardhi iwe kama kitanda kidogo cha kulala mtoto. Kitanda cha kulala mtoto ni mahali pa starehe kwa ajili ya mtoto, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba dunia hii iwe kama kitanda cha starehe, lakini dunia hii hii imekuwa sehemu ya shida kwa binadamu na mahali pa matatizo kwa binadamu. Dunia hii inaweza kuwa kama kitanda cha kustarehe mtoto kwa binadamu kama binadamu anakuwa na Fitra yake. Wapinzani wa Fitra wameigeuza dunia hii kuwa sehemu ya majanga na misaada. Fitra huilewa lugha ya Qur`ani Tukufu, Mtukufu Mtume na pia lugha ya akili. Tabiyat haiwezi kuelewa yote haya; yenyewe hukubali muziki na utani. Fitra hupenda uhalisia tu. Watu husikiliza tetesi na hufurahi sana kusiki-liza tetesi, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ametengeneza yakini (*Yaqiin*) kuwa ndiyo chakula cha Fitra.

### أَلْهَاكُمُ التَّكَاثُرُ

**Kumewashughulisha kujifaharisha kwa wingi!  
(Qur`ani Sura at-Takaathur 102:1)**

Ewe binadamu, umeendekeza lahwi. Matamanio na ashiki ni vitu ambavyo vimekushika. Wewe umekuwa sio mtu wa kutimiza mahitaji yako ya msingi, lakini badala yake umekuwa mtu wa kutaka kuongeza malimbikizo ya hayo uliyonayo. Unataka uwe na magari mengi zaidi, nyumba nyingi zaidi, fedha nyingi zaidi na rasilimali nyingi zaidi.' Baadhi ya watu wamekwisha kuwa na pato kubwa sana hivyo kwamba vizazi vyao mia moja vinaweza kula, lakini bado ulafi wao wa kupata zaidi haujaisha. Wanajishughulisha mno hivyo kwamba hesabu zao hazijulikani.

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ

**Si hivyo! Mtakujajua! Tena si hivyo! Mtakujajua! (Qur'ani Sura at-Takaathur 102:3-4)**

Lakini hali hii haiwezi kudumu milele, baada ya muda sio mrefu watajua.

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ

**Si hivyo! Lau mngelijua kwa ujuzi wa yakini. (Qur'ani 102:5)**

Kama mtu angekuwa amepata yakini basi angeweza kuiona hapa pia.

لَتَرَوْنَ الْجَحِيمَ

**Hakika mtauona moto. (Sura 102:6)**

Mola Wetu anasema abuduni na msimamishe utumwa wenu hadi kwenye kiwango cha yakini (*Yaqiin*). Bin Sina ambaye tulim-jua kama tabibu, pia alikuwa mwanafalsafa, lakini tunaanzisha vi-tuo vyaa afya na maduka ya dawa kwa kutumia jina lake. Mtu huyu

hakuwa daktari. Baada ya kuchoka kufanya kazi yake halisi, ali-kuwa na desturi ya kupumzika kwa kujishughulisha na masuala ya tiba. Mtu huyu alikuwa msomi, na mwanafalsafa ambaye alitambua uhalisi na uwepo. Mtu huyu anasema kwamba kama mtu anakubali jambo kabla ya kuwa na yakini nalo au kama anakataa jambo kabla ya kuwa na yakini nalo atakuwa ametengana na Fitra yake. Hii maana yake ni kwamba mtu asikubali jambo hadi awe na yakini nalo na mtu asikatae jambo hadi amekuwa na uhakika nalo. Sasa hebu tutathmini, kama tumemwamini mtu baada ya kuwa na yakini na yale aliyoyasema au tumekatataa kumwamini mtu baada ya kuwa na yakini na yale aliyoyasema, je tathimini hiyo ilifanyika kwa yakini? Mathalani tunasikiliza sentenso moja ya mtu na tunaanza kumfuata, na tunasikiliza sentenso moja nyingine kutoka kwa mtu mwingine na tunakataa kumfuata. Tunaamini kama mtu akisema na tunakataa kuamini kama mtu akisema.

Watu wa aina mbili walikuwa wakipendezewa na Mitume ﴿﴿﴾. Aina moja ni wale ambaao walipendezewa na miujiza ya Mitume ﴿﴿﴾ na aina nyingine ni wale waliopendezewa na elimu ya Mitume. Wale waliopendezewa na miujiza tu ya Mitume ﴿﴿﴾, walikwenda kwa Mitume kwa sababu ya miujiza. Miujiza maana yake ni mambo yasiyoweza kuelezeaka kwa akili ya kawaida. Wakati mwingine watu wadanganyifu hutumia hila ambazo pia huonekana kama vitu visivyo vya kawaida. Kwa hiyo wale ambaao huenda kwa Mitume kwa ajili ya kuona miujiza tu kwa macho yao pia hupendezewa na ghilba ya watu werevu na kufikiria kwamba ghilba hizo nazo ni miujiza. Lakini watu ambaao hupendezewa na elimu na hekima ya Mitume ﴿﴿﴾, wale wanaoona mwujiza kwa macho ya Fitra kamwe hawawezi kudanganywa na hila za werevu, hata kama maelfu ya hila hizo na michezo ya kimazingaombwe ikioneshwa lakini kamwe hawatadan-ganyika.

Kila mtu anajua ubora wa Maimamu Maasumu ﷺ. Kwa mcheza michezo ya mieleka nguvu msuli ndiyo ubora wake, kwa mtu mkarimu, ukarimu ndiyo ubora wake mkubwa; kila mtu huangalia ubora kwa miwani aliyovaa. Ibn Sina ameona ubora katika lugha ya falsafa. Pale ambapo mwanafalsafa anasema kuhusu ubora wa Ali ؓ hafanyi hivyo kama wafanyakyo wahutubiaji. Amesema kwamba hali na msimamo wa Ali baada ya Mtukufu Mtume - ni sawa na hatua ya *Maquul* (akili) aliyonayo ndani ya *Mahsuus* (his). Pale ambapo tofauti baina ya Maqool na Mahsoos zinakuwa dhahiri basi tunaweza kuelewa ni aina gani ya ubora anaozungumzia? Mahsoos ni vile vitu ambavyo vinaweza kuhiwi na hisi na Maqool ni vitu vile ambavyo havihiwi na hisi lakini vinaweza kujulikana kwa *Aql* (akili) tu. Kama vile Mwenyezi Mungu Mtukufu Yeye ni *Maaquul* sio *Mahsuus*. Ibn Sina anasema kwamba kama vile ilivyo kwa vitu vingine ambavyo haviwezi kutambulika kwa hisi, vitu hivi vinaweza kushikwa na Akili tu, msimamo wa Ali ؓ baada ya Mtukufu Mtume - ulikuwa ule wa *Aql* (Akili) ndani ya hisi. Katika Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anazungumza kuhusu *Bi'that* (uteuzi wa Utume). Baadhi ya watu huwafikiria Mitume kama wanavyowafikiria Maulana (Wachungaji). Mitume hawakuja kuwaondoa wanadamu katika mambo yao ya lazima na kuwafanya wafanye vitu ambavyo hawavipendi. Mitume walikuja kuwaelekeza wanadamu wasifanye shughuli za ufujaji badala yake wafanye shughuli zenyen makusudio.

Binadamu yu kama maji. Kama maji yakiwa yametulia na kutuama huzalisha vijidudu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa mifano mingi ya maji kwa binadamu. Maji yaliyotuama huchafuka; maji yaliyo safi ni yale tu yanayotiririka. Mtukufu Mtume - hakuja kuchukua maji kutoka kwenye mto wa Dini na kumwaga kwenye tangi la Wanadamu badala yake Mitume walikuja kuasiisi mibubujiko ya

chemchem kutoka kwenye Fitra ya binadamu.

Kwenye seminari nyingi watu huendelea kujifunza kwa miamaka mingi, lakini wakizungumza ni kwa saa chache halafu wana-takiwa kujifunza tena kwa ajili ya mhadhara ufuatao. Kwa nini? Hii ni kwa sababu yale waliyojifunza yalikuwa sawa na kuchukua madumu yasiyokuwa na kitu na kuchota maji kutoka mtoni na kumwaga maji hayo kwenye matangi yaliyokuwa hayana maji. Sasa basi kama maji yapo ndani ya tangi katika hali ya kutuama, maji hayo yatavukiza na kuwa mvuke katika kipindi kifupi. Mtu anapofariki dunia hata kama amejifunza katika maisha yake yote lakini wakati wa kifo, mabega hutingishwa na marehemu huambiwa kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye Mungu wako, Muhammad ndiye Mtume wako. Yote haya marehemu alikuwa anayatamka kila siku; Ali ni Walii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, katika maisha yake yote wakati wa uhai wake alikuwa anatamka kaulimbiu hizi za Ali, sasa kuna haja gani ya kumkumbusha wakati yupo kaburini? Mitume ﷺ wamekuja kutiririsha chemchem kutoka ndani ya binadamu.

Qur`ani Tukufu inasema, mtu anayekuwa katika hali ya utakaso kwa siku arobaini mfululizo tu, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenyezi Mungu hutiririsha chemchem za hekima na elimu ndani ya mtu huyo. Hii ni kazi ngumu sana; mtu huyo ajariibu kuwa katika hali ya utakaso kwa dakika arobaini tu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kwa dakika arobaini awe anafikiri kuhusu Mwenyezi Mungu tu, moyo wake uwe unahisi kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu tu. Asikilize kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu tu. Angalia jinsi ugumu ulivyo. Makontena yanaweza kumalizika lakini chemchem ni chanzo kisichokauka.

Kwa nini Mitume ilikuja? Katika hotuba ya kwanza ya *Nahjul-Balaghah*, Amirul-Mu'minin Imam Ali ﷺ anasema;

“Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwateuwa Mitume ﷺ ili kwamba waweze kuamsha kile kilichopo ndani ya binadamu na sio kuweka kitu kilichopo nje ya binadamu.” Imam Ali رضي الله عنه anasema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuumba binadamu na dini hii na binadamu huzaliwa akiwa na dini hii na kwa hiyo Mitume haikuja kuweka dini ndani ya binadamu ambayo ilikuwa nje, lakini badala yake walikuja kuhuisha dini ambayo tayari ilikwishawekwa ndani ya Fitra ya binadamu.

### **Katika Kuisahau Fitra:**

Kitu hiki Fitra ambacho amekabidhiwa binadamu, na humo ndimo uhalisia wake ulimo ni nini, lakini binadamu anakuwa mzembe. Katika Qur`ani Tukufu Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambia wanadamu wasiwe kama wale ambao waliendekeza ufuasi wa madhehebu.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَقْرَفُوا

**“Msiwe kama wale walogawanyika katika makundi”.**  
**(Qur’ani Sura aal-Imraan 3:105)**

Pia imetamkwa katika hadithi nyingi kwamba msivae, msizungumze, msitembee na kufanya vitu vinavyomchukiza Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika aya hii wakati wowote msiwe kama wale ambao wanaendekeza makundi.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ نَسُوا اللَّهَ

**“Msiwe kama wale ambao wamemtelekeza Mwenyezi Mungu Mtukufu”. Akawasahaulisha nafsi zao.**  
**(Qur’ani Sura al-Hashr 59:19)**

Kitu gani kitatokea kama mtu atakuwa kama wale ambao wam-emtelekeza Mwenyezi Mungu Mtukufu? Hivi Mwenyezi Mungu Mtukufu atapata hasara yoyote kwa sababu ya kutelekezwa na ki-umbe Chake? Kama vile watu walivyo katika kanuni kuhusu ndugu zao, wanapowasahau ndugu zao, huhisi vibaya na kusikitika. Sio hivyo kwa upande wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwamba atasikitika kama waja Wake watamsahau. Inapohusu mahusiano ya kindugu watu huwasahau ndugu masikini na huwakumbuka ndugu matajiri tu, lakini watu wanapomsahau Mwenyezi Mungu Mtukufu matokeo huwa ni tofauti. Matokeo ya mja kumsahau Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kwamba atakuwa amejisahau yeye mwenyewe.

### فَأَنْسَاهُمْ أَنفُسُهُمْ

#### **Akawasahaulisha nafsi zao. (Qur'an Sura al-Hashr 59:19)**

Mtu ambaye amejitambua mwenyewe ni kwamba amemtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtukufu Mtume ﷺ amesema kwamba vitu hivi viwili; *Itrat* (Dhuria Watukufu wa Mtume) na Qur'an Tukufu havitatengana; hata kama jaribio la kuvitenganisha vitu hivyo likifanywa, bado havitatengana. Vitu hivi haviwezi kutenganishwa kwa sababu uhalisia wao ni sawa; mionekano yao tu ndiyo inayot-fautiana. Kwa hiyo pale ambapo jaribio la kuvitenganisha litafaniki-wa vyote vitapotea. Qur'an Tukufu haikuwa na Ahlul-Bayt ﷺ kwa namna ya kwamba walikuwa wanaibeba mifukoni mwao. Ile hali ya kuwa pamoja kwa vitu hivi viwili namna yake ni kwamba mwongozo ni mmoja, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba sampuli mbili za mwongozo huu, sampuli ya Qur'an Tukufu na nyingine ni Ahlul-Bayt ﷺ. Chochote kinachosemwa na Qur'an Tukufu kinaweza kuonekana kivitendo katika maisha ya Ahlul-Bayt ﷺ, na chochote kilichofanywa na Ahlul-Bayt ﷺ kinaweza kuthibitishwa na Qur'an Tukufu. Hii ndiyo sababu ambayo imewafanya Ahlul-

Bayt ﷺ waseme kwamba wakati wowote unapokutana na hadithi yetu, ithibitishe kwa kutumia Qur`ani Tukufu. Kama kitu kinakin-zana na Qur`ani Tukufu, basi hiyo sio hadithi ni fungu la maneno ya Kiarabu ambalo linatakiwa kuangikwa ukutani.

Qur`ani Tukufu inasema kwamba mtu asimsahau Mwenyezi Mungu Mtukufu, vinginevyo atajisahau yeye mwenyewe. Sasa Ahl-ul-Bayt ﷺ nao wamesema vivyo hivyo. Imamu Ali رضي الله عنه anasema: “Mtu anayejitambua mwenyewe anakuwa amemtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu.”

Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu ameonesha kwa mintarafu ya upande wake.

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادٍ يَعْنِي فَإِنِّي قَرِيبٌ مُّطَّهِّرٌ

**“Waja wangu wanapokuuliza kuhusu Mimi, kwa hakika Mimi nipo karibu nao sana.” (Qur`ani Sura al-Baqarah 2:186)**

Halafu Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza bayana jinsi alivyo karibu na sisi.

أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ

**Mimi nipo karibu zaidi na nyinyi kuliko mshipa wenu wa shingo.**  
**(Qur`ani Sura Qaaf 50:16)**

Niombeni nitawaitikia. Lakini niiteni kwa moyo kabisa, na hata kabla hamjasema Mwenyezi Mungu Mtukufu tayari jibu la Labbaik litakuja.

Maulana Rum anaeleza kisa kinachohusu mtu mtakatifu, am-baye alikuwa na desturi ya kutaja jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu mchana na usiku. Siku moja Shetani alimwendea na akamuuliza:

kwa kipindi cha miaka arobaini umekuwa unataja jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu mchana na usiku, lakini umepata kupokea jibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hata mara moja? Mtu huyo akaanza kuhisi kwamba swali hilo ni sahihi; kwamba hajapata jibu hata mara moja.

Hisia hizo zilimpunguzia utakatifu wake na yeye mwenyewe akapunguza ibada zake na polepole, mwishowe akaacha kabisa ku-fanya ibada zote. Sasa akawa analala usiku wote bila kutaja jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu. Siku moja wakati akiwa usingizini aliulizwa kwa njia ya ndoto kwamba kwa nini aliacha kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa usiku, akajibu kwani kuna manufaa gani, kamwe sikupata jibu.

Akaambiwa kwamba yeye alikuwa mtakatifu kwa ulimi lakini alikuwa hajamtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Unaomba kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini huwezi kuhisi jibu. Hutambui kwamba kabla hata hujasema Mwenyezi Mungu Mtukufu jibu tayari linakuja kutoka Kwake. Sasa unajibu kwamba hisia hizo, fikra, maelekezo, usikivu vitu ambavyo vinakufanya wewe useme Mwenyezi Mungu Mtukufu, nani aliyeviweka vitu hivi moyoni mwako? Maumivu hayo, uchungu huo ambao ulikufanya umuite Mwenyezi Mungu Mtukufu nani amekukabidhi vitu hivyo? Wewe ni mtakatifu kwa ulimi lakini hujamtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama unataka kufika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu basi kwanza ujitalafakari wewe mwenyewe ndani mwako.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Hadith al-Qudsi kwamba, Yeye yupo ndani ya nyoyo zilizovunjika. Nyoyo zilizovunjika hairejelei zile nyoyo mbazo hazikutimiziwa ahadi zao. Maana ya nyoyo zilizovunjika ni zile nyoyo zilizo laini na pole. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema Yeye yupo ndani ya nyoyo zilizo laini na

anapatikana katika nyoyo hizo. Mtu fulani alimuuliza Imamu ﷺ kwamba kuna umbali gani baina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Binadamu? Imamu akasema, ni sawa na umbali wa mvuto wa pumzi ya mtu anayekandamizwa. Ni kitu gani hicho ambacho humo ndimo Mwenyezi Mungu Mtukufu yumo?

Ni Fitra ya binadamu. Nenda uanze kuitafuta Fitra, na siku utakapoikuta Fitra yako, utamuona na Mwenyezi Mungu Mtukufu pia. Husein ؓ ni kiongozi wa Fitra. Tunatakiwa kuwa watu wa kushukuru kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amefanya jina la Husein litoke kwenye ndimi zetu. Huu ni uthibitisho kwamba Fitra zetu zipo hai.

### **Neno “Fitra”:**

Neno Fitra halionekani katika lugha nyingi. Neno Fitra pia halikuwepo katika lugha ya Kiarabu kabla ya uwepo wa Qur`ani Tukufu. Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza Qur`ani Tukufu ilitumia neno Fitra katika maana hii. Katika lugha ya Kiarabu; *Faatir, Fatr, Maftuur*, ni maneno yaliyotumika katika maana halisi. *Fitri, Fatr*, katika lugha ya Kiarabu maana yake ni “kufungua.” Katika lugha ya Kiarabu maneno yote yana familia kubwa. *Iftar* pia lipo katika familia hiihii, ambalo maana yake ni kufungua swaumu. Kufunga swaumu huanza kwa kutia nia na humalizika kwa kutia nia, lakini katika utamaduni wetu swaumu huanza na aina moja ya chakula na kumalizika kwa aina nyingine ya chakula. *Iftar* maana yake ni kufungua. Mdomo ulifungwa na sasa umefunguliwa. *Faatir* maana yake ni yule anayefungua. *Maftur* maana yake ni kile kitu ambacho kimefunguliwa. *Fatr* maana yake ni kitu kimoja kizima ambacho kimegawanywa katika sehemu mbili (kama kufungua mlango kitendo hicho sio *Fatr*).

Ibn Abbas alikuwa Sahaba mashuhuri aliyeleshimiwa wa Mtukufu Mtume ﷺ na wa Imam Ali ؓ pamoa na kwamba katika awamu yake ya mwisho katika maisha yake alionesa uvivu fulani akiwa na Imam Ali ؓ. Kitu cha muhimu ni mwisho (*Aqibat*). Ni mtu msomi aliyeandika Tafsiri ya kwanza ya Qur`ani Tukufu. Anasema kwamba alikuwa hatambui kuhusu maana ya neno Faatir pamoa na kwamba alikuwa bingwa wa lugha ya Kiarabu. Anasema kwamba siku moja Waarabu wawili wa kabilia la Bedui walimwendea wakawa wanazungumza Kiarabu kile cha ndani kabisa. Anasema kwamba hawa Waarabu wawili walikuwa wanagombania kisima cha maji kwamba ni nani baina yao aliyekuwa mmiliki halali wa kisima hicho. Mmojawao alisema “*Ana Fatartuha*”; maana yake ni; mimi ndiye nimefungua kisima hiki (yaani kwa mara ya kwanza). *Fatar* maana yake ni kitu kilichofunguliwa kwa mara ya kwanza. Ibn Abbas akasema alielewa kwamba *Fatr* maana yake ni kufungua kwa mara ya kwanza kufuatana na msamiati.

Neno linaweza kuundwa katika lugha yoyote lakini maneno yanaweza kusafiri pia. Maneno huzaliwa, hulelewa, hukua na halafu hupita katika safari. Safari mojawapo ambayo maneno huchukua ni kwamba maneno yanazaliwa kwenye lugha moja na halafu yakiwa katika safari huingia kwenye elimu na hugeuka kuwa misamiati. Kama ilivyo kwa misamiati yote inayotumiwa kwenye kompyuta, ni maneno yaliyozeeka lakini yamekuwa misamiati ya kompyuta. Kama Kipanya linatumika katika kompyuta; leo hii tunaposema panya, kinachokuja akilini mwetu ni panya ya kompyuta. Maneno yote yako hivi. Kama vile *Salaat* katika msamiati ni Dua, lakini linapotumika katika Qur`ani Tukufu linageuka kuwa na maana ya swala. Hatuwezi kuielea Qur`ani kwa kutumia kamusi; kwa kweli kamusi wala haisemi kuhusu maneno ambayo yametumiwa katika Qur`ani Tukufu. Kamusi hurejelea tu jinsi neno lilivyozaaliwa. Hurejelea kwenye makazi ya

neno; kamusi haiwezi kusema neno hili limefika wapi leo hii. Taarifa hiyo inaweza kutolewa na sayansi mbalimbali. Ziulize sayansi ma-neno yanasmama wapi leo. Baadhi ya maneno yaliacha kamusi na kuingia kwenye sayansi, lakini baadhi ya maneno yaliondoka na kuin-gia kwenye dini. Maneno fulani yalitumika kwenye utamaduni kabla ya kutumika kwingineko, lakini pale ambapo Qur'ani ilitumia maneno haya, yaligeuka kuwa maelezo ya itikadi.

Sasa, Waarabu walikuwa wanatumia neno *Fatar* katika maana ya kuchimba visima au kumamanua tende, lakini lilipotumiwa na Qur'ani lilitumika kwa ajili ya uhalisia mwengine. Uhalisia ambao ulikuwa uanzishwe na maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; uhalisia wa dini kufanywa ueleweke kwa binadamu. Uhalisia wa dini unapotakiwa kuelezewa kwa binadamu; kama maelezo hayo yaki-fanywa katika lugha ya dini basi ni hao tu wanaolewa lugha ya dini wanaoweza kuelewa. Kwa hiyo kwa watu wa kawaida uhalisia una-takiwa kuelezewa katika lugha inayoweza kueleweka kwa mtu wa kawaida. Kama isemavyo Qur'ani Tukufu, Kitabu kilikuwa katika hali ya Kiarabu: ulinzi; ambapo ni wale viumbe watakatifu tu ndio wangekigusa. Sasa ikawa kifanywe kwa ajili ya watu wa kawaida, kwa hiyo kilifunuliwa (*Nuzuul*). Maana ya neno *Nuzuul* ni kurahis-i-sha kitu hadi kieleweke kwa watu wa kawaida. Sasa Qur'ani Tukufu imekuja katika lugha yetu ili tuweze kuielewa.

Hivyo *Fatr* maana yake ni kufungua kitu kama vile kumamanua mbegu. Kwa nini Fitra inaitwa *Fatr*; kwa sababu Mwenyezi Mun-gu Mtukufu alifungua pazia la kutokuwepo, na uwepo ukapatikana kutokana na hili. Kwa kuwa uumbaji maana yake ni kupata uwepo kutokana na kitu kisichokuwepo, ambapo maana yake ni kumaman-ua kutokuwepo na kuleta uwepo, kwa hiyo mtindo huu wa *Khilqat* (uumbaji) unajulikana kama Fitra.

### **Fitra ni mtindo wa *Khilqat* (Uumbaji):**

Ile namna ya alfabeti zilivyopangwa ni nzuri sana pia Kiarabu: Hali yetu ilivyo ni kwamba sisi tunapamba miili yetu na nyumba zetu lakini hatufanyi lolote kuhusu Fitra. Ni sawa kama vile bibi harusi anangojea kupambwa lakini wanawake wanaotakiwa kumremba bibi harusi wanajipamba wenyewe kwanza.

Lipo neno moja zaidi ambalo lina uzito sawa na neno Fitra, yaani *Siira*. Siira maana yake ni kutembea. Ni neno la Kiarabu lakini tatizo letu ni “*Zabaane Yaare Man Turki, man Turki namidaanam.*” Tafsiri yake: “Lugha ya rafiki yangu ni Kituruki na mimi sijui Kituruki.” Hatujui lugha ya rafiki yetu.

Katika lugha ya Kiarabu, pale ambapo maneno kama Fitra, *Siira*, Jilsat, Riqbat; hutengenezwa katika mfuatano kama huo, yanakuwa na maana malumu ambayo inaelezea aina na mtindo wa kitu. *Sair* maana yake ni kutembea, lakini *Siira* maana yake ni mtindo wa kutembea. Maisha ni *Sair* sio *Siira*. Watu huandika *Siira Nabawi*, yale aliyofanya Mtukufu Mtume ﷺ wakati wa uhai wake. Mtume alioa wanawake 11, kwa hiyo na wewe ufanye hivyo pia kama hiyo ni *Siira*. Alichofanya Mtume ﷺ kilikuwa ni kitendo cha Mtume hii sio *Siira*; Siira ni jinsi alivyofanya hivyo. Mtume ﷺ alikula tende. Kula tende sio *Siira*, lakini kula kitu chochote jinsi alivyokula Mtume ﷺ ni *Siira*. Maana ya *Sair* ni maisha na *Siira* ni mtindo wa maisha.

Watu wanasema tunatakiwa kufuata *Siira* ya Maimamu ﷺ kwa hiyo hivi tunatakiwa kuacha kuvalaa nguo zetu na kwa hiyo tuanze kuvalaa nguo za Kiarabu tu? Hii sio Sira kwamba tunatakiwa kuvalaa nguo kama zile alizokuwa anavaa Mtume. Mtu anatakiwa kuvalaa nguo za zama zake. Tumia gari ya zama zako, kula chakula cha zama zako. *Siira* ya Mtume ﷺ sio kuketi kwenye ngamia; *Siira* ni mtindo wa

kuketi juu ya ngamia. Chukua maisha ya wakati wako, lakini mtindo unatakiwa uwe ule wa Mtume ﷺ. Tumekuwa tukitafsiri Historia kama Siira kwa makosa.

*Siira-e-Risallah* ni mtindo wa kuishi maisha. Yale ambayo ali-kuwa akiyasema Mtukufu Mtume ﷺ wakati wa uhai wake pia na wewe unatakiwa kusema hayo lakini hiyo sio *Siira*; unazungumza kuhusu masuala ya zama zako; lakini mtindo wa kuzungumza unatakiwa uwe kama ule wa Mtume. Unaitazama dunia kwa maono kama yale ya Mtume ﷺ. Ipo milango mingi ambayo hatujaitambua, kwa hiyo ni baina yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu; milango hiyo imefungwa. Lakini mlango mmoja ambao umefunguliwa kwa ajili yetu ni mlango wa Sira, ambao tumeufunga sisi wenyewe na sisi tunasimama katika mistari mbele ya milango ile ambayo imefungwa. Tumekwisha kuambiwa kwamba tukienda karibu na milango ile hautafanikiwa chochote. Kama ukichunguza *Wilayat-e-Taqwiin* na uendelee kujifunza fani hiyo katika maisha yako yote, hautafanikiwa chochote kutoka humo kwa sababu fani hiyo ni kipimo mahsus Cha maisha ya Maimamu ﷺ lakini mtu hawezikukitambua kipimo hicho. Kipimo hicho ni kwa ajili ya Maimamu ﷺ tu. Mlango wa *Siira* umefunguliwa kwa ajili yetu. Tunahitaji kuingia kupitia mlango huu. Katika *Wilayat-e-Taqwiin* chochote kile tunachokijua kuhusu fani hiyo inatosha; tusijaribu kuvuka mpaka huo. Wale wanaojaribu kuingia kupitia mlango huo huchanganyikiwa na halafu huwachanganya wengine. Wale waliokwenda kwenye milango hii iliyofungwa; ama walizuka kuwa *Nasibi* au *Ghali*, na Imam Ali ؓ anasema kwamba “Aina mbili za watu wataangamia kuhusu mimi, aina moja ni wale ambao wananchukia mimi na aina nyingine ni wale ambao hutia chuku katika hayo niyasemayo mimi.”

Ingia kupitia mlango wa *Siira* ambao ni mlango ulio wazi na uone jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyoyafanya mazuri. Kula

chakula, kujifunza, kuzungumza, kuketi, yote hayo ni maisha lakini mtindo wa haya ni *Siira*.

Fitra (Hali ya kimaisha) sio *Khilqat* lakini ni mtindo wa *Khilqat* (uumbaji); kama ambavyo imesemwa katika mstari sawa wa *Sair* na *Siira*. Sawa na *Jilsat* ambayo huja kutoka *Jalsa* ambalo maana yake ni kuketi; lakini *Jilsat* maana yake ni mtindo wa kuketi. (Kwa ajili yetu *Juluus* maana yake ni kutembea lakini kwa lugha ya Kiarabu *Juluus* maana yake ni kuketi). Kama unaketi kwenye jamvi la kulia chakula, Tashahud, majlis vyote hivyo ni vikao vyenye aina maalumu ya kuketi. Wewe unaketije. Mwarabu anasema *Jilsata Ali*, sawa na kusema nimeketi kama alivyoketi Ali.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ni muumbaji wa kila kitu, lakini ilipowadia zamu ya kumuumba binadamu, Mwenyezi Mungu Mtukufu alibadili mtindo wa uumbaji. Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa anaumba kila kitu kufuatana na kanuni fulani. Uumbaji wa Malaika ulifanyika kwa kufuata baadhi ya kanuni mahsusii. Mbingu na ardhi zilumbwa kufuatana na taratibu fulani. Lakini ilipofika zamu ya kumuumba binadamu, Mwenyezi Mungu Mtukufu alibadili mtindo wa uumbaji na alimuumba binadamu kwa mtindo maalumu.

Mathalani mtu anakwenda kwenye kiwanda cha kuoka mikate na anatengeneza mkate mpya kwenye oveni; anatengeneza donati na kuoka mkate. Lakini akifika hapo rafiki wa karibu wa mweyne kiwanda cha kutengeneza mkate, mtindo wake wa kutengeneza donati utabadilika. Vivyo hivyo mtu akienda kwenye duka la nyama la rafiki yake, mwenye duka hilo atamkatia rafiki yake nyama nzuri sana; atabadili mtindo wake wa kukata nyama. Kwenye mkusanyiko mtu anasalimiana na watu na kupeana mikono, lakini atakapomuona rafiki yake wa karibu na anayemjua, atabadili mtindo wa kusalimiana. Hii inaonesha kwamba mtu ambaye amefika hapo ni mtu tofauti.

Upendeleo, “*Karamat*” (uadilifu/ubora) wa Binadamu kuliko viumbe wengine:

Kama ambavyo imetamkwa katika aya ya 30 ya Surah Rum kwamba tumemuumba binadamu kutokana na Fitra na hii ni dini ya sawasawa ambayo imeasisiwa kwa ajili ya binadamu, jambo ambalo watu wengi hawajui. Fitra ni kitu cha thamani cha Mwenyezi Mungu Mtukufu ambacho alikabidhiwa binadamu, ambacho ndicho kimemfanya binadamu apate upendeleo akilinganishwa na viumbe vingine.

Baada ya kuanzisha kitu hiki cha thamani kiitwacho Fitra, pia Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema kwamba watu wengi hawajui jambo hili. Dini ilioanzishwa, iliyonyooka na ya sawasawa ni dini ya Fitra. Uhalisia wa binadamu ni kitu hiki cha thamani cha Fitra ambacho Mwenyezi Mungu Mtukufu amemkabidhi binadamu. Ni kupitia kwenye hii Fitra ambamo binadamu ametofautishwa na kuzidishiwa heshima kama akilinganishwa na viumbe vingine vyta Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema tumewapendelea wana wa Adam, na hii ni kwa msingi wa kitu cha thamani cha Fitra ambacho kipo ndani ya binadamu na hakipo katika kiumbe kingine chochote. Malaika, wanyama na viumbe wengine hawakupewa Fitra.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema tulitoa nafasi ya dhamana kwa viumbe wengine wote.

إِنَّا عَرَضْنَا الْأُمَانَةَ عَلَى السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلُنَّهَا  
وَأَشْفَقُنَّ مِنْهَا وَحَمَلُهَا إِنْسَانٌ إِنَّهُ كَانَ ظُلُومًا جَهُولًا

**“Kwa hakika tulizitolea amana mbingu na arди na milima na vi-kakataa kuichukua na vikaiogopa, lakini mwanadamu akaichukua. Hakika ye ye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana.”**

**(Surah Ahzab, 33:72)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema tulitoa amana kwa mbingu, milima, ardi lakini vyote vikakataa kuichukua amana hii, na vili-iogopa baada ya kuiona amana hiyo. Viumbe hivi havikufanikiwa kuwa Amiin (wadhamini) wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Binadamu alijitokeza na akachukua amana hii. Lakini binadamu ni mijinga na anajidhulumu mwenyewe. Binadamu hajui amebeba wajibu mkubwa kiasi gani mabegani mwake.

Fitra ni kitu cha thamani cha kweli cha binadamu ambamo humo ndimo utu wa binadamu umehifadhiwa. Kama kitu hiki cha thamani kikitelekezwa si tu kwamba hadhi ya binadamu inashuka lakini pia badala yake binadamu huutupilia mbali utu wake.

Vipo vitu vingi ambavyo binadamu huvifikiria isivyo sahihi. Wanadamu ni watu wa kidini lakini dini sio ilani ya maisha yao. Binadamu ni watu wa kiutamaduni, wanaishi maisha kufutana na utamaduni na katika utamaduni huu tunachanganya kiasi kidogo cha dini sawa na kiasi kidogo cha chumvi katika unga. Tunahakikisha kwamba haiwekwi chumvi ya kuzidi kiasi ndani ya chakula. Tumechukua kanuni hiyo hiyo ya matumizi ya chumvi hata kwenye dini pia. Katika miaka sitini ya uhai wetu dini ilikuwa sawa na chumvi ambapo maisha yote yalitumiwa katika njia ya kiutamaduni.

Baadhi ya binadamu wana dini katika njia ambayo wakati anazaliwa adhana iliadhiniwa masikioni mwake na mtu fulani; halafu wakati wa ndoa Maulana alisoma Nikah, na wakati wa kifo mtu fulani aliswalisha swala ya maiti. Baadhi yao huongeza hata swala ya Iddi pia na baadhi ya wengine huvuka mpaka na kuhudhuria Majlis. Watu huwa wanahakikisha kwamba hawaendi mbali zaidi ya hapo katika dini, kwa sababu kama tutafanya hivyo kama shinikizo la

damu, shinikizo la maisha litaongezeka. Kama mume anataka kuwa karibu na dini mke anamzuia; kama mke anataka kuwa karibu na dini mume anamzuia. Kama mtu anasimamisha swala katika Jamaat, watu wanaanza kusema mtu huyo amekuwa Maulana.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia binadamu *Sharaf* (hes-hima) na *Karamat* (uadilifu). Katika lugha ya Kiarabu neno Karamat linatokana na neno Karam na Karam ni sifa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; na mionganini mwa *Asma-e-husna* ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *Kariim*. Imetajwa katika hadithi kwamba kama mtu amepatwa na tatizo kubwa ambalo linafanya maisha yake kuwa ya shida, basi mtu huyo awe anamdhukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa jina hili la *al-Kareem*. Hata kama mtu yupo katika tatizo kubwa sana na kisha anamdhukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa jina la *Ya Kareem* kwa moyo wote na safi, Mwenyezi Mungu Mtukufu atatatta tatizo lake. Changamoto ni kutamka jina hilo kwa ikhlas, ambapo maana yake ni kwamba uwepo wote wa mhusika unatakiwa kuwa pale na pia vitendo vya mhusika vinatakiwa kuwa safi.

Kama vile ambavyo mtu mmoja alimwambia Mwanazuo wa Ki-islamu aswali *Salaate-Istisqa* ili mvua inyeshe. *Istisqa* ni swala in-aswaliwa wakati wa ukame ili mvua inyeshe; hii ni desturi ambayo dini imefundisha kuhusu uhudhuriaji mahsusini mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ili Mwenyezi Mungu aweze kuleta neema Yake. Mwanazuo huyo aliwaambia watu waende kwenye uwanja ulio wazi mnamo siku ya Ijumaa, na kwamba yeye angeongoza swala hiyo. Watu walipokusanyika mahali hapo mwanazuo aliwaambia watu kwamba walidai yeye aongoze swala ya Istisqa na kumwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu alete mvua. Pamoja na kwamba ninyi mmeniambia niswalishe swala ili Mwenyezi Mungu Mtukufu alete mvua lakini ninyi wote hamna imani kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hamna imani na uhakika juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu

Mtukufu. Watu hao wakajibu kwa kusema kwamba wao walikuwa na imani na uhakika kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu angeleta mvua. Mwanazuo akasema kwamba kama watu hao wangekuwa na uhakika kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu angeleta mvua sasa kwa nini walikwenda mahali hapo bila ya kubeba miavuli yao? Wao kwenda mahali hapo bila ya kubeba miavuli ni sawa na kusema wao walikuwa na uhakika kwamba mvua haingenyesha. Ni sawa na kucheza mchezo wa karata kwamba labda wajaribishe kwamba kwa swala hiyo ingewezekana mvua kunyeshaa.

Mtu mwenye uhakika kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Karimu na kwa uhakika huu pale anapodhikiri *Ya Kariim*, haiwezekani kwamba bahari ya Ukarimu huu haithibitiki. Hata kama moyo mmoja uliolaini ukitamka ‘*Ya Kariim*’ upo uwezekano kwamba wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu utadhihirika ndani ya moyo wote.

Karamat linatokana na neno hili la Kariim, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa cheo cha Kariim kwa kila kitu adhimu kama vile *Rasuul-e-Kariim*, *Qur`ani-e-Kariim*, *Khuda-e-Kareem*. Wakati Waarabu wanapotaka kumpandisha mtu cheo ili awe na cheo cha juu zaidi, humuita mtu huyo kwa cheo cha Kariim. Abdul Muttalib ali-kuwa mtu mashuhuri kama *Kariim-e-Arab* Na katika dhuria wa Abdul Muttalib mtoto mmoja wa kiume, Imamu Hassan  amepewa cheo cha *Kareem-e-Ahlul Bayt*. Karamat maana yake ni umashuhuri, uadilifu, ukubwa kabisa kwa umri na kuheshimika. Wakati sifa fulani zinapokusanyika pamoja basi inakuwa Kariim. Kinyume cha Kariim ni *Laiim* na maana yake ni aliye fedheheka, aliye dhalili na wa hali ya chini.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemkabidhi binadamu Karam na Sharaf (uadilifu) juu ya viumbe vingine vyote na msingi wa hii Karamat ni Fitra ya binadamu. Hii ni kwa sababu licha ya Fitra, vitu vingine viro kwa binadamu na kwa viumbe vingine.

## Mipango ya kutunza Fitra inaonesha Umuhimu wake:

Dini imewasilishwa kwa Fitra (Hali ya kimaumbile) ya binadamu, kwa hiyo Imamu Ali ﷺ anasema yawasilishe maneno yetu jinsi yalivyo na Fitra iliyo safi itayakubali. Fitra ni kitu cha thamani ambacho kinahitaji usalama wa hali ya juu na ulinzi, kwa sababu hatari pia ni nyingi. Fitra inastahili kutunzwa na pia inawezekana ikaharibiwa. Fitra huwa haifariki lakini huhinikizwa.

Mtu anatakiwa kuanza kuielewa Fitra kwa namna ya utambuzi (*Maarifat*), kwa sababu kitu chochote kinachoanza na Utambuzi hufika kwenye mwisho wake. Inatakiwa kila kitu kianze kueleweka kwanza kwa namna ya Utambuzi (*Maarifat*). Hii ni kwa sababu Amiri wa Waumini, Imamu Ali ﷺ ambaye ni Imamu wa Fitra anasema: "Kitu cha kwanza kabisa katika dini ni kumtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu (*Maarifatahu*)."<sup>1</sup> Kwanza tumjue Mwenyezi Mungu Mtukufu kabla ya kumwamini, pia kabla ya kutaja majina ya Maimamu ﷺ tunapaswa kwanza tuwatambue.

Kwa kuangalia katika mipango ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amefanya kwa ajili ya malezi ya Fitra tunaweza kutambua maana na umuhimu wake. Hadhi ya kitu huonekana pale ambapo mipango yake inafanya. Sasa natuangalie mipango ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya kawa ajili ya Fitra, na kutokea hapa tunaendelea mbele, tutaweza kupendezewa na mipango ambayo imefanya kwa ajili ya Fitra.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwachagua watu wazuri sana kutoka katika jamii yote ya duniani. Aliwapa Umaasumu; akawakamilisha; akawapo elimu; akateremsha ufunuo kwao na akateremsha vitabu vya dini kwao. Mtu anapomvisha mwanae nguo anajua kule anakotaka kumpeleka mtoto wake. Mtu anapovishwa kati, vazi la kujihami wakati wa mapigano, upanga na mkuki; kwa matayarisho

haya mtu anajua anataka kumpeleka mpiganaji kwenye uwanja wa vita.

Miongoni mwa viumbe vyote Mwenyezi Mungu Mtukufu ali-wachagua wanadamu, aliwateua Mitume, miongoni mwa Mitume alimteua Mtukufu Mtume , kutokana na Mtukufu Mtume aliwateua dhuria wake, kutokana na dhuria wake aliwateua Maimamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alianza kuwatayarisha kwa kuwapa ujuzi wa kimungu, utakaso, na aliwatumma malaika kwenda majumbani mwao. Kutokea hapa tunajua kwamba hawa wanatumwa kwa ajili ya lengo fulani. Lengo hili ni lipi? Ni kwa ajili ya Tabiyat (matunzo) ya Fitra ya binadamu.

Uzito wa Rustom hauwezi kuinuliwa na kila farasi, anahitajika farasi aitwaye Raksh (farasi maalumu wa Rustom). Imamu Ali  anasema kama watu wajinga watanyamaza, nusu ya matatizo yatatatuliwa, na nusu nytingine ya matatizo itatatuliwa kama wanazuoni wataanza kuzungumza. Kwa hiyo kama wanazuoni watavunja kimya chao na wajinga wanyamaze matatizo yote ya dunia yatatatuliwa. Masuala mengi yamejitokeza kwa sababu hii; kwamba wale ambao walitakiwa waseme wapo kimya na wale wanaotakiwa kuwa kimya wanasesma.

### **Upana wa Ulimwengu:**

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaumba wanadamu miongoni mwa viumbe wengi miongoni mwa ulimwengu huu, na baada ya kuwaumba wanadamu aliwakabidhi Fitra ambacho ni kitu chenye thamani kubwa sana, na kutokana na kitu hiki chenye thamani kubwa sana, binadamu amekuwa ndiye kiini cha ulimwengu. Sasa na tuangalie upana wa ulimwengu huu ambao kiini chake ni Fitra ya wanadamu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaumba Malaika, ulimwengu, majinni, na akaumba ulimwengu mpana sana hivyo kwamba kama tukitulia na kuanza kufikiri inaweza kuchukua maelfu ya miaka na bado hatutaweza kufahamu upana wa ulimwengu.

Maulana Rum anasema, mfano wetu ni kama vile kuna shamba kubwa la mita 1000 lenye miti 1000, kila mti una matawi 1000, kila tawi lina majani 1000, na kwenye jani moja, upande moja wa jani hilo anaishi mchwa ambaye wala hajawahi kufika upande wa pili wa jani hilo. Kama mchwa huyu akiulizwa ukubwa wa bustani hiyo; mchwa atasema ni ule wa jani ambalo ndimo anamoishi. Asichojua mchwa huyu ni kwamba kwenye tawi hilo yapo majani mengine 1000 na yapo matawi mengine 1000 kwenye mti huo na ipo miti mingine 1000 kwenye bustani hiyo na zipo bustani nyingine 1000 za aina kama hiyo, kwa hiyo mchwa huyu atajuaje kama yupo mmiliki wa bustani hiyo pia.

Ulimwengu ni mpana sana na ndiyo sababu tunapaswa kuswali *Salaatul Layl* (swala za usiku), na ipo mbinu ya kuswali swala hiyo. Alikuwepo kijana mmoja ambaye mtu fulani alimhubiria kuhusu swala ya usiku. Aliamka wakati wa usiku wa manane na alitaka kumuonesha kila mtu kwamba ye ye anaswali swala ya usiku. Kwanza aligonga mlango lakini hakuna mtu aliyeamka; halafu akagonga nyungu ya maji lakini kila mtu alikuwa kwenye usingizi mzito. Hatimaye aliswali swala ya usiku na akalala na halafu alipoamka akataka kila mtu ajue kwamba ye ye aliswali swala ya usiku. Wakati wa kunywa chai ya asubuhi alianza kwa kunywa maji mengi sana; alikunywa jagi lote la maji. Mama yake akamuuliza, kitu gani kimemtokea na kusababisha anywe maji mengi kiasi hicho, wakati wa chai ya asubuhi anakunywa jagi lote la maji. Kijana huyo akajibu “Hakika uchovu unaosababishwa na swala ya usiku unahitaji jagi lote la maji asubuhi.” Kwa kiasi fulani alitoa taarifa kwamba aliswali swala ya usiku.

Hii haiwezi kuwa kusudio la swala ya usiku, swalı swala hiyo wakati kila mtu amelala. Halafu toka nje, tazama juu mbinguni na uzione nyota zile zinavyomeremeta, halafu jitafakari wewe mwe-nyewe. Mimi ni chembe ndogo kwenye sayari hii ndogo. Dunia hii yetu pia ni chembe ndogo katika ulimwengu huu mpana. Tunaishi katika chembe hii ndogo, ambamo yapo mabara, katika mabara hayo zipo nchi nyingi. Halafu ipo nchi moja, ndani ya nchi hiyo lipo jiji, katika jiji hilo kipo kitongoji, katika kitongoji hicho upo mtaa, katika mtaa huo lipo ghorofa na katika ghorofa hilo zimegawanywa nyumba (*flats*) na ndani yake kipo chumba cha kulala, na ndani ya chumba hicho kipo kitanda kidogo na kwenye kitanda hicho yupo huyu mtu mkubwa anayefikiri kwamba hakuna mtu mkubwa zaidi yake katika ulimwengu huu. Huu ni uelewa wa ulimwengu ambao watu wanatakiwa kuwa nao, kwamba wao ni viumbe wadogo wakil-inganishwa na upana wa ulimwengu, lakini bado Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapa wao kitu hiki cha thamani kijulikanacho kama Fitra ambacho ni upendeleo kwao.

Kwa nini nyoyo zetu haziwi laini, kwa nini shingo zetu zimekuwa ngumu na haziinami chini? Hii ni kwa sababu hatutambui kwamba sehemu hii ambamo tunaishi ni pana sana. Kuvunja majivuno yetu na jeuri yetu ni vema kuswali swala ya usiku na halafu kutoka nje na kutazama juu mbinguni na kuona kwa uhakika kwamba kila nyota ni kubwa mara kadhaa kuliko hii dunia yetu, na zipo nyota ngapi za aina hiyo katika galaksi. Kama dunia hii ya kimaumbile kamwe haioneshi kufika mwisho wake sasa basi vipi kuhusu dunia nyingine ambamo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba huu sio ulimwengu wote, ambayo uwepo wake ameumba Yeye ni kama mpepeso wa macho, kuona mara moja tu.

وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا عِنْدَنَا حَزَانُهُ وَمَا نُنَرِّلُهُ إِلَّا بِقَدْرٍ مَعْلُومٍ

**“Na hakuna chochote ila hazina yake iko Kwetu na wala hatukiter-emshi, isipokuwa kwa kipimo maalumu.” (Surah Hijr, 15:21)**

Tumechukua yote haya kutoka kwenye chanzo kwa kiasi kidogo sana.

### **Mwenyezi Mungu Mtukufu Alibadili mtindo wa Uumbaji:**

Ulimwengu ulio mkubwa kabisa kuliko mwingine wowote ni ule uitwao *Alam Al-Malqoot* (dunia isiyooonekana). Kwanza Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba *Alam Al Malqoot* na kutokea hapo akaanza kuumba *Alam Al Mulk* (dunia inayooonekana). Aliumba galaksi, nyota, sayari, mfumo wa jua na sayari zake na halafu akaumba dunia hii yetu na katika dunia hii akaumba mamilioni ya viumbe lakini vyote vilumbwa kwa mtindo sawa. Lakini baada ya kuumba vyote hivi, wakati zamu ya kumuumba binadamu ilipofika Mwenyezi Mungu Mtukufu alibadili mtindo wa uumbaji. Kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu alibadili mtindo wa uumbaji? Kwa sababu alikuwa anaumba asili ya viumbe vyote; alikuwa anataka kumuumba yule ambaye viumbe vyote vilumbwa kwa ajili yake.

“Yule ambaye nimeviumba vitu vyote kwa ajili yake sasa ninamuumba ye.”

Na mtindo huu ulibadilika kwa jinsi gani? Mtindo huu umetam-kwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenyewe katika Surah Mu`minun.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِّنْ طِينٍ

**“Na hakika tumemuumba mtu kutokana na asili ya udongo.” (al-Mu`minun; 23:12)**

ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ

**“Kisha tukamjaalia awe tone katika makao yaliyo makini.” (23:13)**

Tuliumba tone la manii ya mtu kutokana na asili ya udongo; halafu tukaliweka tone hilo katika makao yaliyo makini (nyumba ya uzazi).

ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْعَغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْعَغَةَ عَظَامًا فَكَسَوْنَا  
الْعِظَامَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ حُكْمًا آخَرَ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**“Kisha tukaumba tone kuwa pande la damu na tukaliumba pande la  
damu kuwa pande la nyama, na pande la nyama tukaliumba kuwa  
mifupa na mifupa tukaivika nyama. Basi ametukuka Mwenyezi  
Mungu; Mbora wa waumbaji.” (Surah Mu`minun, 23: 14)**

Kisha tukaumba tone kuwa pande la damu, na tukaliumba pande la damu kuwa pande la nyama, na pande la nyama tukaliumba kuwa mifupa na kisha tukaifunika kwa ngozi, kisha Mwenyezi Mungu akafurahi sana na hivyo akasema kwamba.

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.  
(Sura al-Mu'minoon 23:14)**

Ni Mola yupi huyu ambaye alituumba sisi katika hali nzuri sana hivyo kwamba tunapaswa kufichua siri kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu anajipongeza mwenyewe. Ni uzuri gani huu wa pekee katika uumbaji wa binadamu ambao umemfanya Mwenyezi Mungu Mtukufu ajipongeze mwenyewe.

Katika Surah Tiin anasema:

وَالنَّبِيُّنَ وَالرَّبِيعُونَ

“Naapa kwa tini na zatuni!” (Sura at-Tin 95:1)

وَطُورَ سِينِينَ

“Na kwa mlima Sinai” (Sura at-Tin 95:2)

وَهُدًى الْبَلْدِ الْأَمِينِ

“Na kwa mji huu wengine amani!” (Sura at-Tin 95:3)

لَقَدْ خَلَقْنَا إِلْأَسْنَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ

“Hakika Tumemuumba mtu katika hali nzuri mno.”  
(Sura at-Tin 95:4)

Kwa mara nyingine hapa Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya kua-pa kwa Tini na Zaituni, anasema tena kwamba amemuumba binadamu katika hali nzuri sana. Hii hali nzuri mno ni inayoendana na mtindo wa uumbaji ambao umetajwa kabla katika Surah Mu`minun. Mwenyezi Mungu Mtukufu alichukua mtindo mpya wa uumbaji, na mtindo huu mpya na wa pekee wa uumbaji ambao ni wa pekee kususiana uumbaji wa vitu vingine vyote na ambao ni mahsusisi kwa uumbaji wa binadamu, uumbaji huu wa pekee unajulikana kama Fitra ya binadamu

Sasa inaonekana kwamba wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu alipobadilisha mtindo Wake wa uumbaji na akawaumba wanadamu kuwa viumbe maalumu sana, sasa ni zipi hizo sifa maalumu zilizopo ndani ya binadamu na ambazo hazipo katika viumbe vingine. Kuna tofauti gani baina ya hii mitindo miwili? Wakati siri hii itakapoju likana hapo ndipo itakapofahamika Fitra ni nini, halafu ndipo binadamu atakapohuisha, kuilea na hata kuitoa mhanga pia hiyo Fitra.

Halafu binadamu atakubali njia ya Fitra, kitabu cha mwongozo kwa ajili ya Fitra na pia hapo ndipo binadamu ataanza kuwatii na kuwafuata Viongozi wa Fitra. Halafu ndipo binadamu ataelewa mapambano ya Fitra kama yale ya Karbala.

### **Falsafa ya Kujipongeza Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

Fitra ipo katika mkondo wa *Siira*, ambapo *Siira* ni mtindo wa misha, ambapo Fitra ni mtindo wa uumbaji. Asili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Muumbaji wa kila kitu na aliumba kila kitu kufuatana na kanuni za uumbaji ambazo hakuzibadilisha kwa mitindo yote ya uumbaji. Lakini ilipofika zamu ya kuumbwa kwa binadamu Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba kwa kanuni zilezile za uumbaji lakini mtindo wa uumbaji ulibadilika. Palikuwepo na viumbe vingine vingi kama Malika, Majinni na viumbe vingi ambavyo havijahamika hapa duniani vilikuwepo kabla ya binadamu. Lakini ilipofika zamu ya uumbaji wa binadamu Mwenyezi Mungu Mtukufu akabadilisha mtindo wa uumbaji.

Aina tofauti za wanyama ambao idadi ya aina zao pia haiwezi kuhesabika wote wameumbwa chini ya kanuni moja mahsusini ya uumbaji, pamoja na kwamba aina zao zinatofautiana. Lakini ilipofika zamu ya uumbaji wa binadamu Mwenyezi Mungu Mtukufu alibadili mtindo Wake wa uumbaji na alimuumba kiumbe wa pekee na wa kisanii. Hii ilikuwa kazi moja bora sana ya uumbaji hivyo kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliipongeza asili yake mwenye..

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.**  
**(Sura al-Mu'minoon 23:14)**

Baadhi ya watu wana kipaji cha kumamanua aya za Qur'an Tukufu; hupachika maono ya kwao wenyewe katika Qur'an Tukufu na kufanya tafsiri za kwao. Katika *Nahjul-Balaghah* Imamu Ali رض anasema kwamba Qur'an Tukufu ni Imamu wako (mkuu na kiongozi) wako na hutakiwi kuwa Imamu wa Qur'an Tukufu. Isije iwe kwamba unafikiri na kujaribu kupata uthibitisho wa maono yako kutoka katika Qur'an Tukufu. Mtu hatakiwi kuifanya Qur'an Tukufu imfuate yeye badala yake mtu anatakiwa kuifuata Qur'an Tukufu na kwenda kule iendako. Hali ni hiyohiyo kwa Ahlu Bayt رض mtu achukue kutoka kwao asijaribu kutoa pendekemo na kuwapa kitu, hii ni kwa sababu ombaomba huchukua kutoka kwa matajiri. Ahlul Bayt رض sio tegemezi kwa watu badala yake watu ndio wategemezi kwao; kwa hiyo ni kitu gani tunachotakiwa kuwapa hawa Ahlul Bayt?

Kwanza kabisa aya hii inamtambulisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba ni Muumbaji mzuri sana. Kwa namna inavyotaf-siriwa kwa kawaida ni kwamba wapo waumbaji wengi na mionganini mwa waumbaji hao Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Muumbaji mzuri kuliko wengine. Ni kama vile wapo mafundi makanika wengi, wzungumzaji wengi, washairi wengi lakini mionganini mwao mmojawapo ni bora kuliko wengine. Hii ni tafsiri isiyo sahihi pale ambapo wapo waumbaji wengine wengi lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ni bora kuliko wengine. Aya hii inatoa maana ya kwamba muumbaji ni mmoja tu lakini viumbe vingi mbalimbali ni vya muumbaji huyu. Yeye ni muumbaji wa kila uumbaji na anao uumbaji tofauti kwa kila uumbaji, na kiumbe anao mwelekeo kwa hadhi ya uumbaji. Baada ya kuumba viumbe vyote alifika kwenye hatua ya kumuumba binadamu, halafu mtindo wake wa uumbaji ulibadilika kwa sababu Yule ambaye alikuwa anatakiwa kuumbwa wakati huo alikuwa ni kiumbe kilicho bora sana. Kwa hiyo Yeye Mwenyewe alisema:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَفْوِيهٍ

**“Hakika Tumemuumba mtu katika hali nzuri mno.”**  
**(Sura at-Tin 95:4)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu hakujipongeza alipoumba milima, malaika lakini baada ya kumuumba binadamu akasema “katika hali nzuri mno.” Hii ni kwa sababu ipo sifa maalumu ambayo imewekwa ndani ya binadamu.

Fitra ni mtindo wa uumbaji. *Fatr* maana yake ni kuumba, lakini neno hilihili linapotumika katika Fitra maana yake ni mtindo mahsus si na maalumu wa uumbaji ambao haupo katika uumbaji mwingine. Fitra ndio huu mtindo maalumu wa uumbaji na hapa ndipo binadamu anajitenga na viumbe vingine, na siri zote za uumbaji wa binadamu hufichuka. “Falsafa ya “katika hali nzuri mno” na “Mwenyezi Mungu Mtukufu kujipongeza Mwenyewe” inafunguka kutokana na hii aina maalumu ya uumbaji. Ni kutokea hapa ambapo tatizo la malaika kuchanganyikiwa linatatuliwa, na ni kutokea hapa penye pia ushetani wa njia ya Shetani unaanza. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba binadamu na akawapa taarifa malaika:

إِنَّمَا جَاءَكُم مِّنْ رَّبِّكُم مِّنْ كُلِّ أَرْضٍ فِي الْأَرْضِ

**Mimi nitaweka khalifa katika ardhi. (Sura al-Baqarah 2:30)**

Enyi Malaika, nataka kumuumba binadamu hapa Duniani ambaye atakuwa mwakilishi wangu; ninamuumba binadamu kutokana na asili ya udongo (teen). Malaika waliuliza swali wakasema kwani palikuwepo na haja gani ya kumuumba binadamu ambapo wao walikuwepo? Kama vile mionganoni mwetu pia wapo wanaosema kuna haja gani ya kuwepo fulani wakati yeye yupo. Kuna haja gani ya mwanazuoni ambapo yeye yupo. Kuna haja gani ya Imamu, Mujta-

hid, Marja ambapo sisi ni *Marja-e-Taqleed* kwa kuzaliwa tupo hapa, kuna haja gani ya Ijtihad.

Kuna haja gani ya kiumbe huyo ambaye atasababisha (*Fasad*) ujisadi na umwagaji damu hapa duniani, hata hivyo tunapokudhukuru kwa kutumia Tasbeeh? Mwalimu wetu mashuhuri Ustadhi Hassan Zaada Amouli anasema wakati Malaika waliposema kwamba:

وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ

**Sisi tunakutakasa kwa sifa zako. (Sura al-Baqarah 2:30)**

Sisi ni viumbe wazuri ambao tupo na tunakutukuza wewe. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema kwamba Yeye hakuwa anataka viumbe watakatifu Walio wazuri badala yake alikuwa anataka binadamu. Ninyi ni Malaika watakatifu lakini sio Watu. Ndiyo Iqbal anasema: “Ni vema kuwa binadamu badala ya malaika, lakini inatakiwa jitihada zaidi.”

Ni rahisi sana mtu kuwa malaika, nitakuonesha fomyula (utaratibu) yake ambayo unaweza kuitumia kwa usiku moja na asubuhi yake wewe utakuwa malaika.

Ili uwe Malaika chukua msala wa kuswalia, Tasbihi, maji ya kutawadha kwa ajili ya wudhu, kitabu cha *Mafatiihul Jinan* (Kitabu cha Dua) na uende nje ya jiji uwe sehemu ya kukupwekesha na uketi ndani ya pango; ambapo hakuna mtu atakayekujia na wewe hutakwenda kwa mtu yejote. Hakuna mwanamke ambaye ni (*Na-Mahram*) sio maharimu wako ambaye huna mazoea naye ambaye unaweza kumtazama; hakuna mtu ambaye utamteta, hakuna duka ambalo utakwenda na kudanganya, hakuna fedha ambayo unaweza kunyang`anya, hakuna mtu ambaye unaweza kudanganyana naye au kumuonea wivu. Hapo ni wewe tu ambaye unajihuisha na ibada tu.

Kwa kuwa utakuwa hujafanya dhambi yoyote na wewe upo katika ibada tu ya kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu tayari umek-wishageuka kuwa Malaika. Lakini kama ukitaka kuwa binadamu basi unachohitaji ni kurudi mjini uchanganyikane mionganoni mwa watu.

Ili kuwa binadamu mtu anahitaji kukaa ulimwengu wa binadamu; mtu anatakiwa kujizuia kumtazama mwanamke ambaye ni (*Na-Mahram*). Ukiweza kufutilia mbali uwepo wa mwanamke ambaye ni (*Na-Mahram*) kwako basi wewe umekuwa Malaika lakini kama utajizuia kumtazama mwanamke ambaye ni (*Na-Mahram*) kwako basi wewe ni binadamu. Kama hakuna rasilimali ya mtu mwingine iliyopo na hujanyang`anya rasilimali yoyote basi wewe ni Malaika; lakini kama rasilimali hiyo ipo na wala huigusi, basi wewe ni binadamu. Kama hakuna mtu aliyepo karibu na wewe ambaye amejaaliwa riziki kubwa kukuzidi wewe na bado hujamuonea wivu basi wewe ni Malaika; lakini kama yupo jirani ambaye anazo rasilimali nyingi na kama hujamuonea wivu basi wewe ni binadamu. “Ni bora zaidi kuwa binadamu badala ya kuwa Malaika, inahitajika jitihada zaidi.”

Malaika wameumbwa na kukamilishwa, lakini binadamu haku-umbwa na kukamilishwa, anapaswa kujikamilisha mwenyewe. Malaika waliumbwba (wakiwa wakamilifu kabisa) na kupelekwa lakini binadamu alipelekwa ili ajikamilishe mwenyewe. Lakini aliji-kamilisha awe nini?

### **Binadamu ameumbwa kwa kusudio gani?**

Binadamu hakuumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ili awe mwanazuoni wa Uislamu, daktari, injinia, Afghan, Mirza, Sayyed, badala yake Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba binadamu ili awe binadamu. Tulitoa amana yetu kwa kila kiumbe.

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبْيَنَ أَنْ يَحْمِلُنَّهَا  
وَأَشْفَقُنَّ مِنْهَا وَحَمَلَهَا إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا

**“Kwa hakika tulizitolea amana mbingu na ardhi na milima na vi-kakataa kuichukua na vikaiogopa, lakini mwanadamu akaichukua.  
Hakika ye ye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana.”**

**(Surah Ahzab, 33:72).**

Viumbe vingine vyote viliogopa baada ya kuiona amana. Baadhi ya vitu fulani ambavyo mtu akipewa huvifurahia lakini mtu akipewa vitu vingine huogopa kuvichukua. *Samawaat* (kila kilicho baina ya ardhi na mbingu) na kitu kigumu kweli hapa; milima pia iliogopa. Binadamu hutoa mfano wa milima kwa sababu ya nguvu lakini hata milima iliogopa; lakini binadamu alijitokeza mbele na akichukua amana hii. Amana hii ilikuwa nini?

Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa amana hiyo kwa mbingu, ardhi, milima. Ama unataka kuendelea kuwa mbingu hivyo ulivyo au nikufanye uwe bora zaidi? Unataka kuendelea kuwa ardhi hivyo ulivyo au nikufanye uwe bora zaidi ya hapo? Unataka kuendelea kuwa milima hivyo ulivyo au nikufanye uwe bora zaidi? Vyote hivyo vikasema Mwenyezi Mungu Mtukufu tuumbe hivyo hivyo. Mwenyezi Mungu Mtukufu akaumba mbingu, ardhi, milima na malaika kama viliyvo lakini ilikuwa ni tangazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba nani mionganoni mwa viumbe Vyangu ambaye hataumbwa abaki kama alivyo, ni kwamba ye ye atapewa tu uwezo wa kujikamilisha ndani mwake, na kumuonesha ye ye njia ya kujikamilisha na ye ye mwenyewe atajikamilisha kuwa binadamu kwa kutumia uwezo na njia ambayo ataoneshwa na muumbaji wake. Binadamu akasema; ni Mimi ambaye nitafanya hivi. Kamwe hatutakiwi kusahahu kitu cha muhimu ambacho ni Ajenda moja pekee, kusudio alilopewa binadamu; ambalo ni ye ye kujikamilisha kuwa binadamu, kuwa watu hai katika dunia hii.

### ***Khalq na Khulq:***

Katika maana ya ki-Qur`ani Tukufu na kifalsafa Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwambia binadamu kuwa mtu. Hii maana yake ni kwamba binadamu anapaswa kufanya kila kitu yeye mwenyewe. Tunachukua msaada kutoka kwa mwanafalsafa mashuhuri, ambaye ni wa pekee, mtu anayeheshimika na ambaye ni zawadi ya Shi'ah, lakini Shi'ah hawatambui thamani ya mtu kama huyu. Huko ulaya angalia jinsi watu wanavyo msifu mwanafalsafa wao ambaye wala sio msomi na Shi'ah wanaanza kudhani kwamba mtu huyo angekuwa mkubwa. Lakini tunazo rasilimali kubwa za aina hiyo lakini Shi'ah hawajui hata namna ya kuwatambulisha na kuwajulisha kwa dunia. Mtu huyu ni Mulla Sadr, na jina lake ni Sadruddin na wanafunzi wake humuita *Sadrul Mutaliim*. Mtu huyu alizaliwa miaka 400 ili-yopita nchini Shiraz. Baada ya Maasumu, tunapozungumza kuhusu watu wa kawaida tusiwajumuishe Maasumu kwa sababu chanzo cha elimu yao ni tofauti. Maasumu hawakusoma kwenye chuo kiku chochote au shule yoyote; hawakufika kwenye kiwango hiki kwa kufikiri. Hapa tunazungumza kuhusu watu baada ya Mtume na Maasumu amba walikuwa wanafunzi wao. Katika historia ya fikira ya binadamu, fikira sahihi na ya kina ambayo Mulla Sadri alikuwa nayo hakuna aliyefika kiwango hicho. Pamoja na kwamba wote wengine wanaaheshimiwa na tumeambiwa tunapaswa kuwaheshimu wanazuoni na walioelimika. Mtu yeyote ambaye amefanya huduma yoyote kwa jamii ya binadamu ni budi kuheshimiwa, si vema kutowaheshimu watu hawa. Lakini upeo na kina cha kufikiri alichofika mtu huyu hakuna ambaye amefika huko.

Jambo hili ndilo alilolitaja Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Qur`ani Tukufu kuhusu uumbaji wa binadamu. Mwanafalsafa huyu mashuhuri aliwasilisha jammbo hili katika mtindo wake mwenyewe. Yeye anasema, binadamu anavyo vitu viwili ndani mwake. Kimoja

ni Khalq na kingine ni khulq. Khalq ni ile sehemu ya uwepo wa binadamu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba na Khulq ni ile sehemu ambayo binadamu alikabidhiwa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ

**Hakika tumemuumba mtu katika hali nzuri mno. (Sura at-Tin 95:4)**

Ewe binadamu, Mimi nimetekeleza sehemu yangu katika umbo lililo zuri sana, na sasa wajibu wako unaanza. Kwa upande wako ni kwamba unapaswa kutengeneza *Ahsan Khulq* (undani wako mwenyewe ulio mzuri sana) ndani ya hii *Ahsan Khalq* (muonekano wako mwenyewe ulio mzuri sana). Wakati *Khalq* na *Khulq* vinakuwa ni kitu kimoja basi vinageuka kuwa binadamu. Lakini kama ukishindwa kuifanya *Khuliq* iwe kama *Khalq* basi ni huo muonekano wako ndio utakuwa *Ahsan* (mzuri) lakini *Khulq*; yaani undani wako mwenyewe hautakuwa *Ahsan* (mzuri). Sasa iulizwe Qur`ani Tukufu ni nani ambaye amefika kiwango hiki cha *Ahsan Khulq*. Qur`ani Tukufu inasema tumemuumba binadamu katika *Ahsanul Taqweem* (katika hali nzuri mno) na kwa upande mwininge pia inasema kwamba;

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ

**“Na hakika wewe una tabia tukufu.” (Sura al-Qalam 68:4)**

Katika muktadha wa mazungumzo yetu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Ewe Mtume! Wewe unaheshimika sana kuhusu *Khulq* yako. Undani wako mwenyewe ulio mzuri sana umetukuka.

Tunapaswa kujikamilisha sisi wenyewe, na chochote tunachofanya tupo katika kujikamilisha. Qur`ani Tukufu inasema Binadamu anajijenga mwenyewe uhalisi wake na si kwamba uhalisi wa binadamu unakamilishwa kwa nguvu, ni kwamba binadamu mwe-

nyewe anapaswa kuung`arisha uhalisi wake. Kazi yetu binadamu sio kuremba na kung`arisha uhalisi lakini badala yake kwanza tunapaswa kuukamilisha na kuufanya ufike katika kiwango cha utu.

Vitendo vyetu vyote na amali zetu zote huwa sehemu ya uwepo wetu. Chochote kile asemacho mtu hakitoki na kwenda hewani tu, mawimbi yake yanatoka nje lakini maana zake na athari zake hubaki ndani mwake. Kama vile unapompiga mtu kofi sauti hutoka nje lakini maumivu hubaki ndani. Sehemu kubwa ya tukio hilo ilibaki ndani na sehemu ndogo tu ndio iliyotoka nje. Kama mtu akichoma moto nyumba yake, moshi hutoka na kwenda kwa majirani pia, lakini moto hubaki ndani ya nyumba yake. Kama mtu akistawisha maua ndani ya nyumba yake upepo utapeleka harufu nzuri ya maua kwa jirani lakini maua yatakuwa ndani ya nyumba yake na bustani ya maua itakuwa ndani ya nyumba yake. Hivyo kumbuka ama mtu anafanya amali njema au amali ovu, athari za amali hiyo zinakawa sehemu ya uwepo wake. Kama mtu anafanya amali ovu maana yake ni kwamba anaunguza uwepo wake. Mtu anaposema uwongo, anaposhambulia, anaposengenya, anapokashifu wengine, basi yale maumivu yanayowapata wengine ni sawa na ule moshi wa nyumba inayoungua na kufika kwa majirani lakini moto unabaki ndani ya nyumba inayoungua. Moto unawaka mahali pengine lakini macho yanauma sehemu nyagine. Katika hali halisi ni kwamba mtu anapofanya vitendo vibaya ni sawa na kujiunguza mwenyewe, ni moshi tu unaotoka na kwenda kwa wengine. Kurahisisha, uovu ninaomfanyia mtu mwingine, sehemu kubwa ya athari ya uovu huo inakuja kwanza na tatizo dogo tu linampata yule ninayemfanyia uovu. Ni vivyo hivyo unapofanya amali njema; ni kwamba unapanda maua ndani mwako na kama mtu ananufaika na hiyo amali yako njema, basi huo ni upepo unaobeba harufu nzuri inayokwenda kwake, sehemu kubwa ya athari ya amali yako njema inabaki ndani mwako na inanufaisha

uwepo wako. Ni kama vile ukitoa sadaka na fedha hiyo inakwenda tumboni mwa mtu mwingine na unadhani kwamba fedha hiyo im-eondoka mfukoni mwako na ndiyo mwisho wake; lakini hali halisi sio hiyo, ni ule upopo wa harufu nzuri ambao umekwenda tumboni mwa mtu uliyempa sadaka, wema halisi wa kitendo chako unarudi kwako. Hapo ni kwamba unajijenga mwenyewe. Ni sawa na kama vile kujenga ukuta wa matofali ambapo unaweka safu ya matofali moja baada ya nyingine na ukuta unajengeka. Ujenzi wa binadamu pia unafanywa katika namna ileile, pale ambapo mtu anaweka safu za matendo, elimu na utambuzi (*Maarifat*).

Sehemu moja ya ujenzi huo inafanywa na Mwenyezi Mungu Mtukufu; na ile sehemu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametengeneza sio binadamu, hiyo ni fremu ambayo imetengenezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ambamo ndimo utu wa binadamu utain-gizwa, na utu unapaswa kuingizwa humo. Hii ndiyo tofauti ya binadamu na viumbe vingine.

Ilikuwa muhimu kuumbwa binadamu katika ulimwengu huu kwani bila ya kuwepo binadamu mfumo wa uwepo haungekuwa kamilii. Ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu alijibu kwa kusema, “yale ninayoyajua ninyi hamyajui.

إِنَّمَا لَا تَعْلَمُونَ

### Hakika mimi nayajua msiyoyajua (Sura al-Baqarah 2:30)

Hii ndio tabia ya Kimalaika kwamba kama mtu hajui kitu basi akubali kwamba hajui. Kama mtu aking`ang`ania kwamba anajua kitu asichokijua hiyo ni tabia ya Kishetani. Wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema “yale ninayoyajua ninyi hamyajui” Malaika walikiri kwamba wao walikuwa wanayajua yale tu ambayo wamefundishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na hawajui lolote zaidi

ya hayo. Lakini Ibilisi akasema kwamba yeche anajua; anajua nini? Akasema Ibilisi: "Mimi ni bora zaidi ya binadamu." Hapa ndipo Ibilisi alipokanushwa na kufukuzwa. Kwa hiyo chochote usichokijua sema hujui. Ipo katika simulizi kwamba: "Nusu ya ujuzi ipo katika kile usichokijua." Allamah Tabatabai; mwanazuoni mashuhuri sana hivyo kwamba baadhi ya wanafunzi wake ni Marajii leo hii wali-kuwa mara kadhaa kwamba hawajui kitu fulani. Lakini machinga ambaye ni mfanyabiashara mtaani, kamwe hasemi hajui.

### **Umbile la Binadamu-Kiwiliwili na Roho:**

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuumba binadamu katika sehemu mbili; sehemu moja ni ya kimaumbile au kimwili. Kama ambavyo imetatajwa kabla katika aya ya Surah al-Hashr, kwamba usije ukawa kama wale ambao wamemsahau Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa hiyo wamejisahau wenyewe pia.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ نَسُوا اللَّهَ فَأَنْسَاهُمْ أَنفُسُهُمْ إِنَّمَا هُمُ الْفَاسِقُونَ

**"Wala msiwe kama wale walomsahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio mafasiki."**  
**(Surah Al-Hashr; 59:19)**

Wakati mtu anapojisahau yeche mwenyewe huanza kumfikiria mtu mwengine kwamba ndiye yeche. Kama kwa ajali, pale inatokea kwa mtu ambaye anasahau nyumbani kwake na anabonyeza kengele ya mlangoni, nyumbani kwa mtu mwengine na akasema hapo ndio nyumbani kwake. Hivi watu wengine watafurahishwa au kusikitishwa na tabia hiyo? Watu wengine watapiga simu kwenye hospitali ya maradhi ya akili kwamba mtu huyu amepata wazimu. Au endapo mtu anaketi juu ya meza na kutengeneza slesi za mkate na kuweka slesi hizo mdomoni mwa mtu mwengine huku yeche akiamini kwamba

anaweka slesi hizo mdomoni mwake. Au kama mtu anahitaji fedha na ili achukue fedha hizo kutoka mfukoni mwake anaweka mkono wake mfukoni mwa mtu mwingine. Mwenye mfuko huo atamwambia kwamba huo sio mfuko wake lakini yeze atang`ang`ania kusema kwamba huo ni mfuko wake. Kwa hiyo mwenye mfuko huo atasema kwamba mtu huyo amekuwa kichaa kwa sababu anadhani mfuko wa mtu mwingine ndio mfuko wake. Wakati mtu anajisahau mwenyewe na anaanza kuwafikiria wengine kuwa ndiye yeze hii ni hali ya usumbufu.

Lakini wakati hali kama hiyo ikawa ipo kwa kila mtu katika jamii, ambapo kila mtu amejisahau yeze mwenyewe na anawafikiria wengine kuwa ndiye yeze, basi hapatakuwepo na hali ya kustaajabisha. Katika hali kama hiyo hakuna mtu anayestaajabu yanayotokea kwa wengine kwa sababu hapa kila mkono wa mtu upo ndani ya mfuko wa mtu mwingine. Hapa jambo la kustaajabisha litakuwa pale ambapo mtu ataweka mkono wake ndani ya mfuko wake mwenyewe. Pale ambapo kila mtu anakula haramu na mtu mmoja anatokea mionganini mwao anakula halali, huyu anayekula halali ataitwa mtu asiyefaa na mpumbavu. Mtu ambaye anapata kipato cha halali na anakula halali anaitwa mpumbavu. Katika *Khubatul Muttaqin* (hotuba kwa wacha-Mungu) Amiri wa Waumini Imam Ali ؓ anasema kwamba sifa moja ya mchaji Mungu ni kwamba watu husema kwamba mtu huyo amekuwa kichaa. Kama vile pale ambapo kupandishwa cheo kazini kwake iliwezekana kwa hongo ndogo tu lakini alikataa kutoa hongo. Watu watasema mtu huyo ni kichaa amaekataa kutoa hongo. Uwongo kidogo tu angefanikisha dili. Watu wanasesma kwamba mtu huyo si mtu wa dunia hii, hawezi kufika popote, hasemi uwongo, anakula halali, hawezi kufanikiwa na kwa hiyo mtu huyu ni kichaa.

Sehemu moja ya binadamu ni mwili, na upo uhalisia mwingine

ambao ni sehemu nyingine iliyosahauliwa. Msiba wa mtu kutojitambua mwenyewe ni kwamba sisi tumesahahu uhalisia wa uwepo wetu. Neno ambalo limezoleka sana katika ndimi zetu ni “Mimi.” Mimi mwenyewe, lakini hatuna ufahamu kuhusu uthibitisho na uhakikisho wa hii “Mimi.” Sisi hufikiria kitu kingine cha Mimi mwenyewe badala ya Mimi hasa. Nitajaribu kufafanua hili kwa kuuliza swali rahisi. Swali ni kiwango cha sisi kujua kama tunajitambua wenyewe au hapana.

Mtu anarudi nyumbani kwake na anatundika nguo yake kwenye kamba, na halafu mtu mwingine anafika hapo nyumbani kumuulizia mwenye nyumba. Anamuuliza mfanyakazi: “bwana mwenye nyumba yupo?” Mfanyakazi anajibu kwa kusema mwenye nyumba yupo ananing’inia kwenye kamba. Mwenye nyumba wala hayupo kwenye kamba ila nguo yake ndiyo ipo kwenye kamba; lakini kama mtu anaanza kutilia shaka kwamba mwenye nyumba yupo kwenye kamba basi mtu huyo atakuwa mgonjwa wa akili, na watu wengine watastaajabu kuhusu tabia ya mtu huyo. Binadamu sio vazi lakini mtu mgonjwa anadhani vazi lake ndilo yeye. Mtu huyu amepotea na amejitelekeza yeye mwenyewe.

Wakati watu wanapowaonesha watu wengine kwamba ni wao, wanasesma Mimi au Mimi mwenyewe, wakionesha kuelekea kwenye miili yao. Hivi Mimi ni mwili? Lakini siku zote watu huonesha na kuelekeza miili yao. Sisi huulisha mwili, huuogesha mwili, tunauhudumia na kuutunza mwili huu. Huwa tunatimiza mahitaji ya mwili na huwa tunauhudumia kwa kuulinda mwili huu usiku na mchana kwa sababu mwili huu ni Mimi mwenyewe, Mimi. Sasa tafakari juu ya jambo hili, huyu “Mimi” yupo wapi? Huwa tunatumia maneno mawili “Mimi” na “Yangu”. Neno yangu linatumiwa wakati viwo vitu viwili; kitu kimoja ni “Mimi mwenyewe” au “Mimi” na kitu cha pili ni kile kitu ambacho kipo chini ya umiliki wangu.

Kama pale ambapo unayo simu ya mkononi utasema nini kuhusu simu hiyo? Utasema Mimi au Yangu? Utasema yangu, kwa hiyo nipo “Mimi” na simu hii ipo chini ya umiliki wangu, kwa hiyo simu hii ni yangu. Wakati panakuwepo na uhusiano baina ya “Mimi” na kitu ambacho kipo chini ya umiliki wangu, kitu hicho ni cha kwangu. “Yangu” ni neno linaloonesha wingi, maana yake ni kitu ambacho kimetenganishwa nami. Sasa tuje kwetu sisi, ninaponyanyua mkono na kusema huyu ni “Mimi” utasemaje hapa? Kiungo hicho sio wewe, kiungo hicho ni mkono wako. Kwa hiyo wakati tunaposema mkono huu, mguu huu, kichwa hiki, bega hili, shingo hii, kifua hiki, macho haya vyote hivi ni vyangu. Yote hii maana yake ni kwamba viungo vyote hivi sio mimi, viungo hivi ni vyangu.

Kipo kitu kingine ambacho mkono, mguu, kifua, macho, pua, huwa vipo chini ya umiliki wake. Huyu “Mimi” anakuambia ufa-hamu kwamba viungo hivi ni vyangu lakini sio mimi. Kichwa ni changu lakini sio mimi. Sasa, wakati utakuwa umerejelea viungo vyako vyote vya mwili wako na kusema kwamba viungo hivi sio mimi ila ni vyangu, basi hata mwili wote huu ni wangu lakini sio mimi. Kwa hiyo vyote hivi ni vyangu, kwa hiyo sasa muulize, ni nani huyu mimi ambaye viungo vyote hivi vipo chini ya umiliki wake? Huyu Mimi au Mimi mwenyewe ni nani? Mmiliki yupo wapi? Ambaye anamiliki vyote hivi? Hatumjui mmiliki huyu ni nani? Tunaviju vitu vingine vyote, tunajua teknolojia, anga, jiografia, na pia tunadai kwamba najua hiki na ninakujua wewe na hata wahenga wako.

Mtu mmoja alikuwa anamtishia mwenzake kwamba baada ya kumkodolea macho mtu yejote anaweza kujua DNA yake pia. Kwa hiyo mtu huyu naajibu swalii hili rahisi: “wewe ni nani?” Kwanza jitafute na ujitambue wewe mwenyewe, vyote hivi ni vyako ambavyo unafikiria kwamba ni wewe. Utakapojitambua wewe mwenyewe basi utaweza pia kujua anuani ya wengine. Hii ndio sababu kwamba

Imamu Ali ﷺ, ambaye ni Imamu wa Fitra alisema; “Mtu anayeji-tambua mwenyewe anamtambua na Mola Wake.”

Utakapojitambua mwenyewe utamtambua Mola Wako pia. Unapokuwa hujitambui wewe mwenyewe utamtambuaje Mola Wako? Baadhii ya watu wamempoteza Mungu Wao. Watu wote hawa wanaokaa na kutoa uthibitisho kuhusu uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika hali halisi ni kwamba wamempoteza Mola Wao. Kama vile watoto wadogo wanapopotea gulioni wanasema mtoto amempoteza mama yake. Hivi ni nani aliyepotea? Mtoto au mama? Mtu aliyepotea ni Yule ambaye amepoteza anuani yake; hapa mama hajapotea isipokuwa mtoto ndiye aliyepotea kwa sababu mtoto hajui anuani yake.

Mtoto huyu pamoja na kwamba yeye ni mtoto lakini hataki kukubali ukweli kwamba yeye ndiye aliyepotea, yeye anasema mama amepotea. Hii ni kwa sababu anataka mtu amtafutie mama yake, lakini kama akisema kwamba yeye amepotea, maana yake ni kwamba anataka apelekwe kwa mama yake. Anaposema Mwenyezi Mungu Mtukufu amepotea, maana yake ni kwamba amtafute Mwenyezi Mungu. Hili ni kosa letu kubwa sana kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hajapotea, ni wewe ndiye uliyepotea; siku utakapojitambua ndipo utakapomtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu pia.

Dondoo za dini, vitabu vya mbinguni, Mitume na Maimamu ni kwamba wote wanapaswa kutuambia sisi kuhusu uhalisi wetu na kutuambia sisi ni nani na ni kitu gani. Ndio sababu Qur'ani Tukufu inasema “Msiwe kama wale waliomsahau Mola Wao, na Mwenyezi Mungu Mtukufu akawafanya wajisahau wao wenyewe.” Mtu aliyejisahau mwenyewe ni yule ambaye amempoteza Mola Wake. Upo uhusiano baina ya mtu kujitambua mwenyewe na Mungu. Ukijitambua mwenyewe basi utakuwa umemtambua Mola Wako ndani yako

mwenyewe. Unatakiwa kuelewa kujitambua mwenyewe ni nini. Tunatakiwa kuwa waangalifu kwamba pale ambapo mtu anajitambulisha kwa kutumia kile kitambulisho chake cha kazi anayofanya, ambacho kinasema mimi ni meneja, mkurugenzi basi huyo sio wewe.

Binadamu sio mwili badala yake yeye ni uhalisi uliovuka mpaka wa mwili. Uhalisi huu ni Roho Yenyewe na sio mwili. Mwili ni njia ya Roho kuja kwenye uwepo, kwa ajili ya kulea Roho na kuisaidia Roho kufikika kwenye ukamilifu wake. Wakati Roho inapofika kwenye ukamilifu wake, wakati wakutenganisha roho na mwili huwadia. Kila madhehebu imewasilisha uhusiano tofauti baina ya mwili na Roho, kama vile nguo tundu na kadhalika, hatutakiwi kupotea ndani ya kitu hiki.

Mwili upo katika udhibiti wa Roho, na Roho inaambiwa kuitumia hali hii, lakini ifahamu kwamba kipando hiki ni cha kuchanganyikiwa, na isije ikatokea kwamba kipando kikakupanda wewe. Baadhi ya watu wanaponunua motokaa kw ajili ya kutembelea basi motokaa huanza kuwapanda wao. Palikuwepo na mtu fulani aliywenda gulioni kumuaza punda. Mtu huyu alitaka kumuaza punda kwa bei ya juu sana hivyo kwamba hakuna mtu aliyeweza kumnunua punda huyo, na mtu huyo akachoka na akalala. Alipoamka mnunuzi alikuwa amesimama, kamba ilikuwa shingoni mwa mmiliki wa punda na punda huyo alikuwa anahesabu fedha. Ni kwamba punda alikuwa anamuaza mmiliki wake. Wakati mwingine hutokea kwamba ulikwenda kumuaza punda lakini punda akakuaza wewe kwa sababu ya uzembe. Motokaa ilinunuliwa kwa ajili ya kutembelea lakini sasa wao ndio wamekuwa kipando cha motokaa. Uhustiano baina ya Roho na mwili ulivyo ni kwamba kama Roho haiutumii mwili, mwili utaanza kuitumia Roho. Hii ndio maana inasemekana kwamba ujishughulishe wewe mwenyewe vinginevyo wewe utashughulishwa mwenyewe.

Roho inatumiwa kwa mambo mengi. Kila kiumbe hai kina Roho. Kama vile mnyama anapokufa, tunasema Roho imeondoka na kuuacha mwili. Roho nayo pia ni kitu cha kimwili ambayo ipo, katika baiolojia inajulikana kama Uhai. Mtu anapokufa, uhai huu huuacha mwili. Tunasema kwamba Roho imeuacha mwili, na aina hii ya Roho ipo ndani ya binadamu na wanyama. Msamiati huu wa Roho ni msamiati wa kibaiolojia. Kama vile moyo ni kiungo nyuma ya kifua ambao husukuma mwili; Kwa kuwa moyo huu hufanya kazi ya kati, kwa sababu ya uhusiano huo huitwa moyo. Moyo (*Qalb*) ambao Qur'ani Tukufu huitaja sio hii pampu iliyopo ndani ya mwili. Lakini moyo wa binadamu ambamo imo elimu, hisia, usunuo, upendo, chuki, mvuto na ambamo Qur'ani Tukufu huingia sio huu moyo ambaao una damu. Kwa uhusiano huo tu huu huitwa moyo. Vivyo hivyo roho inayioacha mwili wakati wa kifo ni uhai lakini sio roho ambayo Qur'ani Tukufu huitaja au uhalisi wa mtu. Roho hii sio ile ambayo ni uhalisi wa mtu, kwa sababu roho hii huuacha mwili mtu anapokufa. Roho ambayo ni uhalisi wa mtu wala haipo ndani ya mwili au nje ya mwili kwa sababu kuwa ndani ya mwili au nje ya mwili ni ishara ya kitu cha kimaumbile. Unaweza kuwa na dukuduku kuhusu suala hili kwa sababu siku zote tumekuwa tunasikia kwamba roho ipo ndani ya mwili. Aina hiyo ya wasiiasi na mshangao unafaa. Hii ni kwa sababu Mtukufu Mtume  anasema; “Ewe Mola wangu! Zidisha mshangao wangu kuhusu uwepo Wako.” Sisi pia tunatakiwa kumwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba azidishe mastaaajabu yetu kuhusu uwepo wetu.

Sisi binadamu tuna uhusiano na vitu vingi ambavyo sio vya kimaumbile. Nitakuuliza swali rahisi. Taarifa na elimu uliyonayo, ndogo au zaidi, yaani ya kisayansi, kidini, vyote hivi sasa hivi viro wapi? Vitu hivi vimehifadhiwa wapi? Vimehifadhiwa ndani ya ubongo? Sasa kama wewe unaamini kwamba vitu hivi vimehifadhiwa humo

basi fanyiwa upasuaji uone kama kweli vipo humo. Taarifa hii uliynayo haipo ndani ya mwili wako. Muulize mwanasayansi akwambie vitu hivi vimehifadhiwa wapi? Kwa hiyo labda vipo nje ya mwili? Hapana, kwa nini, kwa sababu taarifa hii ina uhusiano na ujuzi, na ujuzi sio maada na kwa hiyo haiwezekani kuwepo ndani ya kitu cha kimaumbile. Kitu chochote ambacho sio cha kimaada hakina mahali. Vitu hivi vipo ndani Mwako lakini Wewe pia sio mwili. Kama mtu akikuuliza taarifa hii ipo wapi, usimuoneshe mahali, mwambie swali lako si sahihi. Kama nikikuuliza Nelson Mandela aliumba lini Pakistan, basi swali lenyewe si sahihi.

Ndiyo sababu nilisema Madhehebu ya Imamia ni bora sana. Tazama *Usuul al-Kaafi*, sura ya kwanza ya Tauhiid. Mtu mmoja mkubwa mashuhuri na msomi aitwaye Jaasliq alimwendea Imamu Jafar Sadiq عليه السلام. Mtu huyu alikuwa na elimu ya sayansi, dini na falsafa na akamuuliza Imamu عليه السلام: Mwenyezi Mungu Mtukufu yupo wapi? Ipo tofauti baina ya lini na wapi, Lini maana yake ni wakati, na Wapi maana yake ni mahali. Kama angekuwepo Faqiih mwingine hapo angesema, Mwenyezi Mungu Mtukufu yupo juu mbinguni, ardhibni na kila mahali. Lakini mtu aliyeulizwa kuhusu utambuzi wa Mola alikuwa ni mtu aliyekuwa na utambuzi kamili wa yeye mwenyewe na wa Mola. Mtu huyu alikuwa na elimu kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye mwenyewe, na uwenyewe. Imamu عليه السلام akajibu: Swali lako sio sahihi. Wewe umeuliza kuhusu mahali alipo Mwenyezi Mungu Mtukufu. Yule anayeumba hana mahali. Yeye hana mahali.

Malaika hawana mahali, Roho haina mahali. Roho ina uhusiano na mwili. Roho ile ambayo ipo ndani ya mwili inajulikana kama roho katika baiolojia, ni uhai wa kibaiolojia. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ametengeneza uhalisia wa binadamu ambao sio wa kimaumbile ambapo wala haupo ndani au nje ya binadamu, lakini

badala yake mwili upo chini ya udhibiti wa roho. Mwili ni haja ya binadamu. Kutokea hapa uwanja wa kuelewa Fitra, na kuelewa to-fauti baina ya Fitra, Tabiyat na Ghariza unatayarishwa.

Dini sio kitu cha kukupatia wewe thawabu na pia ibada mbalimbali sio tu njia ya kufanya thawabu zimfikie mtu. Kusudio la mikusanyiko ya kidini, vitabu, majadiliano pia sio kusudio la kupata thawabu tu. Huwa tunajaribu kufanya vitu ambavyo huwa vinatuja sisi vyenyewe. Kama vile mtu anaketi kwenye mtandao usiku kucha na kusema anajaribu kulifanya jua lichomoze. Huko ni kupoteza muda bure. Jua litachomoza katika muda wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa wajibu huu wa Thawabu kukufikia wewe, na wewe hujaambiwa kuiendea Thawabu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema nitakuzawadia wewe na wewe usijishughulishe kuhusu Thawabu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ninyi hamkuumbwa kwa ajili ya Pepo, Pepo imeumbwa kwa ajili yenu. Msiwe na wasiwasi kuhusu vitu hivi. Ninyi mnajaribu kujishughulisha na vitu ambavyo vimeumbwa kwa ajili yenu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, Mimi nimetengeneza Riziki kwa ajili yenu, msiwe na wasiwasi kuhusu Riziki, riziki itawajieni. Kusudio lenu ni kwenda kuitafuta riziki. Dini haikuja kutengeneza Thawabu na Pepo kumfikia mtu. Vitu hivyo vimekuja kwa kusudio la kumfanya mtu afikie Kusudio la kuumbwa kwake. Mikusanyiko ya Kidini ina maana ya kumfanya binadamu afike kwenye hadhi ya utu.

Wakati ambapo wale wanaopoteza Fitra yao, hujishusha hadhi yao hadi kwenye kiwango cha hayawani. Wakati binadamu anapo-jishusha hadhi yake huwa hayawani, wakati hayawani akijishusha hadhi yake zaidi anakuwa Shimr na Khuli. Ipo hadithi isemayo kwamba hayawani wanapofika mbele ya binadamu wakamilifu, huinama na kutii; lakini wapo watu amba ni wabaya zaidi ya hayawani amba huonesha uhayawani wao mbele ya viumbe vi-

takatifu. Mabalaa waliyosababisha yalikuwa mabaya sana hivyo kwamba katika kambi ya maadui wa Uislamu wameandika kwamba ukatili ulikuwa mbaya kwa kiasi kwamba tulihisi kwamba mbingu zingeporoka.

### **Maana ya “Hanif”:**

Dondo ya sura yote hii ni kugeuza uelekeo wako kwa mintarafu ya dini ambalo ni somo la aya hii ya Surah Rum ambalo ndilo msingi wa kitabu hiki.

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّدِينِ حَنِيفًاٌ فَطَرَ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَاٌ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ  
ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

**“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini-ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini ya sawasawa, lakini watu wengi hawajui.” (Surah Rum; 30:30)**

*Hanif* maana yake ni kuelekeza. Katika fasihi ya Kiarabu *Hanif* ni hali. Unapokuwa umesimama na kugeuka kukielekea kitu, mgeuko huo unaweza kutofautiana katika namna. Namna moja ya kugeuka ni kwamba umesimama na miguu yako iko wima lakini nusu ya mwili unageuka kuelekea upande huo. Aina nyingine ya kugeuka ni pale ambapo mwili wako upo mahali pake na ni shingo tu ndiyo inayogeuka. Shingo pia ina kiunganishi ambacho ndicho hugeuka, pamoja na kwamba kina kitufe (*disc*) hivyo kwamba inatakiwa kuinama. Shingo imeumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika hali ya kunyambulika, hivyo kwamba - huenda siku moja mtu huyu atanikumbuka Mimi, atakumbuka ukuu Wangu na kwa hiyo kama akitamani kusujudu kwa paji lake la uso, shingo yake iwe inanyambulika ili kumwezesha ainame chini.

Wakati mwingine mtu anataka kugeuka na anageuka kwa ukamilifu kwa maana kwamba miguu yake pia inageukia upande wa kushoto au kulia. Kwa hiyo panaweza kuwa na aina tofauti za kugeuka:

1. Kugeuka huku Mwili umenyooka, shingo imenyooka lakini ni macho tu ndiyo yanayogeuka.
2. Mwili umenyooka lakini ni shingo tu ndiyo inayogeuka.
3. Mwili unageuka lakini miguu inabaki imenyooka.
4. Miguu pia inageuka kushoto kulia pamoja na mwili.

Wakati mwili au shingo inageuka, miguu bado ipo imenyooka. Lakini miguu inapogueka, mwili upo juu ya miguu, kwa hiyo mwili pia unapaswa kugeuka, maana yake ni kwamba shingo nayo inageuka.

Kila mtu amekabidhiwa ukweli; bila kujali njia yake anayofuata ataoneshwa mara moja ukweli. Wakati mwingine badala ya *Siraat* (njia iliyonyooka) huwa tunafuata *Subuul* (njia zenye michepuko mingi). *Siraat* ni njia iliyonyooka ambapo *Subool* ni njia nyingi za michepuko, upotovu, njia za Shetani. Wakati mwingine binadamu hufuata njia hizi za *Subool*; na ili kuweza kumrudisha ili afuate *Siraat* binadamu huoneshwa ukweli. Binadamu anapooneshwa ukweli anatakiwa kugeuka na kuelekea kwa mintarafu ya ukweli.

Linapotokea hili baadhi ya watu huwa hawataki kabisa kugeuka, hawataki hata kutazama ukweli. Wao hufuata tu ile njia ambayo wameamua kuifuata. Wao wanafikiri kwamba ile njia wanayofuata ndio njia ya mwisho na hawafikirii hata kugeuka na kutazama mahali pengine. Hawa ni wafuasi wa baadhi ya watu wanaojipatia utakatifu wa uwongo, na wao huwafuata watu hao bila kuhakiki. Huwafuata watu fulani kama vile mkia unavyofuata mwili wa mnyn-

ama. Baadhi ya watu hawako tayari hata kutazama ukweli, hawajali hata kugeuka. Mtukufu Mtume ﷺ huko Makkah aliwasilisha ukweli kwao lakini waliziba masikio yao kwa vidole vyao. Mkuu wa Mashahidi Imam Husein ؓ alitoa hotuba hapo Karbala na wao badala ya kusikiliza walipiga ngoma. Desturi hii ya kupiga ngoma ilikuja kutoka Karbala katika namna hii. Wakati Imam Husein ؓ anaanza kuhutubia wao walianza kupiga kelele kwa kupiga ngoma na kugonganisha ngao zao. Haya ndio yanayotokea. Wakati mtu anapooneshwa ukweli huwa hajali hata kuutazama.

Hata hivyo wapo baadhi ya watu ambao wakati mwingine hutazama ukweli kwa kugeuza macho; wakati mwingine mtu hgeuza shingo yake pia kutazama ukweli, na wakati mwingine hgeuza mwili wake pia kuuelekea ukweli. Katika hali zote hizi tatu mtu huyu huwa habadili mwelekeo wa mwendo na kutembea kwake. Anabakia hivyo hivyo pamoja na kwamba huutazama ukweli kwa wakati mwingine kwa macho yake, wakati mwingine kwa uso wake, na wakati mwingine mwili wake, lakini bado huendelea kutembea kuelekea upande huo ambako miguu inaelekea. Hii maana yake ni kwamba licha ya kutazama ukweli kwa kugeuza shingo yake lakini bado yeeye huendelea kufuata njia ya mkengeuko.

Wakati mwingine mtu anapoendesha motokaa huangalia mahali pengine nje kupidia dirisha la motokaa, lakini motokaa inakwenda kuelekea ambako magurudumu yanaelekea. Upande haubadiliki isipokuwa mpaka miguu nayo ibadili upande. Katika kubadilisha upande wa shingo au katika kugeuza macho kulia au kushoto, au katika kugeuza mwili, ukweli hauwezi kuonekana. Hadi hapo miguu itakapogeuuka binadamu hawezi kugeuka na kuuelekea ukweli. Lakini kama miguu ikigeuka na kubadili upande basi hata kama mwili hautaki kubadili upande bado utabadili upande kwa lazima. Katika lugha ya Kiarabu, Waarabu huita kitendo hiki cha kugeuza miguu *Hanif*.

Hapa ndipo unapohitaji kupata starehe kutoka kwenye aya. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّدِينِ حَنِيفًا

**Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini. (Sura ar-Room 30:30)**

Haikutamkwa kwamba ugeuze uso wako tu kuielekea dini.

Maana yake geuza uso wako; lakini kugeuza uso namna gani, geuza uso wako *Hanifan*.

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّدِينِ حَنِيفًا

**Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini. (Sura ar-Room 30:30)**

Hii maana yake ni kwamba isije ikatokea kwamba unaendelea kufuata njia ya ujahiliya na ugeuze uso wako tu kuuelekea ukweli. Qur`ani Tukufu inasema geuza uso wako lakini katika namna ya *Hanif*, ambayo maana yake ni kwamba unageuka pamoja na miguu. Hii maana yake ni kwamba unabadili mwelekeo wote kabisa na unaanza kutembea kwenye njia ya Ukweli. Elekeza uso wako kwa mintarafu ya Dini iliyo sawasawa lakini kama *Hanif*.

الدِّينُ الْفَيْمُ

**Hiyo ndiyo dini ya sawasawa, (Sura ar-Room 30:30)**

Geuka pamoja na uwepo wako wote; miguu yako inatakiwa igeuke kwa mintarafu ya *Siraat* kwa sababu unapaswa kuwa katika safari hii.

Neno *Hanif* lina hazina ya Utambuzi (Maarifat). Wafasiri wameandika mengi kuhusu neno hili *Hanif* lakini Qur`ani Tukufu ime-

lirejelea neno hili katika muktadha mahsus ambapo *Hanif* ana sifa maalumu. Hutokea mtu anaweza akageuka kabisa lakini akawa katika hali ya kuketi au kulala, ambapo mwili wake wote hugeuka lakini huko hakuwezi kuitwa *Hanif*. Kugeuka huku hakukufanywa katika hali ya *Hanifan*. Kama mtu akiwa katika hali ya kulala na akageuza mwili wake kuelekea ukweli hiyo haitakuwa *Hanifan*. Vivyo hivyo wakati mtu anasimama mahali, akiwa ametulia na akageuza mwili wake wote kuelekea ukweli hiyo haitakuwa *Hanifan*. *Hanifan* ni mtu aliyesimama na halafu anaugeuza mwili wake wote kuelekea upande mmoja pamoja na miguu yake na yupo tayari kuanza kutembea kuelekea upande huo. Pale ambapo mtu yupo tayari kutembea au akawa anatembea, mtu huyo haambiwi kugeuza kifua chake au uso wake kwa mintarafu ya dini, anaambiwa ageuze miguu yake kuuelekea ukweli.

### **Maana ya Shi'ah:**

Kwa mazungumzo haya ya mwanzo kuhusu *Hanifa* na katika muktadha wa aya ya Surah Rum ni dhahiri kwamba Qur'an Tukufu inamwalika kila mtu kugeuka na kuondoka kuelekea upande mmoja; njia moja. Ambapo tumekwisha tengeneza njia nyingi tofauti na kwa bahati mbaya tunafikiria dini pia kama kundi au madhehebu. Tumebadilisha Ushi'ah kuwa madhehebu. Ushi'ah sio madhehebu lakini umekwishabdalishwa na kuwa madhehebu kwa sababu ya uzembe na uvivu wetu. Ushi'ah sio madhehebu ila ni anwani ya Uislamu. Maana ya neno Shiite linatokana na familia ya pale ambapo neno *Tashi* (kusindikiza jeneza) pia lipo. Maana halisi ya neno Shi'ah ni kufuata bila kuacha upenyo. Shi'ah maana yake ni kufuata lakini bila kuacha upenyo, kama mtu anatembea huku akiacha upenyo basi neno ni tofauti. Kama hakuna upenyo, na unatembea ukiwa umeambatana kabisa basi hii ni kusindikiza. Tunapotakiwa kusindikiza jen-

eza, maana yake ni kutembea au kufuata jeneza. Baadhi ya watu hulitangulia jeneza lakini tunaamabiwa tulifuate na kutembea nyuma ya jeneza. Pia hii ina maana ya kwamba mtu hatakiwi kuwa umbali wa mita mia moja huku akiwa amebeba simu ya mkononi. Hii sio kusindikiza jeneza. Huwa tunahudhuria mazishi kwa sababu ya uhusiano. Kuhudhuria mazishi ni mionganoni mwa haki za marehemu kwamba walio hai wanatakiwa kumuaga. Hudhuria mazishi ya wengine ili na wengine waje kuhudhuria mazishi yako. Tashi maana yake ni kufuata Jeneza bila kuacha upenyo lakini hatutakiwi kuwa mbele ya jeneza na wala si nyuma ya jeneza pamoja na upenyo. Hutokea kwamba watu wengine hawawezi kuhudhuria mazishi kwa sababu ya ugonjwa. Kila mtu anapaswa kufariki dunia. Pamoja na kwamba tunatakiwa kuomba uhai lakini tujitayarische kufariki dunia. Lakini huwa tunafanya kinyume chake yaani sisi huwa tunajitayari-sha kuishi.

Rafiki mmoja alisema kwamba alipokwenda safari ya Ziara ali-kuwa amevaa viatu vya Peshawari ambavyo vina soli ya mpira wa tairi. Wakati alipokuwa anaswali, mtu huyo aliviweka viatu vyake mbele yake. Alikuwepo mtu kutoka Uajemi (Iran) ambaye alimuuliza mwenye viatu kama alikuwa Mwislamu. Mwenye viatu alikasirika na kusema yeye akiwa msikitini na anaswali halafu anatokeza mtu mwingine kumuuliza kama yeye ni Mwislamu? Mwirani huyo alimuuliza swalii hilo kwa mara ya pili. Mwenye viatu akajibu kuwa yeye ni Mwislamu.

Mwirani huyo alimuuliza mwenye viatu kama alikuwa anamua-mini Mwenyezi Mungu, akajibu kwamba hakika alikuwa anamua-mini Mwenyezi Mungu. Akamuuliza tena kama alikuwa anaamini Siku ya Hukumu. Mwenye viatu akasema kwa nini aulizwe swalii hilo? Mwirani akajibu kwa kusema kwamba alipoviangalia viatu al-ivyovitengeneza, ilikuwa inaonesha kama vile viatu vile haviwezi

kuchakaa hata baada ya Kiyama. Kwamba matayarisho aliyokuwa ameyafanya mwenye viatu yalikuwa yanaonesha kama vile watu havatakiwi kufariki dunia.

Tazama matayarisho ya maisha yetu, makazi yetu. Ukivangalia vitu hivi, hivi ni kweli vinaonesha kama vile tunatakiwa kufa? Tunatakiwa kujitayarisha kwa kifo kwa namna ambayo wakati wowote kifo kikifika tuwe tumejitayarisha. Kwa hiyo tunatakiwa kusindikiza jeneza. Lakini baadhi ya watu wazee hawawezi kuhudhuria mazishi kwa sababu wao ni dhaifu, lakini hukaa kwenye makazi yao na kumlilia mjukuu wao. Watu hawa wanayo huzuni kubwa sana kwa kiasi kwamba hulia hadi kuzimia. Huzimia kwa sababu ya huzuni lakini kwa sababu ya umri hawawezi kuhudhuria mazishi. Hata wale ambao wapo nchi za ng'ambo na hawawezi kuhudhuria mazishi huomboleza kwa kutumia simu. Watu kama hao wamo katika hali ya huzuni lakini huwezi kusema kwamba wao pia wanasindikiza jeneza au ni sehemu ya kusindikiza jeneza. Wapo watu ambao huwapenda marehemu lakini hawawezi kusindikiza jeneza.

Mtu mmoja alimwenda Imamu Husein ﷺ na kumwambia "Ewe Mkuu wangu! Mimi ni Shi'ah wako (*Ana min Shi'atequm*). Mkuu wa Mashshidi Imamu Husein ﷺ alikasirika na akasema *Ittaqillah*, Muogope Mwenyezi Mungu. Umeleta dai kubwa sana. Wewe unamjua Shi'ah wetu ni yupi? Halafu Imamu Husein ﷺ aliorodhesha tabia za Shi'ah na akasema hakuona tabia hizo kwa muulizaji. Lakini ninaweza kushahidilia kwamba wewe ni mtu unayependezwa na kutupenda sisi. Hii ni kwa sababu wewe ni mwenye furaha katika furaha yetu na unahuzunika katika mabalaa yetu, lakini Shi'ah ni mtu ambaye upendo wetu humvuta kutoka kwenye makazi yake na kumleta kwenye uwanja wa mapambano.

Tashaiyya ni anwani ya Uislamu. Hii ni anwani ambayo Mtukufu Mtume ﷺ aliupatia Uislamu. Ilikuwa na maana ya kututaarifu sisi

kwamba Uislamu sio jina la kufikirika tu kiakili kama falsafa, Uislamu sio jina la historia. Uislamu sio jina la imani (*Aqeeda*) na dhana. Uislamu ni jina la kutenda. Ili kuweza kuonesha kwamba Uislamu sio nadharia tu lakini ni dini ya kivitendo anwani yake imewekwa kama Shi'ah maana yake ni kufuata.

Madhehebu ni kugeuka kuelekea kwa mintarafu ya *Diini Hanifa* (dini ya sawasawa). Dini sio madhehebu na kwa sababu tu wen-gine walianzisha madhehebu pia na sisi tulianzisha madhehebu na kubadilisha Shi'ah na kuwa madhehebu. Qur'ani Tukufu inasema:

### ﴿قُرْفُوا﴾

#### **Msitawanyike (Sura aal-'Imraan 3:103)**

Kama wengine wamegeuka na kuwa katika madhehebu basi waachwe wawe hivyo, kwa nini ninyi pia mjifikirie kama madhehebu? Katika lugha ya Kiarabu neno *Madh'hab* linatoka kwenye neno *Dhahaba* ambalo maana yake ni kutembea. Neno *madh'hab* linarejelea mahali pa kutembea. Ni sawa na neno *Suluuk* ambalo maana yake ni kutembea, ambapo neno *Maslaq* maana yake ni mahali pa kutembea. Neno *Sair* maana yake ni kutembea ambapo neno *Masiir* maana yake ni njia ya kupita wakati wa kutembea. *Dhahaba* maana yake ni kutembea na *dhahab* maana yake ni mahali pa kutembea. Maana yake ni sehemu ya Tapo, katiba na manifesto ya Tapo. Na *Ahli Madh'hab* ni ule ummah ambao upo kwenye Tapo. Shi'ah na Dini ni jina la Tapo, sio jina la utulivu na kutuama. Kama mtu anakaa mahali pa takatifu kwa muda wa miaka mia moja, bado mtu huyo hatafikiriwa kuwa yupo katika *Diini Hanifa* (dini ya swasawa) kwa sababu mtu huyo hayupo kwenye Tapo. Tumeambiwa kwamba kabla ya Uislamu Bani Hashim walikuwa katika *Diini Hanifa* (dini ya sawasawa). Wakati huo Qur'ani Tukufu ilikuwa bado hajateremshwa; Mtume alikuwa

hajazaliwa lakini wahenga wake walikuwa katika *Dini Hanifa*. Wakati watu wengine walikuwa wanasujidia masanamu hawa (Bani Hashim) walikuwa wanamsujidia Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Nini maana ya *Dini Hanifa*? Maana yake ni kwamba pale ambapo watu wengine walikuwa wametuama hawa (Bani Hashim) walikuwa katika mwendo (Tapo). Sanamu ni kitu gani? Sanamu ni kitu kilichochongwa kutokana na jiwe na jiwe lipo katika hali ya kutulia. Wakati wowote sanamu la jiwe likifika mbele ya binadamu, akili ya binadamu huyo pia hutulia na kutuama yaani hafikiri. Pale ambapo sanamu la jiwe linakuja mbele ya ibada ya binadamu basi ibada nayo husita. Wakati sanamu linakuja mbele ya *Aqiida* (imani); imani husita. Wakati sanamu linakuja mbele ya binadamu, binadamu husita. Diini *Hanifa* maana yake ni kwamba ile dini ambayo uelekeo wake umengeuka kwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wakati binadamu alikuwa amesimama; kwake yeye kuwa katika mwendo alipaswa kupiga hatua na kugeuza miguu yake, na hii ndio *Hanif*. Mtukufu Mtume ﷺ aliagizwa:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلَّدِينِ حَنِيفًا

**Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini. (Sura 30:30)**

“Ewe Mtume! Wewe na Ummah huu mnatakiwa kugeuka kwa mintarafu ya dini katika hali ya *Hanif*.” Na dini ni nini?

فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا

**Umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu.  
(Sura ar-Room 30:30)**

Dini ni Fitra (Hali ya kimaumbile) ambayo kutokana na hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaumbeni. Hii ni dini iliyo sawa-

sawa lakini watu wengi hawajui. Wakati Qur'ani Tukufu inasema katika aya hii kuelekeza uso wako:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلّدِينِ حَنِيفًا

### Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye dini. (Sura 30:30)

Kumbe uso huu sio huu uso wetu wa kimaumbile wenye macho na pua. Kama ilivyo kwa kifungo, tunasema kifungo changu kimefunguka, sio sahihi kusema kifungo changu, sahihi ni kusema kifungo cha shati langu. Betri yako imekosa nishati maana yake ni betri ya simu yako imekosa nishati. Uso huu sio uso Wangu au Mimi. Huu ni uso wa mwili. Kama nikigeuza shati langu kuelekea Qibla na kiwiliwili changu kipo sehemu nydingine na kuanza kuswali; je hii itakuwa sahihi?

Ni kama vile una shati lako ambapo vifungo vyake vipo nyuma na sehemu ya nyuma ya shati ipo mbele, na halafu unaanza kusimamisha Swala ambapo mgongo unaelekea Qibla. Mtu akikuuliza na wewe unajibu kwamba vifungo vya shati lako vinaelekea Qibla. Aliyekuuliza atakwambia Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka wewe uelekee kwa mintarafu ya Qibla, sio shati lako.

Kwa hiyo sasa kama tukigeuza uso huu, ambao una masharubu, ndevu, pua, macho na kama kifua hiki tunageuka kwa mintarafu ya Qibla na Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi ni sawa na kugeuza nguo yako kuelekea Qibla. Mwenyezi Mungu Mtukufu atakwambia sikukwambia ufanye hivi, Mimi nataka WEWE ugeuke unielekee Mimi. Kwa hiyo kwanza tunatakiwa kujua: Hivi Mimi ni nani, hiki kitu Mimi na mwenyewe. Huyu Mimi au mwenyewe ni Fitra (Hali ya kimaumbile). Uso wa Fitra ndiyo unaohitaji kugeuzwa kwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

### **Fitra (Hali ya kimaumbile) na Sunnah:**

Fitra (Hali ya kimaumbile) Ni mtindo wa Uumbaji ambao ulifanywa kwa kiumbe mahsusini ambao haukufanywa kwa viumbe vingine vyovvyote isipokuwa kwa binadamu. Lipo neno jingine, Sunnah ambalo lipo katika hadithi na Qur`ani Tukufu. Sunnah mwelekeo na mbinu. Sunnah ya Mwenyezi Mungu Mtukufu maana yake ni mbinu na sheria ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sheria na mbinu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu haibadiliki. Sheria kwa ajili ya uumbaji, sheria kwa ajili ya dini haibadiliki. Sunnah na Siira ni maneno yanayotofautiana. Sunnah ni mbinu, mwelekeo na Siira ni mtindo. Sheria ya uumbaji haikubadilika alipokuwa anaumbwa binadamu, maana yake ni kwamba Sunnah haikubadilika lakini mtindo wa uumbaji ulibadilika. Nitaeleza jambo hili kwa mfano. Unahitaji kukumbuka kwamba mifano ni njia ya kutayarisha akili; akili inapokuwa imetayarishwa, mfano unatakiwa kuondolewa ili maana halisi iweze kuingia ndani. Kama vile mtu anapotoboaa tundu; kwanza keekee inaingia ndani sasa inapokuwa tayari tundu limekwisha tobolewa, keekee inatolewa nje.

Fitra ni mtindo wa uumbaji ambapo Sunnah ni sheria ya uumbaji. Mfinyanzi hufanya kazi ya kisanii. Ni kazi ya kisanii ya hali ya juu sana duniani kote lakini huko bara la India ufinyanzi ni kazi ambayo imeshushiwa hadhi. Kila mahali mwanachuoni anaheshimiwa lakini katika utamaduni wa bara Hindi huwa mwajiriwa. Hii ni zawadi kwa wafalme na wafalme wakuu. Tumechukua dini kutoka kwa Raja na Maharaja. Katika vitala vya wafalme ilikuwa ni mazoea kuwepo aina 13 za wahudumu na wafanyakazi na mmojawao alikuwa Maulana. Hawa Maulana ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapa Uimamu (uongozi) wakawa waajiriwa. Walikuwa wanachukua malipo kwa ajili ya kuongoza Swala na kufanya mambo mengine. Walipo-geuka kuwa Maimamu basi shughuli zao zote zilibadilika na kuwa wajibu na sio kuajiriwa. Mapinduzi ya Kiislamu yalipofanyika hali

ilbadilika. Wale ambao waliofanywa kuwa waajiriwa na binadamu kwa mara nyingine walikuwa wanachuoni na ma-Agha. Kama mapinduzi yaliwabdalisha waajiriwa kuwa wakuu na kuwafanya waheshimiwe, basi hiyo ni dhamira ambayo inasema hivi; dini inasema kwamba yule aliyekufanya upendeleo huu wewe unatakiwa kurudisha upendeleo huu kwake.

Mfinyanzi anapofinyanaga vyungu, kuna kanuni. Kwanza anahitaji udongo na udongo huo uwe udongo wa aina maalumu unaofaa kwa kazi ya ufinyanzi. Kwanza anahitaji kutengeneza kinyunya halafu anakiacha kwa siku chache. Kwa nini? Ili kinyunya hicho kikuze hali ya kuwa chombo. Upo mlolongo kwa ajili ya kugeuza udongo kuwa vyombo. Sasa anachukua mabonge ya udongo na kutengeneza mtindo. Baada ya kuweka mtindo anachukua gurudumu na kuweka udongo ndani yake. Sasa huanza kuzungusha gurudumu na wakati anazungusha gurudumu hutumia vidole vyake vya kisanii na kuupatia mtindo huo umbile. Mfinyanzi anatakiwa kuwa na vidole vyenye kipaji sio vidole vya kawaida, hivyo ndivyo ambavyo huvitumia kuupatia udongo umbo. Hii ndiyo kanuni ya kutengeneza vyombo. Mfinyanzi anatengeneza nyungu kubwa, chombo, bakuli ambalo mteja ameagiza kutengenezewa. Sasa mtu anamwenedea mfinyanzi na kumuagiza amtengenezee aina maalumu ya vyombo. Mteja huyo anamwambia mfinyanzi amtengenezee kitu chenyе urembo amba-cho atakiweka kwenye chumba chake cha uchoraji kwa lengo la kufurahisha macho ya wageni wake. Mteja anasema sasa kwa ajili ya kitu hiki nimepaswa kuja kwako kwa sababu ninazo fedha lakini wewe unacho kipaji. Mtu mwenye kipaji sio yule mwenye fedha bali ni yule mwenye ujuzi wa kugeuza udongo kuwa kitu cha kisanii. Kanuni ya utengenezaji ni ileile kwamba anahitaji udongo huohuo, anatengeneza kinyunya, anakiweka kwenye gurudumu, na kutumia vidole vyake. Kila kitu anachokifanya katika kutengeneza kitu cha

urembo ni mfano uleule kama anavyotengeneza nyungu isipokuwa tofauti ni moja tu kwamba mtindo ambao atatumia katika kuten-geneza kitu hiki cha urembo utakuwa tofauti. Kama hatabadilisha mtindo basi kitu hicho pia kitakuwa nyungu, bakuli au kitu kingine ambacho hakitafaa kuweka kwenye chumba cha uchoraji.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba ulimwengu huu, na chini ya kanuni fulani aliendelea kuumba kila kitu kilichopo katika ulim-wengu huu na baadaye ndipo ilipofika zamu ya kuremba ulimwengu huu, wakati wa kazi bora kwa ajili ya kiumbe huyu. Sasa Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka kuumba kitu ambacho kingeng'arisha ulimwengu, kitu ambacho kingekuwa cha fahari ya ulimwengu huu. Ili aweze kufanyakazi hii bora kanuni ya uumbaji haikubadilika, lakini alitofautisha mtindo. Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa mtindo mpya wa uumbaji. Alikipatia kitu hiki uumbaji mahsus. Lakini aina gani ya uumbaji? Na tuelewe sifa hii maalumu ya binadamu katika maelezo ya kina zaidi ili tuweze kukielewa kitu hiki cha thamani cha Fitra.

### **Maana ya Maada katika Falsafa:**

Kama ambavyo nimekwishasema kabla kwamba sehemu moja ya ulimwengu ni wa kimaumbile. Zipo aina mbili za umaumbile. Aina moja ni ile ya vitu vinavyoonekana ambapo vitu vyenye maumbo vinajulikana kama vitu vya kimaumbile, ambapo ipo aina nyingine ya umaumbile katika falsafa. Katika falsafa maada maana yake ni kwamba ukamilifu wote unaohitajika kwenye kitu kile inawezekana usiwepo lakini uwezo wote wa kujikamilisha upo ndani ya kitu hicho. Mathalani: Mbegu ya ngano inaotesha mmea wa ngano. Hii ni kinanuni ya ulimwengu wote kwamba mmea hutokana na mbegu. Mbegu ina uwezo wa kuotesha mmea mahsus. Kama ikipandwa mbegu ya ngano haiwezi kuotesha mmea wa shayiri; mtoto wa farasi

hawezi kuwa punda. Hii ni kanuni kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu aliviumba vittu vyote hivi kwa sababu vilikuwa vinaweza kujikamilisha vyenyewe. Malaika ameumbwa. Malaika hata baada ya miaka 100, 1000 au mamilioni ya miaka yeze atabaki kuwa Malaika tu. Malaika Izraeli hawezi kubadilika na kuwa Jibrili, na Malaika Jibrili hawezi kubadilika kuwa Mikaili. Viumbe kadhaa havikuumbwa ili vijikamilishe vyenyewe lakini badala yake vilipewa uwezo na uwanja wa kujikamilisha vyenyewe. Viumbe ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliviumba na kuvipatia uwezo wa safari yao kuelekea kwa mintarafu ya ukamilifu wao unaanzia na uwezo huu wa kujikamilisha. Hakuna ukamilifu ndani mwao lakini ukamilifu utakuja ndani mwao. Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuweka mmea wa ngano ndani ya mbegu lakini aliweka uwezo wa mmea wa ngano ndani ya mbegu na binadamu aliambiwa apande mbegu hii ndani ya ardhi ili mmea uweze kuota. Ninyi fanyeni kiasi fulani na sisi tutafanya kiasi fulani, lakini hata vile tutakavyofanya sisi thawabu zitawajieni ninyi tu.

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ

**“Je, Mnaona mnayolima?” (56:63)**

أَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الْزَارِعُونَ

**“Je, Ni ninyi mnayoyaotesha au ni Sisi ndiyo wenyewe kuotesha?”  
(56:64)**

لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ حُطَامًا فَظَلَّمْنَا تَنَكَّهُونَ

**“Tungelitaka tungeliyafanya mapepe, mkabaki mnastaajabu.”  
(Surah Waqia, 56:65).**

Qur`ani Tukufu inamtaka binadamu kuyaangali yale aliyolima.

*Harthu* maana yake ni kulima ardhi, kuilainisha, kupanda mbegu na kuifukia kwenye ardhi. Baada ya kufanya hivyo kazi yako imek-wisha, nenda ukalale. Sasa kuanzia hapa kazi ya mtendaji mwingine inaanza. Ukuaji unaanza; mbegu inahitaji kumamamnuliwa, na sasa mizizi inatakiwa kwenda chini na matawi yanatakiwa yatokeze nje. Na sasa tunatakiwa kutoa chakula kwa ajili ya makuzi. Sasa mmea unapokua na kufika kiwango fulani huzalisha mbegu na mbegu hizo huhitaji kufunikwa. Sasa tazama kile ulichokifanya na kile ambacho Sisi tumefanya. Wewe ulichofanya ni kupanda ile mbegu ardhini. Ni nani aliyeiwezesha mbegu hiyo kuota. Wewe ulipanda mbegu moja lakini Sisi tumeiongeza mbegu hiyo na kuwa mia moja.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa mfano huu kwa ajili ya *Infaq*, kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Zipo aina mbili za mbegu; aina moja ni ile ambayo mkulima huhifadhi kwa ajili ya kupanda msimu wa kupanda ukifika; ambapo aina nydingine ya punje husagwa na kuwa unga. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema; sasa tazama katika mkokotoo wa mahesabu yako na mkokotoo wa mahesabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wewe unadhani kwamba zile nafaka ulizozipeleka kwenye mashine ya kusaga unga na uka-oka mkate na kupika vyakula vingine kutokana na unga huo ndio zimekuwa na manufaa. Na zile nafaka ulizozihifadhi kwa ajili ya kupanda ulidhani kwamba hizo zilikuwa kwa ajili ya ardhi.

Wewe unadhani kwamba zile nafaka zilizosagwa na kuwa unga na ukapika chakula chako ndizo zenye manufaa ambapo zile ulizopanda ardhini zimepotea bure ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema hicho ni kinyume. Kwa nini? Ile mbegu moja uliyopanda ardhini Mwenyezi Mungu Mtukufu ataifanya kuwa nafaka mia moja. Mwenyezi Mungu Mtukufu atazalisha punje kutokana na kila punje moja na kutokana na kila punje tena atazalisha punje saba. Na kama

Yeye akitaka atafanya idadi hiyo kuwa mara mbili. Namna gani? Mbegu moja ambayo wewe umepanda Mwenyezi Mungu Mtukufu ataotesha mashina saba, na kutokana na kila shina atazalisha punje mia moja, kwa hiyo kutokana na punje moja uliyopanda ardhini Mwenyezi Mungu Mtukufu atazalisha punje 700, na kama akitaka atazidisha na kuwa 1400.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ataangalia uaminifu wa mja Wake, na kama mhusika ni mtu safi na mwaminifu basi Mwenyezi Mungu Mtukufu ataongeza hata zaidi ya punje 1400; Yeye ataongeza na kuwa tele, amali zako njema ambazo hata hutaweza kuhesabu.

مَئُونَ الَّذِينَ يُنْفَقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَّلَ حَبَّةً أَنْبَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ  
سَبْعَ لَيْلَةٍ مِائَةُ حَبَّةٍ وَاللَّهُ يُضَاعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلَيْهِ

**“Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuza mashuke saba; katika kila shuke pana punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa. Mjuzi.”**  
**(Surah Baqarah, 2:261).**

Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa mfano huu kwa nani; alitoa mfano huu kwa wale wanaofanya *Infaq*. Kwa hiyo tazama katika mkokotoo wa mahesabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; mahesabu yake hayahesabiki. Wale wanaohesabu na kumpa Mwenyezi Mungu Mtukufu naye pia hunesabu na kurudisha ambapo wale wanaotoa bila kuhesabu naye Mwenyezi Mungu Mtukufu huwapa bila hesabu.

Infaq ni kama maji. Ipo mifano miwili ya maji. Kama ilivyo kwenye bwawa, maji yanapomwagika kwenye bwawa, ipo mashine ya maji, maji yanapopita kwenye mfereji wa kupunguza maji ya bwawa, humwagika kuingia kwenye mashine ya maji na kuzalisha nishati ambayo hutumika kutoa mwanga kwa watu wengi. Ni maji

yale tu yanayopita kwenye mfereji wa kupunguza maji ya bwawa ndiyo yanayozalisha nishati. Yale maji yanayobaki huwa yametuama. Kama vile ilivyo katika dimbwi la maji, maji hubaki pale yakiwa yametulia na hutuama na hukuza vijidudu, vyura, ruba na wadudu ndani yake ambao husababisha maradhi. Tazama maji yaliyopo katika kijito, huwa hayajai na kwa sababu yanatiririka, yana samaki ambao hukupatia wewe nyama tamu na nzuri kiafya. Leo hii daktari anasema kwamba unapougu kwa sababu ya kula chakula ambacho ni kiporo unatakiwa ule nyama ya samaki, kwa sababu samaki ni viumbe wenyе afya, kwa nini? Kwa sababu wao wanaishi katika maji safi yanayotirirka. Samaki hawazaliani katika mifereji. Fedha ipo kama maji, kama fedha inaingia kutoka upande mmoja na inaotoka upande mwingine, basi ni sawa na mfereji wa kupunguza maji ya bwawa ambamo maji hupita na kumwagika kwenye mashine ya maji na kuzalisha nishati. Nishati hii itaangaza duniani kote, wala usidhani kwamba nishati hii imepotea bure. Fedha inayopatikana kutokana na nishati hii huhifadhiwa kwenye akaunti za mabenki na hugeuka kuwa kama maji yaliyotuama, na ni kitu gani kitakachozalishwa humo? Tunasema kwamba utajiri huu uliolimbikizwa ni kwa ajili ya watoto wetu lakini watoto wanaoishi kwa kutumia utajiri huu hugeuka na kuwa watenda dhambi, vijidudu, vyura, wadudu. Na kuititia utajiri huu huanza kuangamiza jamii. Mwenyezi Mungu Mtukufu hutoa baraka katika Infaq. Mfano wa Infaq ni kama vile ile mbegu yenye uwezo wa kugeuka na kuwa mmea. Katika falsafa uwezo huu unajulikana kama maada.

### **Dunia Inayoonekana na Dunia Isiyoonekana Iliyopo Ndani ya Binadamu:**

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba vitu fulani katika hali ya ukamilifu na vitu vingine vimeumbwa viweze kujikamilisha vyenyewe. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba ulimwengu huu ambao una

pande mbili. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba upande mmoja wa ulimwengu kama maada na upande mwagine aliumba ulimwengu ambao si wa kimaada. Ulimwengu wote wa kimaada unajulikana kama “*Alam-al-Mulq*”; ambapo upande ule ambao si wa kimaada unajulikana kama “*Alam-al-Malqoot*” ambao pia unajulikana kama ulimwengu usioonekana. Kama ambavyo imetajwa katika Surah ya al-Baqarah kwamba watu ambao ni wacha-Mungu (*Muttaqqiin*) ni wale ambao huamini katika *Ghaib* (yasiyoonekana)

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ

### **Hao wanaoamini katika yale yasiyoonekana. (Sura al-Baqarah 2:3)**

Maana ya Ghaib (yasiyoonekana) ni dunia ambayo sio ya kimaada au dunia ya kimetafizikia. Dunia ya yale yaonekanayo ni *Alam-e-Shahadat*; hii ni dunia ambayo unaweza kuhisi kwa kutumia milango ya hisia. Dunia ya yaonekayo ni ile iliyopo kabla ya ukuta na ng’ambo ya ukuta pia; nje ya kiwiliwili na ndani ya tumbo pia ni dunia ya yasiyoonekana. Kitu chochote ambacho unaweza kukiona, kukisikiliza, kukinusa kukionja na kukigusa vyote hivyo ni vya dunia ya yanayoonekana. Dunia ya yale yasiyooneka ni ile ambayo binadamu huithibitisha kwa akili (*Aql*) na kwa kupitia *Qalb* (moyo) binadamu huishuhudia dunia hii ya yale yasiyoonekana (*Malquit*).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuamini katika yale yasiyoonekana na kuamini katika dunia isiyoonekana mtu anatakiwa kushuhudilia dunia hiyo. Mtu fulani alimuuliza Amiri wa Waimini Imam Ali عليه السلام kama alikwisha wahi kumuona Mwenyezi Mungu Mtukufu. Imam Ali عليه السلام alijibu: Mwenyezi Mungu Mtukufu na aku-laani wewe. Wewe unanifikiria mimi kama unavyojifikiria wewe. Wewe unadhani kwamba Ali anamwamini na kumwabudu Mwe-

nyezi Mungu Mtukufu yule ambaye amesikia habari zake? Hapana! Nimemuona Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini amini kwamba si-jamuona Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa macho haya bali nime-muona kwa macho ya utambuzi. Aba Abdillah ﷺ anasema kwam-ba; “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni lini ulipotea, lini ulijificha hivyo kwamba mimi nilihitaji kukutafuta. Wewe unaonekana, lakini mimi ndiye niliyepotea.” Kwa hiyo unahitajika kuingia katika ile du-nia ya yale yasiyoonekana na kushuhudia dunia hiyo hivyo kwamba unaweza kuamini.

Dunia ya yale yaonekanayo ni dunia ya maada. Mwenyezi Mun-gu Mtukufu aliumba dunia yote hii (yenye yale yaonekanayo na yale yasiyoonekana) kwa chanzo cha uwepo Wake na alituonesha sisi se-hemu ndogo tu ya dunia ya maada. Lakini bado dunia zote hizi mbili inayoonekana na isiyoonekana hazikutangazwa na Mwenyezi Mun-gu Mtukufu kama kazi bora ya uumbaji. Halafu Mwenyezi Mungu Mtukufu akamuumba binadamu kama uwepo mmoja pekee ambamo ndani yake ipo dunia ya yale yaonekanayo na yale yasiyoonekana. Alam-al-Mulq na Alam-al-Malquut, yaonekanayo na yasiyoonekana yote yapo ndani ya binadamu. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoumba dunia ya yaonekanayo; yaani ulimwengu wa ki-maumbile hakusema;

**فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ**

**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.**  
**(Sura al-Mu'minoon 23:14)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoumba dunia ya yasiyoonekana (Malquut) pia hakujipongeza mwenyewe kwa kusema;

**فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ**

**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.**  
**(Sura al-Mu'minoon 23:14)**

Lakini ilipofika zamu ya kumuumba binadamu; alisema;

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.**  
**(Sura al-Mu'minoon 23:14)**

Ni kitu gani hiki cha uumbaji wa pekee uliopo ndani ya binadamu?

### **Upekee katika Uumbaji wa Binadamu:**

Katika Surah Mu'minun, kwanza viashiria vya Waumini vimetajwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

قُدُّ أَلْحَانَ الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ حَاسِعُونَ وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ الْلَّغْوِ  
 مُعْرِضُونَ وَالَّذِينَ هُمْ لِلرَّكَاهِ فَاعِلُونَ وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ إِلَّا عَلَىٰ  
 أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكُتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مُلَوِّمِينَ فَمَنْ ابْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ  
 هُمُ الْعَادُونَ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاغُونَ وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَاتِهِمْ  
 يُحَاطِطُونَ أُولَئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

“Hakika wamefaulu waumini. Ambao ni wanyenyeketu katika Swala zao. Na ambao hujiепusha na mambo ya upuuzi. Na ambao kwa Zaka ni watendaji. Na ambao wanazilinda tupu zao. Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyowamiliki mikono yao ya kuume. Kwani si wenye kulaumiwa. Lakini anayetaka kinyume cha hayo basi hao ndio wapetukao mipaka. Na wale ambao wanachunga amana zao na ahadi zao. Na ambao Swala zao wanazihifadhi. Hao ndio warithi. Watakaorithi Firdausi, wadumu humo” (Surah Mu'minun, 23:1-11)

Hao ndio watakaokuwa wawakilishi wetu, sio warithi tu wa ardhi lakini pia wa Firdausi. Sasa uone jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyomuumba mwakilishi huyu.

وَأَقْدَّ خَلْقُنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ طِينٍ

**“Na hakika tulimuumba binadamu kutokana na asili ya udongo.”**  
**(Sura al-Mu’minun 23:12)**

Tulimuumba binadamu kutokana na asili ya udongo. *Sulala* maana yake ni juisi, na sisi hatuwezi kutoa juisi kutokana na udongo lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweza kufanya hivyo. Unapokunuwa juisi yoyoyte ya tunda usianze kunywa mara moja, kwanza tafakari kuhusu kinywaji hicho. Juisi hiyo tamu imetokana na tunda tamu ambalo lilikuwa linaning’inia kwenye tawi. Na tawi hilo lilikuwa na ladha chungu. Tawi hili lilikuwa kwenye shina na shina kwenye mizizi na mizizi kwenye ardhi. Ndivyo ilivyo kwa udongo, hivi udongo nao ni mtamu sana? Kwa hiyo vyote hivi ambavyo vimekuja kutokana na tunda la chungwa; utamu wote huu ultoka wapi? Utamu huo ultoka ndani ya ardhi na ni Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye Ndiye aliyekongoa ardhi na kuweka juisi yake ndani ya tunda hili. Miti hii na mimea hii ni mashine zinazokongoa ardhi na kutengeneza juisi ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameziweka. Unapokula tikiti usianze kula mara moja tu, litazame angalau mara moja tu. Kontena hili la maji lina maji mengi sana ndani yake; nani aliyeyaweka maji hayo humo na kwamba pia katika ardhi ya jangwa kwenye mmea ambao ni mwelesi sana. Ardhi ambamo mmea umeota na kukua ni kavu. Maji hayo yalilindwa namna gani ndani ya tikititi? Vitu hivi ni vitabu vya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambavyo unatakiwa kuvisoma. Unapokula komamanga lakini wewe tazama jinsi yale maganda yake yalivyounganishwa na kila mojawapo. Tazama mahameli hii ambayo ipo katikati ya matabaka ya maganda. Hizi ni

desturi, asili na kazi ya usanii ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vitu vyote hivi unavyokula na vingine unavyokula na kusaza; unatakiwa kwanza utazame hii kazi, usanii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na halafu umshukuru Yeye.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema tulimuumba binadamu kwa asili ya udongo. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatutaarifu sisi kuhusu hatua kuu za uumbaji kama vile unavyokumbuka vituo vikuu vya safari ya treni. Vivyo hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfanya binadamu asafiri na kupita kwenye maelfu ya vituo lakini ni vituo vikuu tu ndivyo vinavyotajwa katika hadithi hii ya uumbaji wa binadamu katika Qur'an Tukufu.

Kutokana na asili ya udongo, tuliumba manii kwa namna gani? Hili halikutajwa ndani ya Qur'an Tukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliumba chakula kwa ajili ya binadamu kutokana na asili ya udongo, chakula hiki kiligeuka kuwa damu na kutoka katika hali ya damu kikageuka kuwa manii. Halafu tukaweka manii haya ndani ya:

لَمْ يَجِدْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ

Tuliyahamisha manii haya katika hifadhi iliyomakini. Sasa katika hifadhi hii makini tuliweka mfumo mwengine. Mama pia hajui nini kinachotokea ndani ya hifadhi hii makini. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema hakuiacha shughuli hii kwa mama; ni Yeye Mwenyewe ndiye aliyemuumba mtoto ndani ya nyumba ya uzazi. Kama Mwenyezi Mungu Mtukufu angemwachia mama kazi hiyo mama angejihusisha zaidi na macho makubwa ya mtoto, pua iliyonyooka na ngozi nyeupe ya mtoto, au angesema mimi nataka mtoto wa kiume. Haombi mtoto muadilifu; mtu katika sifa bainishi na maadili mema. Hatambui kwamba kama Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka angeweza kumuumba mtoto wake wa kike Kauthar (mwema sana).

ثُمَّ جَعْلَنَا نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ ثُمَّ خَلَقْنَا النُطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْعَغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْعَغَةَ عِظَامًا فَكَسَوْنَا الْعِظَامَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۝ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**“Kisha tukamjaalia awe tone katika makao yaliyo makini. Kisha tukaumba tone kuwa pande la damu na tukaliumba pande la damu kuwa pande la nyama, na pande la nyama tukaliumba kuwa mifupa na mifupa tukaivika nyama. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa Waumbaji.” (Surah Mu’minun, 23:13-14).**

Halafu tukamleta mtoto kutoka kwenye *Matiin* na kuwa katika *Alqa*, halafu kutoka kwenye *Alqa* na kuwa katika *Muzgha*; halafu *Muzgha* kuwa katika mifupa, halafu mifupa tukaivika nyama, halafu nyama tukaifunka kwa ngozi. Sasa kiumbe chote cha kimaada kilikamilishwa halafu tulifanya nini?

ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۝

**“..halafu tukamfanya kiumbe mwengine..”  
(Sura al-Mu’minun 23:14)**

Tulimpa kiumbe huyu uumbaji mwengine zaidi ambao ulikuwa ndiyo uumbaji wa mwisho. Hii ni hatua ambapo bahari mbili zili-kutana. Hiyo ilikuwa ni hatua ambapo kiumbe wa kimaada na kiumbe wa kiroho waliunganishwa pamoja. Huu ulikuwa uumbaji wa mwisho na baada ya hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema;

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

**“Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji”  
(Sura al-Mu’minun 23:14)**

Pongezi na salamu kwa Mbora wa waumbaji; ambaye alizifanya dunia hizi mbili kuwa moja katika uumbaji mmoja tu. Hii ndiyo sababu binadamu anaitwa kiumbe mwenye akili tambuzi. Imam Ali رض anasema: “Ewe binadamu! Hivi unajifikiria wewe kuwa ni chembe ndogo tu? Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka ulimwengu mpana ndani mwako lakini unayo mapungufu ya kutojitambua wewe mwenyewe.”

**Kwa Nini Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema “Nilipuliza Roho Yangu ndani ya binadamu.”**

**فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ**

**“Basi nitakapomkamilisha na nikampulizia roho Yangu, basi mwangukieni kumsujudia.” (Surah Hijr, 15:29).**

Ulimwengu unaouona huku nje upo ndani mwako. Unazio-na nyota na mwezi, vitu hivyo pia vipo ndani mwako na unaona *Alam-al-Malaquit* huku nje ambayo pia ipo ndani mwako. Hii ni hatua ya roho (*Ruuh*) ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu alipulizia ndani ya binadamu. Roho ya Mwenyezi Mungu Mtukufu haina maana ya roho hasa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu aliihusisha roho hii na asili Yake. Wanazuoni wanasema kwamba upanuzi huu kuitwa *Izaafat-e-Tashriqia* na maana yake ni heshima. Ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka kukipatia heshima kitu au mtu fulani huki-husisha kitu hicho au mtu huyo na asili hii. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwambia Ibrahim asafishe nyumba Yake (*Baitullah*). Mwenyezi Mungu Mtukufu haishi ndani ya Kaaba lakini anasema ‘nyumba yangu’ ili kwamba Kaaba iheshimiwe na kutukuzwa. Kwa ajili ya mtu fulani Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema mtu huyu ni mja (*Abd*) Wangu, yaani ni mja Wangu kwa sababu wen-

gine ni waja Wangu kwa ukarimu Wangu (Ni'mat) lakini huyu ni Wangu pekee. Mwenyezi Mungu Mtukufu alivihuisha vitu vingi na asili Yake na akasema ni vitu Vyake. Hii ni kwa sababu hadhi ya vitu fulani ni mfano wa kuigwa kuliko kukihuisha kitu kama hicho na mtu mwingine; hawasilishi haki zake kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anakihuisha kitu kama hcicho na Yeye Mwenye. Hapakuwepo na kingine chochote katika ulimwengu huu wote ambacho roho ya binadamu ingeweza kuhusishwa na kuwasilisha haki ya hadhi yake.

وَنَفْخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي

**“Na nikampulizia roho Yangu” (Sura al-Hijr 15:29)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambia Malaika kwamba atakapoluliza roho Yake ndani ya binadamu mnatakiwa kumsujudia. *Ruhu* imesemekana ambapo maana yake ni kwamba kiumbe huyu anao utukufu mkubwa, ukuu na uwezo, hivyo kwamba alihuisha asili yake na Yeye Mwenyewe na akawaambia Malaika kumsujudia kiumbe huyu. Kitu ambacho Malaika walikuwa hawakijui kabla ya kushuhudia kitu hicho, na halafu wakamsujudia.

### **Tofauti Bainya Fitra na Tabiyat:**

Roho ya binadamu ni chanzo cha Fitra (Hali ya kimaumbile) ya binadamu. Ilikwisha tamkwa hapo mapema kuhusu vitu vitatu walivyonyavyo wanadamu; *Fitra, Tabiyat na Ghariza*. Sasa ni wakati wa kuelewa tofauti baina ya Fitra na Tabiyat. Fitra ni mtindo maalumu wa uumbaji wa binadamu tu, ambao haukutumika kwa kitu kingine chochote. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba binadamu kama akili tambuzi ya Mwili na Roho. Mahitaji ya roho yanajulikana kama Fitra ambapo mahitaji ya mwili ni *Tabiyat*. Lakini kwa kuwa

vyote hivi viwili vinatimiziana mahitaji yao, vimewekwa pamoja. Mwili pia una uwezo mwangi kwa ajili ya msaada wa roho. Hiyo roho iliopo ndani ya mwili ni uhai ambao ultajwa kabla kwamba ulipewa tu heshima ya hadhi ya roho. Binadamu ni mapambano baina ya Mwili na Roho, na mapambano haya yanatambuliwa kwa misamiati mbalimbali katika Qur`ani Tukufu kama *Taqwa* (uchaji Mungu), *Fujuur* (utendaji dhambi), *Aflaha* (mafanikio), na *Dasa-saha* (ukandamizaji).

Tuliweka vitu hivi viwili mwili na roho na mahitaji yao; Fitra na Tabiyat ndani ya binadamu na sasa vyote hivi vitapambana. Na sasa tuangalie katika vita hivyo vya Fitra na Tabiyat, ni yupi atakayeibuka mshindi. Kama binadamu akiitumia Tabiyat kuiamsha Fitra yake, binadamu atafaulu, lakini kama Fitra itashindwa na kihinikizwa chini ya Tabiyat basi binadamu atakuwa ameangamia. Wakati Tabiyat inapotawala, binadamu huanguka na kushuka chini ya hadhi ya utu. Hadhi yake hushuka na kwenda chini mno hivyo kwamba huenda chini ya kiwango cha hayawani.

Mapambano ya Karbala yalikuwa baina ya Fitra na Tabiyat, upande mmoja ulikuwa wa wale waliotawaliwa na Tabiyat na upande mwagine ulikuwa wa wale waliotawala Tabiyat yao kwa kutumia Fitra. Mapambano haya huwa yapo katika kila taifa ambapo Haki na Batili hupambana. Kila taifa lina Husein na Yazid. Wakati mwagine Yazid huja kwa umbo la Firauni, Nimrod na Shaddaad. Na wakati mwagine roho ya Husein huja katika umbo la Ibrahim, Musa na Isa. Wakati wowote Fitra inapotiishwa, ukuaji wa Uyazid huanza ndani mwake. Wale waliokuwa wanatongoa *Kalima-e-Rasuul* walitokeza na kumuua mjukuu wa Mtume kwa namna ya kikatili sana na kuwafanya ukatili hata wanawake na watoto watakatifu wa familia ya Mtume ﷺ.

## **Msingi wa Kanuni Katika Kuelewa Dini iliyo Sahihi:**

Katika Surah Bani Israel;

وَلَقْدْ كَرِمْنَا بَنِي آدَمَ

**“Hakika tumewatukuza wanaadamu” (Sura al-Israa’ 17:70)**

*Karamat* (daraja kubwa la kifungua mimba) kuliko viumbe vingine vyote. Wajibu wa binadamu sasa ni kuhifadhi karamat hii. Zipo Karamat za aina mbili; aina moja ya Karamat ni ile ambayo kila binadamu huumbwa na kuzaliwa nayo, na aina ya pili ni ile ambayo binadamu anatakiwa kuijenga na kuikuza kwenye ile Karamat ya aina ya kwanza. Wanazuoni husema *Karamat* na *Sharafat* (heshima) ni za aina mbili; aina moja ni ile ya Fitra na aina ya pili ni ile ambayo binadamu mwenyewe hufanya kazi ya kuipata na kuhifadhi uadilifu na heshima hii ya Fitra yake. Dini imewasilishwa kwa binadamu na chanzo cha utukufu wake, heshima na upendeleo wake ni Fitra yake ambayo ni umbile maalumu alilokabidhiwa binadamu na sasa binadamu anapaswa kuhifadhi hii sifa bainifu kwa sababu wakati mwingine sifa hii bainifu hupotezwa.

Hili ni somo linalohitaji tafakuri na uelewa wa kina; na tunatakiwa kuelewa na kuchunguza vitu hivi kwa utaratibu aliotufundisha mkuu na lango la elimu Imam Ali عليه السلام. Anasema kwamba wakati Mtukufu Mtume صلوات الله عليه وآله وسلام alipowasilisha suala moja la kidini kwake suala hilo lilifungua milango 1000 ya elimu kwa ajili yake na kutoka kwenye kila mlango ilifunguka milango mingine 1000 kwa ajili yake na kutoka kwenye kila mlango aliweza kufungua milango mingine zaidi 1000 ya kujitambua yeeye mwenyewe. Huu ndio ubora wa Mwalimu (Muallim) ambaye dhana moja inayofundishwa naye hufungua milango mingine milioni moja ya uelewa. Mtukufu Mtume صلوات الله عليه وآله وسلام anasema elimu ambayo amefundishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu hai-

kuwa chache na vipande vipande; anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa elimu katika muundo wa mambo mengi. Ila namna ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amenipatia elimu ambayo katika busara moja, zinatokeza busara zingine mamilioni. Na wakati Mtukufu Mtume ﷺ akimfundisha mtu hufanya katika namna ileile; kwamba maana moja ambayo alimfundisha Amiri wa Waumini Imam Ali ؓ ye ye alielewa na kufasiri maana milioni moja. Kwa hiyo mfuasi wa Imam Ali ؓ anatakiwa awe hivyo ambapo kanuni moja ya kidini inafundishwa kama haikutatua matatizo milioni moja lakini angalau inaweza kutatua matatizo kumi katika maisha yetu. Hili linaweza kutokea tu pale ambapo akili ikiwa pana na iliyo tayaridh kupo kea mashauri mapya lakini akili finyu ni ile isiyolewa kitu chochote.

Mtukufu Mtume ﷺ aliye tuliwa kwa ajili ya Ummah wa Kiislamu. Alipewa mwujiza wa Kitabu. Ni jambo la kustaa jabisha kwamba Ummah ambao Mtume wake mwujiza wake ni Kitabu umejitenga mbali na Kitabu na wanatosheka na kusikiliza tu. Kitabu ni mwujiza wa Mtukufu Mtume ﷺ na ni kitakatifu sana. Kila mtu anatakiwa kuwa na maktaba yake binafsi kwenye makazi yake. Tunatakiwa kujihusisha na vitabu kwa sababu sisi sio vituo vya ufunuo (*Wahy*) kwa hiyo vitabu ni chanzo cha wasomi. Maasumu walikuwa na njia maalum ya kupata elimu na Mwenyezi Mungu Mtukufu alifanya mipango maalum ya kuwapa elimu Maasumu hao. Aliwafanya Maasumu kuwa onesho la elimu Yake.

Kanuni ya kisomi ni kwamba kila kitu ambacho binadamu anatakiwa kukielewa anapaswa akielewe. Pamoja na kwamba chanzo cha dini ni Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini dini ni kwa ajili ya binadamu. Dini haitaelewaka isipokuwa hapo ambapo binadamu atajitambua mwenyewe. Kama mtu anataka kuielewa dini bila kumwelewa binadamu kwanza basi mtu huyo hataweza kuelewa.

## دِيْنُ الْفَيْمَةِ

**“Dini iliyo sawasawa” (Sura al-Bayyina 98:5)**

Badala yake atapinda na kuanzisha dini yake mwenyewe, au ataharibu dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo sehemu kubwa ya Qur`ani Tukufu inazungumzia suala la Mtu Kujitambua Mwenyewe ambapo binadamu anafundishwa kuhusu yeye mwenyewe, ambapo hilo ndilo somo la kitabu hiki.

### **Uimamu (Uongozi) - Haja ya Fitra:**

Ukikusanya aya zote za Qur`ani Tukufu zinazohusu sheria za Kivitendo za Uislamu zinafika kwenye idadi ya mia tano (500) pamoja na zile zilizorudiwa zaidi ya mara moja. Zipo aya mbalimbali kuhusu Swalaa na Zaka; zipo aya ambazo zinahusu Hijja, Swaumu, Halali, Haramu, na kama ukihesabu idadi yao zinafika mia tano (500) ambapo idadi ya aya zote za Qur`ani Tukufu ni zaidi ya elfu sita (6000+). Hii maana yake ni kwamba aya mia tano (500) ni zile aya ambazo zimezalisha *Tauihul Masail* (mkusanyiko wa sheria za kivitendo ambazo zime-tolewa na *Marjae Taqliid*). Maelfu ya Fatwa hizi katika kitabu hiki ki-moja zitokanazo na *Marja-e-Taqliid* ni mwalimu wako na unatakiwa kufanya marejeleo humo kwa ajili ya vitendo vya kidini. Kwa kuwa kitabu hiki ni mwalimu wako unatakiwa kufanya mazoezi kuhusu yale yaliyomo humo na hata kama Fatwa haiko sahihi basi pia Mwenyezi Mungu Mtukufu atakusamehe kwani wewe utakuwa umetenda kufuatana na Maelekezo ya Mwalimu. Lakini kama hukurejelea kwa Marjae (njia za sheria za kivitendo) na umetekeleza kivyako basi kitendo chako si sahihi Mwenyezi Mungu Mtukufu hatakusamehe. Baa-dhi yetu husema kwamba wao hawatekelezi sheria za kivitendo kufuatana na *Taqliid* ya watu ambao sio Maasum, bali huwa wanatekeleza sheria za kivitendo kufuatana na *Taqliid* ya Maasum tu; lakini in-

apokuja kwenye Maasumin ﷺ wanasema hatuwafuati wale ambao wapo kama binadamu (*Bashar*) (upinzani ambao walizusha kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa mtu wa kawaida kama wao). Wameweka kisingizio hicho kwa kila mtu.

Maasum ﷺ wenyewe wamesema kwamba wao wamecateuwa wao hao Marajii, na ni kweli kwamba Maasum kama sharti la kutimiza haja huwafanya wale ambao sio Maasum kuwa waalimu (*Hujjat*). Ni katika namna hiyohiyo kwamba Amiri wa Waumini, Imam Ali ﷺ alimteuwa Malik Ashtar kuwa Hujjat huko Misri. Malik Ashtar hakuwa Maasum, kwa hiyo kama Wamisri wangekataa na kusema kwamba wao hawatamuata mtu ambaye sio Maasum, basi Imam Ali ﷺ angesema nini? Angesema kwamba ni yeye ndiye aliyempa mamlaka hayo, na amepewa mamlaka hayo ya urithi na Mtukufu Mtume ﷺ. Na Mtukufu Mtume ﷺ pia hakuja kivyake, yeye ali-teuliwa kuwa Mtume na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo alisema yeyote ambaye atamkataa Malik atakuwa amemkataa Ali, na yule ambaye amemkataa Ali atakuwa amemkataa Mtukufu Mtume ﷺ na yule ambaye atamkataa Mtukufu Mtume ﷺ atakuwa amemkataa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa hiyo hioneshi tofauti kama katika zama hizo Ali alipomteuwa Malik kuwa Hujjat kwa Wamisri na katika zama za leo Faqih Mwadilifu anateuliwa kuwa Hujjat wa watu. Maasumin ﷺ wanasema kwamba wale wanaowakataa Mafaqiih Waadilifu walioteuliwa na wao ni sawa kwamba amewakataa WAO na mtu ambaye amewakataa wao ni sawa na kumkataa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Dini yetu ina viwango na vigezo. Katika Ushi'ah kila kitu kina kiwango. Kipo kiwango cha amali, imani, tabia, dunia, Kiyama na tutapimwa kwa kufuata viwango hivi. Uimamu umeten-genezwa kufuatana na kiwango.

Maana halisi ya Uimamu ni kiwango. Uimamu ni neno la Kiarabu. Kama ambavyo imekwishatamkwa kabla ni kwamba maneno

husafiri; huzaliwa katika lugha na yanapoingia kwenye sayansi au dini huanza kuwakilisha maana za theolijia. Ngoja nikwambie mfanano ili uweze kuelewa maana ya Uimamu. Utakuwa umemuona fundi mwashi ambaye hujenga ukuta wa nyumba. Wakati fundi mwashi anapojenga ukuta anahitaji kuhakikisha kwamba ukuta umenyoooka na hii inatakiwa kuhakikishwa kuanzia na tofali la kwanza. Kama tofali la kwanza halikuwekwa sawa basi ukuta wote unaosimamishwa hautakuwa umenyoooka na utaanguka baada ya muda mfupi. Kitendeakazi ambacho fundi mwashi huyu hukitumia kinaitwa pimamaji au kamba ya kupimia tabaka za matofali, na zipo aina mbalimbali za vitendeakazi kama hivyo, kama vile vyenye zebaki (*mercury*) na hata vile vyenye dijitali siku hizi. Lakini katika zama za kale kitendea kazi hiki kilitengenezwa kwa kamba, na ambacho kilitumiwa kuhakiki kazi ya fundi. Kama fundi mwashi hakutumia kitendea kazi hiki na akafanya jeuri ya kudai kwamba hahitaji kitendeakazi chochote kwa sababu wakati wowote anapojenga kuta zinakuwa zime-nyooka, kazi yake itakuwa haifai. Wakati mwingine baadhi ya kuta hujengwa zikiwa zimepinda lakini hupigwa lipu ya simenti kufanya ukuta uonekane umenyoooka. Kuta za namna hiyo haziaminiki na mtu hawezi kujenga ghorofa kwenye ukuta uliopinda. Kamba hii inayotumika katika kuhakiki unyookaji wa ukuta huitwa “Imamu” na Waarabu katika lugha ya Kiarabu. Neno hili la Kiarabu lilitumika kwa kusudio hili.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba binadamu, na alisema kabla yake kwamba binadamu hakuumbwa katika hali ya ukamilifu badala yake aliambiwa autafute na kuupata ukamilifu ili awe mtu (yaani kukuza na kulea sifa bainishi za mtu). Sasa tutatambua ni kwa nini tunahitaji Imamu. Sio kwa sababu ya matamanio ya kidunia ya leo kwamba tunahitaji Imamu. Ilikuwa kama Bani Israel ambao walimhitaji Musa kwa ajili ya kuwa-

pa vyakula vitamu. Musa alikuwa anakwenda kwao na ufunuo (*Wahy*) na wao walimwambia aache mahubiri hayo kwa sababu yalikuwa yanawachosha. Sasa Musa angefanya nini? Walikuwa wakimwambia: “Ewe Musa, tumechoka kula chakula cha aina moja kila siku, funika kitabu hiki chukua kikapu hiki cha sokoni; hatuna vitunguu, vitunguu thaumu na mboga. Tumechoka kula nyama sasa, tunahitaji mboga.” Haya ni mahitaji ambayo waliyawasilisha kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Musa akawaambia ninyi ni wapumbavu ambao mnadai mambo madogo badala ya kudai mambo makubwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuwaleta Mitume na Maimamu ili waje kutimiza matamanio ya binadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka silika na matamanio (Ghariza), Tabiyat na Fitra ndani ya binadamu, lakini hakuwatuma Maimamu kwa ajili ya matamanio na Tabiyat ya binadamu, bali Maimamu walitumwa kwa ajili ya kutunza na kukuza Fitra ya binadamu, Maimamu ﷺ hawakutumwa kwa makusudio ambayo Bani Israel walimtumia Imam. Bani Israel siku zote walikuwa wakilalamika kuhusu masuala yahusuyo matamanio. Wakati mwingine walisema hawana maji halafu walipopewa maji wakatoa hoja kwamba wao wapo katika makabila 12 kwa hiyo walikuwa wanahitaji chechem 12 kwa ajili ya moja kwa kila kabila.

Amiri wa Waumini ﷺ pia aliliambia jeshi lake na wafuasi wake huko Kufa kwamba alitaka kuwachukua na kuwapeleka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wao walikuwa wanatamani kumpeleka yeye kwa mintarafu ya matamanio ya dunia. Yeye alitaka kufanikisha kitu kingine kuitia kwao ambapo wao walitaka kumfanya yeye kuwa njia ya kufanikisha kitu kingine tofauti. Mwenyezi Mtukufu amewatumwa Maimamu ﷺ kwa kusudio la mahitaji ya Fitra.

Fitra ilimwambia Mwenyezi Mungu Mtukufu “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Umeniumba mimi katika jinsi hii (ambayo napaswa kujikamilisha mwenyewe) basi nakuomba nipe na mwongozo pia.”

اَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ

### “Tuongoze njia iliyonyooka” (Sura al-Faatiha 1:6)

Haina maana ya huduma ya matamshi tu. Hii ni haja ya Fitra. “Ewe Mola Wangu, ikiwa Wewe umeniumba mimi bila kunikamilisha na unataka mimi niwe mtu basi tafadhali nakuomba unipe elimu ya kuniwezesha mimi kujikamilisha mwenyewe pia.” Mwenyezi Mungu Mtukufu alituma elimu ya kujikamilisha, ambayo ilikuwa ni Kitabu kitakatifu, lakini sasa Fitra ilitoa madai zaidi kwamba ipewe elimu kwa ajili ya kujijenga yenyewe lakini pia sasa ilihitaji viongozi.

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ

### “Njia ya wale uliowaneemesha: (Sura al-Faatiha 1:7)

Ambayo maana yake ni “nipe mfano wa kuumba Fitra (Hali ya kimaumbile) pia ili kwamba isije ikatokea kwamba uso wa Fitra ya kila mtu utonekana kuwa tofauti. Kwa hiyo sasa nipe Mfano bora, Fitra ambao tutawaangalia wakati wa kujikamilisha sisi wenyewe ili kwamba mifano yote iwe sawa. Kwa kuwa sasa tumekuja kujikamilisha sisi wenyewe, Fitra yetu, uwepo wetu, tunapaswa kutengeneza katika njia ileile ambayo fundi mwashi hujenga ukuta wa nyumba. Qur`ani Tukufu inasema:

أَفَمَنْ أَسَسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ تَقْوَىٰ مِنْ اللَّهِ وَرِضْوَانٍ خَيْرٌ

“Je aliyweka msingi wa jengo lake juu ya kumcha Mwenyezi

**Mungu na radhi zake ni bora” (Sura at-Tawba 9:109)**

Mtu aliyeweka msingi wa uwepo wake Kwenye Ucha Mungu na Radhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, uwepo wake utakuwa tofauti.

*Asasa, Maana yake ni kuweka msingi. Hivyo mtu aliyeweka msingi wake kwenye Ucha-Mungu atapata mafanikio ambapo mtu aliyeweka msingi wake kwenye uovu na ufisadi ataangamizwa.*

﴿أَمْ مَنْ أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ شَفَافٍ جُرْفٍ هَارٍ فَانْهَارَ بِهِ فِي نَارٍ جَهَنَّمَ﴾

**“..... au aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo lin-alomomonyoka, na likamomonyoka likaanguka pamoja naye katika moto wa Jahannam.....” (at-Tawbah; 9:109).**

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumuumba binadamu katika hali ya ukamilifu, na kwamba binadamu anapaswa kujikamilisha mwenyewe, kwa hiyo sasa binadamu anapaswa kuanza kazi hii ya ujenzi. Kwa namna kama ile ambayo fundi mwashi hujenga ukuta; anapoweka tabaka moja la matofali, huhakiki kwa kutumia kitendeakazi hiki kama ukuta unakwenda juu ukiwa umenyooka au hapana. Kwa hiyo ili aweze kuhakikisha kama ukuta wa matofali, udongo wa kawaida au mawe umenyooka inahitajika kamba hii au kitendeakazi chochote basi katika kuhakiki unyookaji wa ukuta wa uwepo wa binadamu tunahitaji kitendeakazi kikubwa zaidi na bora. Kwa hiyo baada ya kumkabidhi binadamu kazi ya kujikamilisha mwenyewe na halafu akampa nyenzo za kazi hiyo, pia Mwenyezi Mungu Mtukufu alimteua Imamu kwa ajili yao.

Imamu anahitajiwa na Fitra kwa sababu unapojenga jengo ambaloo unajijenga mwenyewe unahitaji Imamu pia. Imamu ni kipimo cha kupimia kama unakwenda kwa kufuata njia iliyonyooka au hapana. Imamu awepo hapo nawe uangalie ujenzi wako; kama ujenzi wako unafanana na ule wa Imamu basi wewe uwe mtu wa kush-

ukuru. Kama ikitokea wakati fundi mwashi anajenga ukuta anaketi juu ya ukuta na kusema kwa maneno; "kitendeakazi, kitendeakazi, kitendeakazi" si rahisi kuhakiki kama ukuta umenyoka au hapana. Fundi mwashi anapaswa kuupima ukuta kivitendo. Kwa hiyo binadamu hawesi kufikiriwa kuwa mfuasi wa Imamu isipokuwa awe amepima na kuhakiki Fitra yake kwa kumtumia Imamu. Ni nani hawa Imamiyya (Wafuasi wa Imamu)? Imamiyya ni jina la jumuiya ambayo uwepo wake umenyooka kwa sababu Imamu ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu alimteua yupo na jumuiya hiyo. Uimamu umewekwa kwa ajili ya binadamu na vitu vyote vile ambavyo vime-jumuishwa kwenye Uimamu haviwezi kueleweka isipokuwa binadamu aeleweke kwanza.

Kwanza binadamu anahitaji kutambuliwa halafu ndipo tu ambapo haki za Uimamu nazo zitatambuliwa. Kama mtu akijaribu kuutambua Uimamu kabla ya kumtambua binadamu basi hataweza kuelewa kitu. Kwanza amtambue binadamu ni nani, basi hapo ndipo atakapotambua mahitaji ya binadamu na hapo ndipo atakapotambua vyema sababu ya kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu amewateua Maimamu.

Hivyo katika Qur'ani Tukufu sheria za kivitendo (*Ahkam*) zime-zungumziwa katika aya mia tano (500) mionganoni mwa aya elfu sita (6000+) zilizomo ndani ya Qur'ani Tukufu. Hizi aya za Ahkam zime-zungumziwa kwa hiyo ni kitu gani kingine kimezungumziwa katika aya nyingine. Chochote kile ambacho kimesemwa katika aya elfu sita (6000+) ni vitu vile ambavyo baada ya kujifunza humfanya binadamu atambue haja ya zile aya mia tano (500) zinazoshughulikia sheria kivitendo za Uislamu. Hizi aya elfu sita (6000+) zilimpatia binadamu utambuzi (*Maarifat*); zinfasili, zinaeleza, zinafafanua na kufundisha binadamu kwa binadamu. Aya hizi humtaarifu binadamu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuumba yeze kama ki-umbe kitukufu na akakikabidhi *Karamat*.

- Qur`ani Tukufu imepangwa katika namna iliyo nzuri sana. Ni imani iliyorasimishwa na madhehebu ya Shi'ah kwamba jinsi aya na Sura za Qur`ani Tukufu zilivyopangwa leo zinaendana kabisa na ni kama katika jinsi alivyozikusanya Mtukufu Mtume ﷺ. Mzee mmoja mwanazuoni wa madhehebu ya Shi'ah alifanya kosa la kisomi lakini alitubu baadaye kuhusu kosa hilo. Mwanazuoni huyo alichapisha kitabu juu ya kupidishwa kwa Qur`ani Tukufu lakini baadaye alitambua kosa lake na akingali bado hai alisahihisha kosa hilo na akachapisha jibu kuhusu kile kitabu cha mwanzo na alitamka kwamba kile kitabu cha kabla yake kilichapishwa kimakosa.

Jibu aliloandika katika kitabu kingine halikupendwa na watu na ni kitabu hiki ndicho kinachotumiwa na watu wengine leo hii kama rejea ya kukashifu Ushi'ah; kwamba Shi'ah wanaamini kwamba Qur`ani Tukufu imepindishwa. Qur`ani Tukufu iliyopo mikononi mwetu leo ni ile ile ambayo ilifunuliwa kwa Mtukufu Mtume ﷺ mfuatano uleule ambao Mtukufu Mtume ﷺ alikusnya. Qur`ani Tukufu ilitereshwa katika mfuatano mmoja na ikakusanya katika mfuatano mwingine. Aya ya kwanza iliyoteremshwa ipo katika Sura ya mwisho ambapo aya ya mwisho kuteremshwa ipo katika Sura ya tano. Ukusanyaji huu ulifanywa na Mtukufu Mtume ﷺ. Kila aya iliyoteremshwa Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia masahaba ni katika Sura gani aya hiyo iwekwe. Sura pia zilitengenezwa na Mtukufu Mtume ﷺ.\*

Kwa upande mmoja Qur`ani Tukufu inasema kuhusu *Sharaf* na *Karamat* ya binadamu na halafu tazama kinachokuja katika aya ya jirani.

وَلَقْدْ كَرِمًا بَنَى آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ  
وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِمَّنْ حَلَقْنَا تَعْظِيْلًا

**“Hakika tumewatukuza wanadamu na tumewabeba nchi kavu na  
baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa  
fadhiba kubwa kuliko wengi mionganii mwa tulioawaumba.”  
(Bani Isarail, 17:70)**

Baada ya aya hii, aya ya 71 inaanza;

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامٍ هُمْ

### Siku tutakapowaita watu kwa Imamu wao..... (Sura al-Israa 17:71)

Imamu huyu atakuwa nani? Imamu atakuwa kile kipimo ambacho binadamu atafanana nacho. Wale ambaao wamekengeuka watafufuliwa wakiwa na Maimamu wao waliokengeuka, na wale ambaao waaminifu watafufuliwa na Maimamu wao waaminifu, bila kujali kaulimbiu walizokuwa nazo midomoni mwao. Waoga watafufuliwa na Maimamu waoga, wanaojiheshimu wenyewe watafufuliwa na Maimamu wao wenyewe kujiheshimu wenyewe. Jinsi ummah ulivyokuwa, Maimamu wao watakuwa hivyo pia.

Wapo Maimamu wa *Hidayat* (mwongozo) na pia Maimamu wa *Naar* (Moto) ambaao watawachukua wafuasi wao Jahannam. Tutam-fufua kila mmoja na Imamu wake.

Kwa hiyo kwanza tunatakiwa kumwelewa binadamu, sehemu kubwa ya Qur`ani Tukufu inamuelezea “binadamu” kwa mtu. Ni hapo tu ndipo mtu ataielewa Qur`ani Tukufu, Dini na Madhehebu ya Uimamu. Kila kitu ambacho kimetokea hapa duniani kipo katika jinsi ileile.

### Binadamu wa Bara la Magharibi:

Kama ukiitazama Ulaya, watu wa huko pia kwanza walimwelewa binadamu na chochote walichokipata kuhusu binadamu. Wao waliten-geneza itikadi yao, jamii na utamaduni vikiwegemezwa kwenye

uelewa wao kuhusu binadamu. Utamaduni wa nchi za Magharibi unaitwa utamaduni na ustaarabu wa binadamu lakini kwanza mtazame binadamu wa Magharibi. Binadamu wa Magharibi wala hana Fitra, ye ye ana Tabiyat tu. Wanafikira fulani wa Kimagharibi hukanusha hata uwepo wa Tabiyat ndani ya binadamu; wao wanasema kwamba Fitra na Tabiyat ni vitu vilivyobuniwa, na kitu pekee kilichopo ndani ya binadamu ni silika (*Ghariza*). Na sio silika zote, wao wanasema ipo silika moja tu ambayo ndio msingi wa utu wa binadamu na hiyo ni matamanio ya ngono. Fasili haitoki kwa watu wa kawaida wa Magharibi bali inatoka kwa watu wanafikira mashuhuri wa Kimagharibi. Ni magharibi hiyohiyo ambayo sisi huifikiria kama pepo yetu na ambayo ndio hatima ya matamanio yetu. Baadhi ya watu wameweza kufaulu kufika kwenye pepo hii na halafu wanaandikia marafiki zao kwamba chochote kinachosemwa na Maulana kuhusu pepo kama vile mito, chemchem na kadhalika vyote viro hapa Magharibi. Pepo hii ya Magharibi imeegemezwu kwenye utambuzi wa binadamu, na mtu wa Magharibi hana Fitra na hana hata Tabiyat; msingi wake ni silika na silika hiyo ni matamanio ya ngono.

Mwanafikira mmoja, Darwin alimwasilisha binadamu kama spishi ya wanyama iliyopita kwenye mageuko kadhaa kabla ya kuwa binadamu. Yeye anasema kwamba mnyama wa chembe moja ya uhai alitokeza katika uwepo halafu aliendelea kukua na kubadilika kuwa nyani, na kutokea hapo akabadilika kuwa mnyama. Huyu ni binadamu wa Magharibi ambaye ni uso uliokuwa wa mnyama kwa hiyo kuna haja gani ya Fitra? Huyu sio binadamu ambaye Qur'ani Tukufu inamwasilisha. Kwa kuwa upo mfanano katika muonekano baina ya nyani na binadamu wao husema kwamba mkia wa nyani ulidondoka na mnyama huyo akawa binadamu. Lakini kile amba-cho Qur'ani Tukufu inasema ni kinyume; Qur'ani Tukufu haisemi kwamba nyani au sokwe waligeuka kuwa binadamu, Qur'ani Tukufu

inasema kwamba binadamu alijishusha daraja na kuwa katika daraja la chini sana hivyo kwamba alibadilika kuwa nyani.

Kwanza walimuona binadamu kwa njia hii; mwanafikira mmoja aliandika historia ya binadamu kama mnyama aliyegeuka kuwa binadamu baada ya mkia wake kudondoka, shingo yake ikanyooka, na kiwiliwili chake kikanyooka na kwa mabadiliko kadhaa ya viungo, nyani akageuka kuwa binadamu. Halafu akatokeza mwanafikira mwingine akazungumzia jinsi binadamu mwenyewe alivyoumbwa. Sigmund Freud ni bingwa wa saikolojia mashuhuri wa Kimagharibi na wanafunzi wa saikolojia wamekwishakutana na jina hili. Huyu ni msomi wa utamaduni wa Kimagharibi. Alisema kwamba binadamu ni jina la matamanio ya ngono na vitendo vyake vyote vipo katika msingi wa ngono. Uhusiano wote wa binadamu na wenzake umeegemezwa kwenye maslahi ya ngono. Haya yalikuwa maono ya kidhalimu, yasiyo ya kibinadamu na ya kionevu yaliyotolewa na Freud kuhusu binadamu. Hata aliweza kusema kwamba uhusiano wa watoto na vichanga na wazazi wao pia upo kwenye misingi ya ngono. Anasema kwamba mtoto mchanga huvutiwa na mama yake kwa ajili ya kunyonya maziwa ambayo ni chakula chake, pia ni kwa sababu ya silika ya ngono. Anaendelea kusema kwamba wakati wa utoto wake alikuwa anampenda mama yake na alikuwa anamuonea wivu baba yake. Hii ilikuwa kwa sababu ya mvuto wa ngono wa jinsia tofauti ambao binadamu anao. ([http://en.wikipedia.org/wiki/Sigmund\\_Freud#Psychsexual development](http://en.wikipedia.org/wiki/Sigmund_Freud#Psychsexual_development))

Kwanza walimtambua binadamu kwa namna hii, sasa walipaswa kutengeneza mfumo kwa ajili ya binadamu ambao pia ulikuwa kwenye mpangilio huo. Mifumo yoyote ile kama: elimu, utamaduni, uchumi, na mifumo yote ya kijamii walizozienda iliegemezwa kwenye msingi wa jinsi walivyokuwa wanamtambua binadamu. Mifumo hii ilikuwa na bado mpaka sasa, sio mifumo ya kibinadamu. Leo hii

sisi tupo tayari kufanya lolote kwa ajili ya Utamaduni wa Kimagharibi. Iqbal alikwenda kwenye utamaduni huu na alirudi na kulionya taifa lake kuwa na hadhari kuhusu Utamaduni wa Kimagaharibi. Sisi husema kwamba watu wa magharibi wameendelea sana.

Mzee mmoja msomi amezungumzia maendeleo yao katika maneno yake, anasema kwamba maendeleo yao yote yameegemezwa kwenye kazi mbili ambazo zimegawanywa katika shughuli mbili za viwanda. Nusu ya viwanda vyao huzalisha bidhaa zinazoamsha matamanio na nusu nyingine huzalisha bidhaa za kumaliza hayo matamanio yaliyoamshwa.

Sasa na tumtazame binadamu wa Qur'ani Tukufu, tutazame taswira ya binadamu wa Qur'ani Tukufu. Binadamu wa Qur'ani Tukufu ameumbwa kutokana na Fitra; binadamu huyu anayo Tabiyat na pia silika na matamanio ndani mwake, lakini siri ya binadamu huyu kuwa mwenye kupendelewa na mashuhuri mionganoni mwa viumbe vingine vyote ni Fitra yake. Binadamu wa Qur'ani Tukufu ni mkuu, aliyepevuka, mashuhuri, muadilifu, wa kuheshimika na yeye ni mwakilishi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hapa duniani. Hivyo mfumo wa maisha utakuwa kufuatana na uwakilishi wa binadamu. Kwa hiyo ili kuweza kubadilisha mfumo kwanza hapana budi binadamu abadilishwe.

### **Tabiyat:**

Tulitaja vitu vitatu vya msingi kuhusu binadamu na ambavyo huchakachuliwa mara nyingi. Binadamu anayo Fitra, halafu anayo Tabiyat na Ghariza. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimumumba binadamu kwa kumpa umbile la binadamu na halafu akampa umbile lisiloonekana ambalo ni roho. Mahitaji ya roho yanajulikana kama Fitra ambapo mahitaji ya mwili yanajulikana kama

Tabiyat. Huu ni uumbaji maalum ambao haupo kwenye viumbe vingine. Huu ni

### فِطْرَةُ اللَّهِ

(uelekeo wa kimaumbile uliotengenezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu). Fitra ambayo ni uumbaji mahsusini kwa binadamu na sifa maalum ni pale ambapo roho na mwili vilipounganishwa pamoja na kuumba uwepo.

Pia mwili ni sehemu ya binadamu lakini uhalisi wa binadamu upo ndani ya roho yake. Hii ndio sababu mwili hubaki hapa lakin ni binadamu huendelea mbele. Binadamu mwili wake hufariki na kuzikwa kulingana na hadhi yake. Mwili upo kama nguo ya roho. Kwa kuwa mwili ni miliki ya binadamu pia nao hupata heshima ya kuzikwa kiheshima. Si kwamba mwili wa binadamu hufariki wakati wa kifo tu, hata wakati wa uhai wa binadamu hufariki mara kadhaa na hurudishwa tena kwenye uhai.

Hii ni sheria ya mwili kwamba chembe hai za mwili huvunjika, hufariki na chembe hai mpya huzaliwa. Katika miaka michache mwili wa binadamu hubadilika lakini hufika wakati ambapo mwili hutulizwa kiajali au ambapo wakati wake umekwisha. Kama asemavyo Haafidh: “Roho ilikuwa inaondoka nikasema hapana usiondoke” roho ikajibu “nitafanya nini na nyumba hii inavunjwa na kuharibiwa!” Roho inasema; “nimekwishachukua kazi ambayo nilipaswa kuchukua kutoka kwenye mwili huu sasa naondoka.”

Kifo ni pale roho inapoondoka kwenye mwili na mwili huo kuinjia kwenye dunia ya kaburi, ambapo mwili huingia ndani ya kaburi ambalo ni shimo lililochimbwa kwenye ardhi. Dunia ya kaburi ni tofauti na shimo la kuchimbwa ardhini. Mwili hauulizwi maswali au kufanyiwa hesabu ndani ya shimo hili. Ni sawa kama vile nguo

inayoning'inia ndani ya kabati la nguo ambapo hawapo Munkara na Nakir. Nguo haiwezi kuulizwa maswali kwamba ilichafuka mara ngapi, ilifuliwa na kupigwa pasi mara ngapi. Kama ukiuuliza mwili kwa nini rangi yako ni nyeusi sasa kosa lipo wapi hapa.

Maswali yote na majibu yote yanakuwa ndani ya dunia ya kaburi ambayo yatakuwa na roho. Roho haikuumbwa ife; yenyewe hupata uhamisho. Kifo ni jina la uhamisho. Roho ambayo iliunganishwa kwenye dunia hii ya kimaumbile sasa imetenganishwa kutoka hapo na imehamishiwa kwenye dunia nyingine. Roho itaulizwa maswali na mwili unabaki katika dunia hii. Roho inapokuwa hapa duniani inahitaji mwili kwa sababu ya jinsi ilivyoumbwa, ili roho iweze kufanikisha kusudio lake la kuumbwa. Wakati roho ipo na mwili huu, mwili pia huwa na mahitaji yake.

### **Maana halisi ya neno “Tabiyat”:**

Qur’ani Tukufu imeandikwa katika lugha ya Kiarabu na ili tuweze kuielewa Qur’ani Tukufu tunahitaji msaada kutoka lugha ya Kiarabu. Qur’ani Tukufu imetumia neno hili Tabiyat mara nyingi. Mwanzoni mwa Sura Baqarah neno Tabb limetumiwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemwambia Mtukufu Mtume ﷺ: “Ewe Mtume usichoshwe na baadhi ya watu.” Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na shauku sana ya kuwaongoa wale waliopotea; alikuwa anafanya jitihada kubwa sana ya kuwaongoza hadi anachoka sana. Hapa ndipo Qur’ani Tukufu inasema:

سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ  
خَتَّمَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَعَلَىٰ سَمْعِهِمْ وَعَلَىٰ أَبْصَارِهِمْ غِشَاوَةٌ

**“Ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye hawataamini. Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya ya masikio yao ;na juu ya macho yao pana kifuniko.” (Sura al-Baqarah 2:6-7)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao. *Khatama* maana yake ni kufunga moyo na hakuna maneno yata-kayoingia ndani ya nyoyo zao, bila kujali kama unawafundisha au hapana. Hawataamini, nyoyo zao zimefungwa.

Maana ileile ambayo imetolewa kwa neno *Khatama* huko nyuma limeelezewa na neno *Tab* katika sehemu zingine. Mwenyezi Mungu Mtukufu amezifanya nyoyo zao kuwa *Tab*. Waarabu wanasema kwamba baada ya kuandika barua hupiga muhuri na kufunga barua. Huu muhuri wa mwisho au kufunga barua unajulikana kama *Tab*. *Tab* maana yake ni muhuri umepigwa. Muhuri ni alama ya kukamilika kwa barua. Katika zama za kale muhuri uliwekwa kwenye pete.

Siku hizi riziki, bahati, jaala huwekwa kwenye pete lakini hapo zama za kale muhuri ulikuwa unawekwa kwenye pete. Pia pete zi-meendelea na polepole riziki na bahati ni vitu ambavyo vimewekwa kwenye pete. Baadhi ya watu husema kwamba tangu alipoanza ku-vaa pete hali yake imekuwa ahueni. Wengine husema kwamba tangu alipoanza ku-vaajiwe lile afya yake imeanza kuzorota. Kuzorota kwa afya yako hakusababishwi na pete bali kunasababishwa na koles-teroli, ni kwa sababu ya kile chakula unachokula na si pete unayovaa kwenye kidole chako.

Kwa kweli jiwe linalalamika kwamba hivi lipo kwenye mikono ya nani? Jiwe linasema mtu huyu anataka Riziki kutoka kwake jiwe; kama Mwenyezi Mungu Mtukufu angekuwa amelipatia jiwe hilo sifa hizo basi Mwenyezi Mungu Mtukufu angelilipatia hisia pia. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa hisia hizo mtu huyu (*Sha`uur*) na anaomba vitu kutoka kwenye jiwe hilo, huyu ni mtu mwenye akili za namna gani? Wakati mwingine viumbi vingine humstaajabu binadamu, hata wanyama humstaajabu binadamu.

Maulana Rum ameandika kwamba siku moja mtu fulani alikuwa amepanda kipando cha punda, na baada ya kutembea kwa muda fulani punda alimkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu. Punda alisi-mama na kuanza kufanya minong'ono (*Munajaat*) ya du'a na Mwenyezi Mungu Mtukufu; "Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu mimi nimetosheka na kuumbwa kwangu hivi nilivyo kwamba umeniumba mimi ni punda, mimi sina manung'uniko dhidi Yako kwamba ume-niumba mimi punda. Lakini Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu huyu mtu aliyeketi mgongoni kwangu kuna tofauti gani baina yake na mimi? Mimi ninajihisi vizuri tu kwamba ni punda lakini kuna tofauti gani baina yake na mimi hivyo kwamba yeye anaketi mgongoni kwangu." Kama binadamu anajishusha daraja basi hata wanyama humstaajabu kwamba yeye ni nani?

Jiwe hustaajabu kwamba mtu huyu aliyelivaa ni mtu mwenye akili za namna gani? Nabii Ibrahim ﷺ aliwaona hao waabudu masanamu ambao walikuwa wanayachonga masanamu hayo wao wenyewe. Kwanza walikuwa wanakusanya mawe na miti, halafu waliwapa watu kazi ya kuchonga masanamu hayo, kazi ambayo ilichukua miezi na miaka kuikamilisha. Baada ya kumaliza kazi ya kuchonga masanamu haya, waabudu masanamu hao walikuwa na mazoea ya kuketi mbele ya masanamu hayo wakiwa wamekunja mikono yao na kuomba chochote kutoka kwa masanamu hayo.

Masanamu yalikuwa yanawadhihaki waabudu masanamu hao kwa upumbavu wao kwamba watu hao waliyachonga masanamu hayo kwa mikono yao halafu wanaomba mahitaji yao kutoka kwa masanamu hayo. Hivi inawezekana kwamba mtu anakitengeneza kitu kwa mikono yake halafu anaomba mahitaji yake kutoka kwenye kitu hicho? Ni kama vile mtu anatayarisha mkate kwa mikono yake; halafu anauweka mkate huo mbele yake na kusujudu kwa lengo la kuuomba mkate huo umpe Riziki yake. Mkate utauliza kwamba

mtu huyo ameutayarisha mkate kwa mikono yake halafu tena yeye anaomba Riziki kutoka kwa mkate huo?

Nabii Ibrahim ﷺ pia aliwauliza waabudu masanamu hao kwamba ni upumbavu ulioje waliokuwa wanaufanya; vitu ambavyo wao wamevitengeneza kwa mikono yao ni vitu ambavyo vinawategemea wao; kwa hiyo kama wao walikuwa wanataka kuomba Riziki basi waombe kutoka kwa yule aliyewaumba na si kutoka kwa vitu hivi ambavyo wamevitengeneza wenyewe.

Dunia imekwisha endelea sana, kitu ambacho ni cha kweli kwamba Japan ni Imamu (Kiongozi) katika teknolojia. Ni kweli kwamba Japan imeipatia dunia ubunifu mbalimbali wa kiteknolijia. Lakini wao hufanya nini? Baada ya kuchoka ambapo amaketi mbele ya kompyuta na kuendeleza teknolojia ya NANO, Wajapani huzulu hekalu na kusujudu mbele ya jiwe. Ingekuwa ni bora zaidi kama angesujudu mbele ya kompyuta, angalau hiki kilikuwa kitu changamani. Pale ambapo binadamu hushuka daraja huenda kwenye upeo wa daraja la fedheha zaidi. Ndama wa Saamri alitengenezwa na Saamri mbele ya Mungu na watu walitakiwa kuabudu sanamu hilo. Huku ndiyo kufedheheka kwa binadamu kwamba wote walitengeneza sanamu ya ndama kwa mikono yao na halafu wakaanza kuabudu sanamu hilo.

Waarabu wa zama za kale walipomaliza kuandika barua waliikuwa na mazoea ya kufunga barua kwa kupiga muhuri juu ya barua, na muhuri kwa kawaida ulikuwa unachongwa kwenye pete ya jiwe. Zipo falsafa kadhaa za kucaa pete. Katika dini ni Mustahab kucaa pete; imependekezwa kwa sababu mbalimbali kama vile ingeweza kuwa alama ya mu`min. Katika zama za Bani Umayyah na Bani Abbas ilikuwa vigumu sana kuwatambua waumini, kwa hiyo pete hii ikawa ndio kitambulisho. Hata leo hii waumini wanatambuana wao kwa wao kwa pete. Ilikuwa hivyo katika zama hizo. Au sababu

nyingine ni urembo kwa mwanamume kama vito vilivyo urembo kwa mwanamke.

Ili kuweza kumlinda mwanamume asivae dhahabu, hii ingekuwa Mustahab kwa kuwa dhahabu imeharamishwa kwa mwanamume. Kitu chochote kilichotengenezwa kwa dhahabu kama vile pete, kibwete kidogo, utepe au saa vyote hivi ni haramu kwa mwanamume. Vipo vitu fulani ambavyo ni vizuri lakini vilikwishakuwa chini ya jina la mtu mwininge, kama vile dhahabu imehusishwa na wanawake. Mwalimu wetu alikuwa akisema kwamba chipsi hizi ni tamu lakini kwa bahati mbaya zimehusishwa na jina la watoto. Falsafa hii ya kucaa pete ama ni kwa ajili ya urembo au utambulisho lakini kwa vyovyote vile hakuna Riziki kwenye mawe hayo. Mawe hayo hayana uhusiano wowote na nyota yoyote, Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuumba nyota kwa ajili ya riziki ya binadamu, wapo malaika kwa ajili ya Riziki. Mwenyezi Mungu Mtukufu hukukabidhi hatamu ya binadamu mikononi mwa nyota badala yake amekabidhi hatamu hiyo mikononi mwa Maimamu .

Katika zama za kale mihuri ilitengenezwa kwenye pete na walikuwa wakipiga muhuri hiyo mwishoni mwa barua. Muhuri kwa Kiarabu unajulikana kama *Khatam*. Kwa kuwa kupiga muhuri mwishoni mwa barua hiyo ilikuwa ni ishara kwamba barua ilikuwa imekamilika; pete pia ikaitwa *Khatam*. Khatam maana yake ni pete yenye muhuri. *Tab* maana yake ni kwamba unapomaliza kuandika yaliyomo ndani ya barua unaweka saini kama ishara ya kukamilika kwa barua leo hii, lakini hapo zama za kale muhuri ulipigwa mwishoni mwa barua. Kupiga muhuri kulionesha kwamba hapo ndipo ulikuwa mwisho wa barua na hakuna kinachoandikwa baada ya hapo. Hii inajulikana kama *Tab* ambayo maana yake ni tangazo la kukamilika.

### **“Tabiyat” ya viumbe vyote:**

Viumbe hai vyote ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliviumba na mionganii mwao upo mwili wa binadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka vitu vyote vya lazima katika miili ya viumbe hai ikiwa ni pamoja na mwili wa binadamu ambamo mahitaji yote ya kimwili yaliwekwa ndani ya binadamu, na halafu tangazo la ukamilishaji lilifanywa. Baada ya tangazo jina la uumbaji huu likawa *Tab-e-Bashar* ambalo maana yake ni: huyu ni binadamu aliyekamilika kimaumbile. Uumbaji wake wa kimaumbile umekamilika na hapatakuwepo na nyongeza zaidi ya hapa. Kwa hiyo chochote kilichowekwa ndani ya uwepo wa umbile la kimwili la binadamu ambacho kilimkamilisha binadamu, uwepo huu wa kimaumbile na uhalisia wa binadamu unajulikana kama Tabiyat. Hii inaitwa Tabiyat kwa sababu mahitaji yote yalitimizwa na kukamilishwa.

Tabiyat ipo katika kila kiumbe na maana yake ni kwamba kila kiumbe kimeumbwa katika hali iliyokamilika. Lakini tabia na sifa maalum zinatofautiana. Kama vile tabia ya moshi ni kwamba wakati wowote unapokokwa moto moshi huenda juu, lakini kama ukitupa kipande cha jiwe juu kitaanguka chini. Vivyo hivyo kama ukimwaga maji kwenye ardhi yatatiririka kufuata mteremko. Maji haya yame-pata wapi ujuzi wa kutiririka kufuata mfereji; moshi unajuaje kwamba unatakiwa kuelekea kwenda juu? Jibu ni kwamba katika Tabiyat ya Maji maana yake ni kwamba wakati maji yanaumbwa tabia hii iliwekwa ndani ya maji, kwamba wakati wowote yakimwagika, yanapaswa kuelekea kwenye mfereji. Kila kitu kina tabia tofauti na hivyo mwenendo tofauti pia. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka ndani ya kila Tabiyat kitu ambacho Tabiyat inatakiwa kufanya.

Hivyo Qur’ani Tukufu pia inasema kwamba tumeumba kila kitu na tukakiweka katika mkondo wake. Jua liliumbwaa likawekwa kwenye njia yake. Mwezi uliumbwaa ukawekwa kwenye njia yake na

kwa sasa viumbe hivi vinapaswa kuwa katika njia zao. Viumbe hivi vina Tabiyat tu, na Tabiyat haitegemei kujuzwa au kufundishwa. Kama vile maji ambavyo haya fundishwi yaelekee upande gani yanapomwagika, na moshi nao haufundishwi unapaswa kuelekea upande gani. Udongo haufundishwi unapaswa kufanya nini; mvua haifundishwi jinsi ya kunyesha. Kitu chochote cha kimaumbile ndicho tu ambacho hakihitaji kuambiwa kielekee wapi, kwa sababu tabia hizi ziliwekwa ndani ya kitu hicho wakati wa kuumbwa kwake na baada ya kuweka tabia hizi ndani ya kiumbe hicho uumbaji wake ulikamilika na Khatm yake ilifanyika, na kwa sababu ya hii Khatm, Tab yake ikawepo. Sasa, Mwenyezi Mungu Mutkufu amekiumba kitu hiki na Tabiyat iliyokamilika.

Kila kitu cha kimaumbile kinayo Tabiyat ndani mwake. Mti ni kitu chenye umbo, unayo Tabiyat. Wanyama wanayo maumbile kwa hiyo nao pia wanayo Tabiyat. Maji yana umbo kwa hiyo yanayo Tabiyat. Vitu vyote vya kimaumbile vina miili na maana yake ni kwamba sifa zao maalum zimebekwa ndani mwao na uumbaji wao umekamilika. Vivyo hivyo binadamu naye anayo Tabiyat. Na tauliza pia kwamba Tabiyat yako ikoje na maana yake ni kwamba mahitaji na sifa maalum za mwili wako zikoje.

### **Tabiyat ni kitu kilichopo baina ya Binadamu na Wanyama:**

Fitra inatofautiana na Tabiyat. Upo mgongano na mapambano baina ya Fitra na Tabiyat. Vitu ambavyo vimewekwa ndani ya mwili wa binadamu ni Tabiyat na Tabiyat hii inataka kuitawala na kuitiisha Fitra na kuitumia kwa malengo yake yenye. Kwa upande mwingine Fitra inataka kuitiisha Tabiyat. Katika vita hii ya ndani, yeoyote anayeshinda vita hivi akisi ya tabia yake huonekana nje kufuatana na Fitra yake, lakini yule ambaye Fitra hushindwa na kukandamizwa basi tabia yake ya nje itaendana na Tabiyat yake.

Tabiyat ya binadamu na ile ya wanyama inafanana; hakuna tofauti kubwa baina ya Tabiyat ya Binadamu na ile ya Wanyama. Hii ndio sababu Madaktari wa Sayansi ya Tiba hutumia miili ya wanyama ili waweze kujizoeza na mfumo wa kimaumbile wa mwili wa binadamu. Mtu anatakiwa awaulize hawa Madakitari wa Sayansi ya Tiba kwamba inakuwaje wao huwa wanawatibu binadamu lakini hufanaya majoribio kwenye miili ya wanyama. Wanasyansi hawa wa Tiba huanza na vyura, halafu panya, halafu paka na majoribio ya mwisho hufanywa kwenye maiti ya binadamu. Yale mambo am-bayo wamejifunza kutoka kwenye miili ya wanyama kabla na sasa wanatazama ndani ya binadamu wanaona hakuna tofauti kubwa. Hii ni kwa sababu Tabiyat za viumbe hivi zinafanana, kwa hiyo wanafanaya kitu sahihi, vinginevyo wangeanza kumkatakata binadamu tangu mwanzo wa mafunzo yao.

Hata dawa wanazotengeneza kwanza hufanya majoribio kwa panya, nyani na wanyama wengine. Kwanza wanampa mnyama chanjo ya kifafa halafu wanampiga sindano mnyama yenyе virusi vya kifafa kuona kama chanjo itafanyakazi au hapana. Kama ikifanyakazi basi wao huhitimisha kwamba dawa hiyo itafanya kazi kwa binadamu pia.

Hata huandika kwamba mwanasyansi huyu amegundua tiba ya saratani baada ya kufanya majoribio ya dawa hiyo kwa mwili wa panya na saratani yake ikatibika. Wakati wowote dawa fulani inapoonekana inafaa kwa mnyama pia hufaa kwa binadamu. Kwa nini iwe hivi? Hii ni kwa sababu sehemu hii ya binadamu na wanyama inafanana. Hii ni upande wa kimaumbile wa binadamu ambao uumbaji wake, mahitaji na maradhi pia yapo kwa wanyama. Sehemu hii ya uumbaji haina heshima na upendeleo kwa binadamu. Kitu kinachompa upendeleo binadamu ni Fitra yake, na hii ndio sababu Mweenyezi Mungu Mtukufu hakufanya majoribio ya dini kwa wanyama.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwasilisha dini kwa binadamu pekee kupitia kwa wawakilishi Wake.

### **Mgongano wa Fitra na Tabiyat na matokeo yake:**

Katika mapambano haya ya Fitra na Tabiyat, kama Fitra ikishindwa (haifi) na kutiishwa basi tabia za mtu huyo hugeuka kuwa za kihayawani na hutawala. Mtu huyo huanza kuishi maisha ya kunywa, kula, kusema, kuketi, kusimama, na hufanya kila kitu kama wanyama. Kama vile ambavyo wanyama ambaao huzaliwa pamoja kama kaka na dada lakini baada ya muda fulani husahau uhusiano huu, lakini Fitra tangu kuzaliwa hadi kifo haiwezi kumsahau kaka yake na dada yake. Wazazi wa wanyama huwasahau watoto wao wakisha kuwa wakubwa lakini Fitra haisahau. Fitra huwakumbuka wazazi hadi kwenye umri wa uzee na hata baada ya kifo.

Fitra hukumbuka masomo yote lakini masharti ni kwamba haitakiwi ishindwe na isije ikadhoofishwa na vumbi la Tabiyat. Fitra hukumbuka yote kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni nani, Mtukufu Mtume  ni nani na dhuria wake ni nani. Lakini Fitra inapohinikizwa na Tabiyat binadamu hugeuka kuwa hayawani. Na hayawani hajali mama, dada, dini, Mtukufu Mtume  na hata dhuria wake. Ndiyo sababu inasemekana kwamba mapambano ya Karbala yalikuwa ni vita baina ya Tabiyat na Fitra.

Upande mmoja walikuwepo watu ambaao walikuwa nayo Fitra ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaao walikuwa wanafahamu kila kitu, ambapo upande mwingine walikuwepo watu hayawani. Kama Tabiyat ya binadamu ikigeuka na kuwa ya kihayawani mtu hugeuka na kuwa ya hayawani zaidi. Udhalimu na ukandamizaji uliofanywa ulivuka upeo wa kuzungumzika. Kwa kuwa tumekuwa watu we-

nye nyoyo ngumu tunapaswa kusikiliza sana kuhusu majanga, kulia vinginevyo jina la Husein linatosha kuliliwa.

### **Binadamu – Kiumbe Asiyetambulika:**

Binadamu ambaye ndiye kiini cha uumbaji wote amefanya matendo mabaya kiasi kwamba hayawani wamehisi aibu, ambapo kwa upande mwingine amefanya matendo adhimu sana hivyo kwamba hata Malaika wamejawa na shauku. Binadamu anahitaji kujigundua hapo ndipo tu binadamu atawenza kuelewa dini.

Mwenyezi Mungu Mtukufu katika maneno yake matakatifu ambamo ametoa ilani ya mwongozo wa binadamu, ambayo ni Qur`ani Tukufu iliyo na sehemu kubwa inayohusu kumwelewa binadamu, kumtambua na kumwendeleza binadamu. Sura ya kwanza ya mafundisho ya Qur`ani Tukufu ni kumtambua binadamu ili aweze kuelewa na kuona njia ya kuelekea kwa Mola Wake. Lakini binadamu huyu ni changamani katika uumbwaji wake. Kila sehemu ya uumbwaji wake ni changamani na kila sehemu inastahili utambuzi wake mahsusii.

Kitabu kimoja chenye manufaa sana kimeandikwa na msomi mmoja Mfaransa, Alexis Carrelaambacho kinaitwa “*Binadamu, Kiumbe Asiyefahamika*.” Mtu huyu ni Daktari wa Tiba na yeye anahusika na mwili wa binadamu tu. Katika uchambuzi wake wa mwili wa binadamu amefika kwenye hitimisho kwamba uhalisia wa binadamu bado haujajulikana kwa binadamu mwenyewe. Uchambuzi na uchunguzi wa mwili wa binadamu haukuanza leo, kwani umekuwa chini ya uchunguzi tangu mwanzo wa kuumbwa kwake. Binadamu ametafiti sana kuhusu mwili wa binadamu, na kila siku utafiti huo huongezeka. Viungo vya binadamu, uumbwaji wake, umbo lake, mfumo wa mwili huonesha kitu kipyka kila siku.

Msomi huyu ametumia maisha yake katika kuchunguza mwili wa binadamu. Anazo rejea za vitabu vyote vya wasomi wote wa kabela yake, baada ya kumchunguza binadamu kivitendo ndani ya maabara aliandika kitabu “*Binadamu, Kiumbe Asiyefahamika*” na maana yake ni kwamba hadi leo hii binadamu bado hajajulikana kwa binadamu mwenyewe. Hii inaweza kushuhudiwa tu pale ambapo binadamu atawenza kujitafakari yeze mwenyewe kwa kiasi fulani kuhusu uumbwaji wake.

Binadamu bado hajagunduliwa kwa ajili ya binadamu, bado hajagundulika hata kwa upande wake wa kimwili. Chukua kiungo chochote cha binadamu na utaona dunia ya maajabu ndani ya kiungo hicho. Kama ukichukua jicho la binadamu na utazame tu ile namna ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameliumba jicho hili; ni dunia ya maajabu. Kama hatutaelewa kitu kingine chochote kuhusu binadamu natuelewe tu kazi ya kiungo hiki kimoja cha binadamu ambacho ni jicho; Mwenyezi Mungu Mtukufu ni shahidi, kwamba hutanyanya kichwa chako kutoka kwenye sijida.

Jicho hilihili ambalo sisi hulitumia kutenda dhambi, tunakuwa watovu wa adabu, ambalo tunalitumia bila uangalifu wowote na ambalo hatulipatii haki zake. Hii ni Tabiyat ya binadamu ambayo ipo kwa Binadamu na viumbe vingine pia. Kitu cha thamani ambacho kilimpa binadamu upendeleo kilikuwa ni roho yake na Fitra yake, ni sifa bainifu na uwezo wa roho. Fitra ni mtindo maalumu wa uumbaji. Sifa bainifu na uwezo wa roho ndio huitwa Fitra ambapo sifa bainifu na uwezo wa mwili ndio huitwa Tabiyat. Kusudio la maisha yetu ni kutimiza mahitaji ya Fitra ambapo bado hata hatujatambua Tabiyat ya binadamu. Tunahitaji kuilea Fitra yetu lakini kwanza tunahitaji kuitambua yenye.

### **Ghariza (Silika za kimaumbile):**

Kipo kitu kingine cha tatu ambacho Mwenyezi Mungu Mtukufu amekiweka ndani ya binadamu mbali na Tabiyat na Fitra. Kitu hiki ni Ghariza. Pamoja na kwamba kitu hiki kinahusiana kwa karibu sana na Tabiyat lakini kimetengwa. Uwepo wake na kazi zake zimetengwa. Ghariza ni kwa ajili ya vile viumbehai tu vyenye mwendo (wanyama na binadamu). Tabiyat ni kwa ajili ya kila kitu chenye uwepo wa kimaumbile. Maji, moto, mawe, majabali, hewa, oksijeni, haidrojeni na kila kitu chenye uwepo wa kimaumbile kinayo Tabiyat. Tabia na sifa zote bainishi kwa ajili ya uumbaji huu ziliwekwa ndani, zikiwa zimekamilika na kufungiwa. Hii ni Tabiyat ambayo imetajwa kabla kwamba maana yake halisi ni kufunga na kupiga muhuri.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alitengeneza uwepo wa kila kitu, aliweka sifa bainifu ndani yake, akafunga na halafu alipopiga muhuri juu yake; kitu hicho kilipewa jina la Tabiyat. Chochote kilichohitajiwa na maji kiliwekwa ndani mwake na kikawa ndio Tabiyat yake. Chochote kilichohitajiwa na hewa kiliwekwa ndani yake kwa ukamilifu na hakuna hata molekuli moja ambayo ilibaki kwa ajili yake. Tabiyat yake ikakamilika. Kama ukitoa maana ya kimsamiati ya kujitegemea ya Tabiyat basi inaweza kurejelewa kama uwepo kamili wa kimaumbile wa vitu vyote vyenye maumbile.

Kila sifa bainifu ya mtu mmoja ni tofauti na ya mtu mwingine. Kama vile ambavyo watu wawili hawafanani, vivyo hivyo katika ulimwengu huu hakuna vitu viwili vinavyofanana. Kwa sababu kama vikifanana basi vitu hivyo haviwezi kuwa vitu viwili. Tofauti inahitajika kwa ajili ya kuongezeka kwa viumbe. Ni hapo tu ambapo inakuwepo tofauti ndipo uwezekano wa kuongezeka utakuwepo. Tabiyat ya kila kiumbe imeumbwa hivyo.

Viumbe fulani vimeumbwa kwa namna ambayo kwamba mbali ya kuwa na umbile pia vina uhai, vinakua kama vile mimea na vipo viumbe vingine ambavyo huzaliana pia na huzaa spishi ya aina kama wao. Viumbe hivi huitwa Wanyama au hayawani. Katika wanyama hawa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka kitu cha tatu pia amba-cho tutakitaja kwa kutumia mfano.

Sisi sote tunayo mazoea na Kompyuta. Katika Kompyuta zipo sehemu kuu mbili; sehemu moja ni Vifaa vya mitambo ya kompyuta na sehemu ya pili ni Programu za kompyuta. Vifaa vya mitambo ya kompyuta ni vijenzi vyenye maumbile ambavyo vimeunganishwa pamoja na kujenga kompyuta. Progaramu za kompyuta ni programu nyingi zinazotumika kuendesha mashine hii. Katika Progamu za kompyuta pia zipo aina mbili za program; aina moja ni zile programu na programu za kompyuta ambazo zinaweza kusimikwa kwenye vifaa vya mitambo ya kompyuta kama vile mfumo wa uendeshaji na matumizi mengine. Unaweza kusimika madirisha, vista au MAC au kokwa ndani ya kompyuta. Halafu unaweza kuongeza vitu vingine ambavyo vitafaa katika matumizi yako. Ipo programu nyininge ambayo ipo ndani ya kompyuta kwa kosa la kupuuza ndani ya kompyuta mara tu unaponunua kutoka dukani. Hii inajulikana kama (*Basi Input/Output system*) Mfumo msingi wa kuingizia na kutolea, maunzilaini hii ambayo imo ndani ya kompyuta huamua kile ambacho kompyuta inaweza kufanya bila ya kutumia program kutoka kwenye disk ya kurekodia taarifa ndani ya kompyuta. Kwenye kompyuta binafsi, mfumo msingi wa kuingizia na kutolea una alama zote za siri zinazotakiwa kudhibiti bodidota ya kompyuta, skrini, kifaa cha kuhifadhi data, (*disk drives*) mawasiliano ya mfululizo (*serial communications*) na kazi zingine tofauti tofauti. Mfumo msingi wa kuingizia na kutolea (BIOS) upo ndani ya kumbukizi fikia nasibu (*ROM*) ya kitengo kikuu cha uchakataji (*CPU*). Hiki ni kitu amba-

cho huwezi kuweka kitu kingine badala yake au kufanya kukibadili kabisa. Kitu hiki kimesimikwa na mzalishaji kiwandani wakati wa kutengeneza vifaa vya mitambo ya kompyuta yenewe. Ni kitu kama hiki ambacho hata simu za mkononi zinacho, kwamba kinakuja na mfumo wa uendeshaji ambao huwezi kuubadili. Kama vile yapo madirisha ya simu, simu Symbian, simu Android, Apple IOS. Haya majukwaa ya OS hayawezi kubadilishwa na unaweza kusimika programu zako zingine zijulikanazo kama Maunzilaini tumizi (APPS) katika teknolojia ya simu (*Mobile Technology*). Kama hiki kifaa cha kuandikia maneno (OS) hakipo kwenye simu wala simu hiyo haitawaka. Katika jinsi ya kipaji, kifaa cha kuandikia maneno (OS) kimewekwa ndani ya kumbukizi fikio nasibu (ROM) ya simu. Huu mfumo msingi wa kuingizia na kutolea (BIOS) uliopo ndani ya kompyuta na kifaa cha kuandikia maneno (OS) kilichopo ndani ya simu ya mkononi, huendesha kila kijenzi cha mitambo ya simu ndani ya vifaa hivi.

Kitu chochote ambacho binadamu amekiunda hajafanya hivyo bila kuwa na mfano kwanza. Pamoja na kwamba tunasema kwamba vitu viwili vimefanywa katika sayansi; moja ni ugunduzi na pili ni uvumbuzi. Pamoja na kwamba katika hali halisi binadamu hajavumba kitu kwa sababu kuvumba sio kazi ya binadamu juu ya kitu chochote. Wajibu wa binadamu ni kugundua tu; binadamu hawezি kuvumba kitu kwani yeye anao uwezo wa kugundua tu. Binadamu amegundua kila kitu kama vile sheria, kanuni, fomyula, uhalisia na haya ni mafanikio makubwa ambayo yamefikiwa na binadamu hivyo kwamba amegundua hadi kwenye kiwango cha chembe ndogo na uhalisia na siri ndani ya binadamu. Wajibu wa akili ni kugundua siri katika chembe ndogo katika ulimwengu wote. Binadamu hajatengeneza kitu chochote bila ya mfano kwanza. Katika mfano wa kompyuta na simu ya mkononi ambao

nimetoa, pia hii inatia msukumo ambao binadamu amechukua kutoka kwa wanyama.

Silika zilizopo ndani ya wanyama ni kwa ajili ya kuendeleza uwepo wao. Wanyama wanahitaji utambuzi wa vitu kwa ajili ya uwepo wao, lakini utambuzi huu haufanyiwi kazi ya kuupata bali upo ndani ya wanyama kimaumbile. Kama ukifanya uchambuzi wa dunia ya wanyama, ipo elimu ya kustaajabisha na ni dunia ya kushangaza. Kama ukitafakari tu kipengele hiki cha jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyoweka utambuzi huu wa wanyama kimaumbile na wanavyozaliwa nao. Ni jinsi gani wakati wanapozaliwa tu huweza kuona njia yao ya kwenda kwenye malezi. Mnyama anapozaliwa ile siku ya kwanza ya kuzaliwa kwake, fanya tafakuri juu ya hili. Kama vile unapotaka tunda usifanye haraka kuanza kula tunda na mboga, kwanza tafakari na soma pia. Angalia uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu uliopo ndani ya tunda na mboga hizo. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka vitu viwili ndani ya matunda; kitu kimoja ni kwa ajili ya tumbo na kitu kingine ni kwa ajili ya akili (Aql) pia. Mnyama hufanya haraka kula chochote kilichopo mbele yake, lakini binadamu anatakiwa kutafakari kwanza kabla ya kuanza kula kile kilichopo mbele yake. Kama vile, vitu hivi vimetoka wapi hadi vikafika kwenye akili ya binadamu na akaweza kuendeleza kisahani (*disc*) ambacho anaweza kukiweka ndani ya kompyuta na kufanya kila kitu kifanye kazi?

Kitu hiki (BIOS) mfumo msingi wa kuingizia na kutolea na program, binadamu amekichukua kutoka kwa wanyama. Wakati mnyama anapozaliwa angalia jinsi mnyama huyu mchanga anavyoenenda. Kama umemuona mbuzi, ng'ombe na kondoo anapozaa, mtoto mchanga wa mnyama anapozaliwa miguu yake yote huwa imekabwa na kazi ya kwanza ni kuinyoosha miguu yake. Baada ya kunyoosha miguu yake, basi mama wa kichanga hicho (mbuzi)

pia hujua kwamba mtoto amezaliwa. Katika kipindi hiki mama wa kichanga huwa anahisi maumivu makali sana kwa sababu maumivu ya uzazi kwa kawaida huwa makali sana kwa wanawake, binadamu na wanyama pia. Baada ya mbuzi kuzaa mtoto wake huwa kwenye maumivu makali sana ambayo huwa bado hayajatulia, kwa hiyo badala ya kushughulikia maumivu ya tumbo lake au kuanza kula majani hugeuka na kwenda kwa mtoto wake na kuanza kulamba mwili wa kichanga chake hicho. Kwa nini mbuzi mzazi analamba mwili wa mwanae? Sio kwamba mwili huo ni mtamu na una ladha tamu. Mbuzi huyu anajua kwamba anapaswa kufanya hivyo kwa sababu miguu ya mtoto wake ilikuwa imekunjika ndani ya tumbo lake kwa kipindi cha miezi kadhaa na hivyo huo ni wakati ambapo miguu ya mwanawe inatakiwa ipate nguvu ya kumfanya awe huru ili aweze kusimama kwa miguu yake mwenyewe. Mtoto hujaribu kunyoosha miguu yake na msaada mwingine hupata kutoka kwa mama yake. Hii kazi ya kulamba mwili wa mtoto ni ujumbe ambao mbuzi humpa mwanae ili kwamba mzunguko wa damu upate nguvu na miguu hunyooka. Mbuzi mzazi anajua kwamba hiyo ni kazi yake ambayo anapaswa kuifanya na huanza kufanya kazi hiyo ya kutoa ujumbe haraka kwa mtoto wake. Katika kipindi cha chini ya dakika thelethini (30) mtoto huanza kusimama na baada ya kuanguka mara kadhaa mtoto husimama kwa miguu yake mwenyewe.

Halafu kitu cha kwanza ambacho mtoto hufanya ni kutafuta chakula. Mtoto alipokuwa ndani ya tumbo la mama yake alikuwa hana kazi ya kutafuta chakula kwa sababu alikuwa anapata chakula kwa njia ya mfumo wa kujiendesha wenyewe kupitia bomba lililounganishwa. Lakini sasa huyu mtoto wa mbuzi anajua kwamba kipindi cha kupata chakula bila kukihangaikia umekwisha na kwa hiyo mtoto wa mbuzi huanza kuhangaika ili apate chakula. Vitu vingi viro; majani, wanyama wengine wapo lakini haendi huko, yeye huenda kwa mama yake

tu. Mtoto hutazama mwili wote wa mama yake na hujua sehemu ipi ya mwili wa mama yake chakula chake kinapatikana na baada ya dakika chache za jitihada huona chakula chake.

Suala ni kwamba mtoto huyu wa hayawani ambaye amezaliwa punde tu, hakufundishwa na yejote, hajaona mfano wowote kabla ya hapo, hakupata mafundisho yoyote darasani na mara tu alipozaliwa, amejua kwamba anapaswa kunyoosha miguu yake na halafu anajua kwamba anapaswa kutafuta chakula na pia anajua mahali chakula chake kilipo. Yeye amezaliwa leo, hajaona kitu chochote, hajafanya Taqliid yoyote.

Chukua mfano mwingine wa kasa, wanyama wenyewe maisha marefu kuzidi wengine wote kwani wao huishi kwa mamia ya mka. Mnyama huyu huishi baharini na kwa ajili ya lengo la kuzaliana kasa jike huenda ufukweni kwa kusafiri maelfu ya maili. Huenda mwendo mrefu kutoka baharini hadi ufukweni na huchimba mashimo ambamo hutaga mayai yao. Kasa jike anajua ni sehemu gani ya ufukwe yenye mchanga mwingi na kisha anaiona sehemu hiyo kama vile anatumia dira iliyokongomewa ndani mwake. Kasa jike huchimba mashimo kwenye mchanga kwa jitihada kubwa na halafu anataga mamia ya mayai ndani ya mashimo hayo. Baada ya kutaga mayai hufanya mpango wa ulinzi wa mayai hayo. Hufukia mashimo hayo na uelewe kwamba ili yai liweze kutotoa mtoto linahitaji kiwango fulani mahsusini cha joto. Katika kipindi kifupi anapaswa kutaga mayai na kufukia mashimo yenye mayai na kiasi cha mchanga ni kile ambacho kitadumisha kiwango mahsusini cha joto.

Baada ya kufanya yote haya, kasa jike hurudi baharini. Halafu baada ya miezi kadhaa mayai hutotoa watoto na watoto wa kasa hutoka nje. Hutotolewa watoto wa kasa mamia kwa maelfu kwa siku moja na hutoka nje kutoka kwenye kina cha shimo la futi moja lililofukiwa mchanga. Hawa watoto wa kasa hutoka nje na wanahi-

taji waende mahali. Upande mmoja ipo nchi kavu upande mwininge kuna bahari. Lakini maelfu ya watoto hawa wa kasa huelekea upande wa baharini tu. Hapajatekea hata mara moja mtoto wa kasa aelekee nchi kavu. Anaporudi baharini mtoto wa kasa katika siku yake ya kwanza anawajua maadui zake pia bila kuwepo mama yake. Anajua ni sehemu zipi za bahari zenye hatari kwake na huzikwepa. Mtoto wa kasa anajua anapaswa kwenda kwenye kina cha kiasi gani polepole na anajua anapaswa afanye nini.

Ni dunia ya maajabu ya kwamba utambuzi huu umetoka wapi na kuingia kwa myama huyu. Na hii ni kawaida ambayo imekuwa ikiendelea kwa mamilioni ya miaka. Kasa ni viumbe ambao walikuwepo wakati wa dinosaria. Wale wanyama wenye umbile kubwa ambao walikuwepo hapo kale na ambao masalia yao yanagunduliwa leo hii, Na miili yao mikubwa iliyeyuka na leo hii petroli ambayo inachimbwa ni mafuta yatokanayo na mafuta ya wanyama hawa ambao walifukiwa chini ya ardhi. Kwa hiyo ni nani amewaambia mama zao kwanza kusafiri safari ndefu na kufika ufukweni na halafu nani amewaonesha watoto wa kasa njia ya kwenda baharini. Kasa anaiishi maisha ya aina hiyo na anafuata mpangilio huo wa maisha kwa mamilioni ya miaka na mpangilio huo utabakia hivyo hata kwa mamilioni ya miaka mingine.

Vivyo hivyo dunia ya nyuki wa asali pia inastaajabisha. Jinsi nyuki anavyojenga masega ya asali ni kazi bora sana ya uinjinia na hakuna tofauti na jinsi alivyojenga masega hayo maelfu ya miaka iliyopita na sasa. Ukitazama dunia ya mchwa; viumbe hawa huishi katika makundi na hujenga nyumba zao katika makundi. Wale ambao wamefanya uchunguzi wa dunia ya wanyama, husema kwamba maisha yao yana sifa bainishi kama za binadamu.

Inafaa kutamka hapa kwamba wanyama ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaumba wanazo sifa bainishi za kimaumbile kama

zile za binadamu. Kama kila moja ya sifa bainifu mbalimbali za binadamu ikipewa picha ya kimaumbile inakuwa aina fulani ya mnyama. Kila mnyama ni sanamu ya kimaumbile ya baadhi ya sifa bainishi za binadamu. Hatuwezi kuchora picha ya sifa bainishi. Kama vile unataka kuchora picha ya wivu basi haiwezekani hata msanii bora sana kuchora picha hiyo. Hii ni kwa sababu wivu sio kiumbe cha kuonekana. Mchoraji anaweza tu kuchora picha za vitu vya kimaumbile lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweza kutengeneza picha hiyo na hata ameumba mfano wa kimaumbile wa kitu hicho.

Kama vile ambavyo unataka kumwambia mtu achore picha ya wizi wa kutumia nguvu na sio mwizi mwenyewe. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alichora picha na umbo linalotembea la mwizi pia. Vivyo hivyo ubakhili na uchoyo hauwezi kuchorwa katika picha. Mtu bakhli ni yule ambaye hapendi kutumia na vipo viwango, wapo watu ambao hawapendi kutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambapo baadhi ya watu bakhili hawataki kutumia hata kwa ajili ya wao wenyewe.

Kama ukitaka kuchora picha ya ubakhili basi huyo ni Mchwa. Mchwa hukusanya chakula katika maisha yake yote lakini hali chakula hicho, yeye hulimbikiza tu. Kama mchwa akila kile chakula chote anachokusanya basi ataongezeka umbo na kuwa mkubwa kuhliko tembo. Mchwa hukusanya chakula kwa miezi tisa na halafu kwa miezi mitatu huitumia katika kulinda kile alichokusanya. Angalia akili iliyofichama ya mchwa; hukusanya punje za ngano na anajua kwamba mbegu za ngano zikifukiwa ardhini zitamamanuka katika msimu maalum. Punje hii ambayo imehifadhiwa kwenye ghala la mchwa ambalo lipo chini ya ardhi itapasuka na kuota na kwa hiyo itaharibu nyumba ya mchwa pia.

Huyu mchwa kibarua hukusanya punje na huzikabidhi kwa mchwa mtunza ghala. Huyu mchwa mtunza ghala huipasua punje

katika vipande viwili kwa sababu mbegu iliyopasuliwa vipande viwili haiwezi kuota. Sasa nani amemwambia mchwa kwamba mbegu huota ikiwa chini ya ardhi, na nani amewaambia mchwa namna ya kuilinda? Ungeona upande mwingine wa kushangaza wa mchwa wanapokata jani la mti katika vipande. Sasa hatuna muda wa kutafakari juu ya mchwa kwa kuwa sisi wenyewe hatuna hata muda wa kujitafakari. Tunapaswa kutafakari juu ya vitu hivi, ambavyo ni vitabu vilivyojaa masomo.

Kama ukitaka kuupatia wizi umbo basi umbile lake ni panya. Mtu mmoja alimwendea Imam Sadiq عليه السلام na alimwomba amtafsirie ndoto yake ambamo amemuona panya kitandani mwake. Imam Sadiq عليه السلام alimjibu mtu huyo kwamba mke wake ni mwizi. Picha ambazo sisi huziona kwenye ndoto zetu ni picha za vitu vingine, ambapo uhalisia wake ni tofauti na picha hizo.

Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoumba Tabiyat ya binadamu aliweka kisahani (ROM=kumbukizi fikio nasi-bu) ndani ya binadamu. Ndani ya kisahani hiki Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka mahitaji yake yote na halafu akapiga mhuri uumbaji wake, akakamilisha Tabiyat yake na akampeleka binadamu katika dunia hii. Sasa binadamu anapokuja katika dunia hii, kile kisahani kinaanza kufanya kazi na humpa binadamu ujumbe kuhusu yale anayopaswa kufanya wakati huo na baadaye.

Sifa zote hizi ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka ndani ya Tabiyat yake zinaitwa Ghariza. Ghariza maana yake ni utambuzi na mwongozo mahsus ambao binadamu huzaliwa nao katika uwepo wake. Hali maalumu ambayo imewekwa ndani ya mnyama ni Ghariza. Hali hii ni maalumu kwa wanyama wenye uhai. Mawe, miti, milima inayo Tabiyat tu sio Ghariza. Hii ni kwa sababu miti haina mwendo, haihitaji kubadilisha mahali ilipo, yenyewe hukua tu. Lakini upo uwepo mahsus kwa wanyama am-

bao umekabidhiwa kwao na kwa sababu hiyo wanyama wanapaswa kutembea. Mnyama anapaswa kufanya vitendo fulani, amepewa miguu. Uwepo wake unahitaji mwongozo na hali hii imewekwa ndani mwake.

Kwa nini hali hii inaitwa Ghariza? Neno Ghariza asili yake ni neno *Gharz*. Kwanza tunahitaji kuelewa maana ya neno Gharz ambalo maana yake ni kupanda kitu. Katika kupanda mbegu hutumika neno Harz. Lakini kwa mimea mingine haina haja kupanda mbegu lakini hupandwa mche mdogo. Katika kupanda mche mdogo Waarabu hutumia neno Gharz. Kitu chochote ambacho hufukiwa chini ya ardhi kinayo sifa bainishi kwamba baada ya kupandwa ndani ya ardhi hutandaza mizizi yake humo. Mizizi hutandaa kwa sababu mmea unajua kwamba watu wengine wanaweza kuja kutaka kuung'oa mmea huo. Mmea unajua kwamba unapaswa kujiimarisha ndani ya ardhi ili usije ukang'olewa.

Wakati kitu kinapopandwa ndani ya ardhi na kutandaza mizizi yake humo kwa kiasi kwamba hakiwezi kung'olewa kwa urahisi, hii inajulikana kwa neno Ghariza. Ghariza maana yake ni kwamba kitu kikiwa kimechimbiwa kwa namna ambayo hakiwezi kung'olewa na kama kiking'olewa basi kitatoka pamoja na udongo. Ghariza maana yake ni sifa bainifu ambayo ilipandwa katika kina kirefu sana ndani ya uwepo wa binadmu na wanyama kwa kiwango kwamba haking'oki, kama Mlima. Maana ya Ghariza ni zile sifa bainifu, maelekezo hayo, mielekeo hiyo, vitu ambavyo vimewekwa ndani ya binadamu na wanyama na viumbe hivi. Huzaliwa nazo vitu hivyo na kwamba vitu hivyo vimepandwa katika kina kirefu sana hivyo kwamba ukitaka kuving'oa having'oki.

Kama ukijaribu kuondosha Ghariza basi utu na unyama utatoka nao pia. Hisia hizi na maelekezo haya yamewekwa kwa kutengansishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwanza Mwenyezi Mungu

Mtukufu aliumba umbile la mwili wa binadamu, halafu akakamilisha Tabiyat yake, na baada ya kukamilisha hiyo akaiwekea Ghariza kwa utenganisho ambayo ni mahitaji ya binadamu; lakin hayo yaliwa mahitaji ya utu na sio mahitaji ya kimaumbile ya binadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alikamilisha mwili wa binadamu.

Hii ilikuwa ni hatua ya uumbaji wa mtu, baada ya hatua hiyo ulikuwa ni wakati wa kukamilisha upande wa kimaumbile wa binadamu ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka Ghariza ndani ya binaamu. Maana ya Ghariza ni silika za asili ambazo zimebekwa na zipo ndani ya binadamu na wanyama na huzaliwa nazo. Mabingwa wa saikolojia ya binadamu wanasema kwamba zipo takribani silika za asili kumi na nne (14) ndani ya binadamu.

Wakati ulipokamilika uumbaji wa upande wa kimaumbile wa binadamu, wakati wa kupuliza roho ndani ya binadamu akawadia. ‘Sasa napaswa kumfanya awe mtu.’ Wakati huu Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka Fitra ndani ya binadamu. Kwa hiyo mtu ni nani? Mtu ni muunganiko wa Fitra, Tabiyat na Ghariza. Tabiyat na Ghariza vilikamilishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini Fitra inahitaji Tabiyat na Ghariza ili iweze kujielimisha yenewe. Fitra hujiangeza yenewe na hukua.

Kiumbe ambaye hana Fitra ila anayo Tabiyat na Ghariza tu ni mnyama. Kiumbe ambaye hana Ghariza pia ni yule ambaye hana uhai. Binadamu anazo Ghariza (silika za asili) kadhaa ndani mwake. Njaa, kiu vyote vimepandikizwa ndani mwake na kisahani hiki kimewekwa ndani ya binadamu. Hizi silika za asili (Ghariza) huanza kufanya kazi polepole. Tamaa ya ngono pia ni silika ya asili. ‘Ewe binadamu! Wewe ni Fitra, Tabiyat na Ghariza na tumekukabidhi wewe udhibiti na mamlaka. Utu wako sio kwa sababu ya Tabiyat na Ghariza yako, utu wako upo juu ya msingi wa Fitra.

Nimekupeleka hapo duniani ili ujikamilishe wewe mwenyewe, kujikamilisha kuwa nini? Sio kulea Tabiyat na Ghariza yako, vitu vilivyopo ndani mwako, programu zote hizi nimeziweka Mimi. Nimeweka uwanja kamili usiokuwa na kitu kwa ajili yako ambao unapaswa uutengeneze wewe mwenyewe. Mimi nimetengeneza fremu na wewe mwenyewe unapaswa kuweka kila kitu ndani humo. Na hiyo ndio Fitra yako. Na chochote utakachoweka ndani humo ndivyo na wewe utakavyokuwa.'

Haya ni mapambano ambayo wengi hushindwa. Pale ambapo binadamu hushindwa kujitambua kwamba yeje mwenyewe ni nani, hushindwa kufuata njia yake ya utu. Ama huwa anailea Tabiyat yake au huitunza Ghariza yake tu na anapopata muda huelekeza usiku-vu wake kwenye Fitra yake. Baadhi ya watu huwa wapo kwenye kiwango cha Tabiyat tu na maana yake ni kwamba inahusu ukuaji wake tu. Watu hawa wanataka kuenea na kukua kama mti. Kufuatana na tafsiri ya Ayatullah Jawwad Amouli watu kama hao wapo kama mti ambao umekua na kutandawaa. Na baadhi ya watu huwa wana Ghariza peke yake ndani mwao. Jinsi wanyama wanavyokuwa kwenye mwendo kwa kutumia silika za asili ndivyo watu wengine hutembea kwa silika zao za asili tu. Hii ndio sababu ya wanyama kuwa alama ya binadamu kwani wao wanazo silika za asili tu na sio akili.

Maisha ambayo mnyama alikuwa anaishi miaka milioni moja iliyopita bado anaishi maisha kama hayo hata leo hii; mnyama hajaendelea kabisa. Lakini ukiangalia maisha ya binadamu, maisha yake ya miaka mia moja iliyopita yamebadilika kwa kiwango kikubwa. Binadamu amepewa akili ambayo ni mojawapo ya uwezo wa Fitra, lakini wakati fulani akili nayo huwa chini ya udhibiti wa Ghariza. Fitra hutawaliwa na Ghariza. Wajibu wa binadamu ni kuelimisha Fitra yake kwa kutumia Tabiyat na Ghariza.

Hapo Karbala vilikuja vitu vitatu vili vyokamilika yaani Fitra, Tabiyat na Ghariza. Upande mmoja ulikuwepo na watu ambao mwenendo wao uliwekewa mpaka kwenye Tabiyat na Ghariza, ambapo upande mwingine alikuwepo mtu ambaye aliikamata na kutwaa Tabiyat na Ghariza, na amefika hadhi ya Fitra. Haya ni majeshi mawili. Ni kitu rahisi sana. Kwa nini Kufi hakuja? Tunajaribu kutafuta sababu za kijamii na kisiasa. Kwa nini watu hawahudhurii kwenye Majalis (Mikusanyiko ya kidini) leo hii. Tunajaribu kutafuta sababu zinazohusiana na usalama (nchini Pakistani). Viwanja fulani ambavyo vimeachwa wazi, havikuachwa wazi kwa sababu za kijamii na kisiasa, lakini viwanja hivi vimeachwa wazi kwa sababu za kibinadamu. Fitra haiwezi kuwa nje ya kiwanja hicho ambamo inapaswa kuwamo na vivyo hivyo na Ghariza pia haiwezi kuwa nje ya kiwanja ambacho hicho ambamo inapaswa kuwepo. Kila kimoja ya vitu hivi viwili kitakuwepo ndani ya viwanja vinavyoendana navyo. Kwa nini Kufi hakufika Karbala? Alikuwa na utashi na matamanio, lakini kwenda Karbala na Tabiyat na Ghariza bila Fitra haingetosha, Fitra pia ilikuwa inahitajika. Na Kufi alishindwa katika uwanja huu. Mtu anayeifanya Fitra yake kuwa mshindi huenda kwenye uwanja huu.

Swali ambalo kwa kawaida huulizwa ni kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka hivi vitu vitatu ndani ya binadamu. Kwa nini haikuwekwa Fitra peke yake, ambayo haingetuweka kwenye hizi changamoto zote ambazo ni ngumu? Jibu ni kwamba kama ingewekwa Fitra peke yake basi sisi tusingekuwa binadamu, tungekuwa Malaika. Mwenyezi Mungu Mtukuffu aliwaumba binadamu pamoja na kwamba Malaika tayari walikuwepo kwa sababu Malaika hawangeweza kutimiza mahitaji yale ambayo yangetimizwa na binadamu.

Sababu ya pili ni kwamba Fitra huzaliwa pale ilipo Tabiyat. Fitra inapaswa kuzaliwa pamoja na Tabiyat. Tabiyat ni uwanja na Fitra

ni tunda. Ghariza ni njia na Fitra ni ule uwezo unaotumia njia. Fitra inapaswa kukua na kuelimikia, na kwa ajili ya ukuaji huu inahitaji Tabiyat na Ghariza. Miongoni mwa hizi silika ipo njaa na kiu; sasa kwa kuwa Fitra inahitaji Tabiyat kwa ajili ya ukuaji na akili ambayo Tabiyat inayo ipo ndani ya Ghariza.

### **Falsafa ya Furaha:**

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka njia ya kuendelea kudumu kwa binadamu ndani mwake mwenyewe kwa busara ya ajabu. Kama tukitafakari kuhusu binadamu basi yeye mwenyewe ni kiumbe wa kustaajabisha. Binadamu amepewa uwajibikaji wa kuendelea kudumu yeye mwenyewe na jamii ya binadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametengeneza mpango wa ajabu wa binadamu kutekeleza wajibu huu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametengeneza mpango wa chakula kwa ajili ya binadamu kuendelea kudumu. Binadamu anatakiwa kula chakula kwa sababu chakula kinahitajika mwilini mwake.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka furaha katika chakula kwa sababu sio lazima kwamba kila mtu anaweza kuwa na uwezo wa kujitambua mwenyewe jinsi inayofaa ambamo ataelewa falsafa ya chakula. Kama kitendo cha kula chakula kingefaradhishwa kama Swala, pasingekuwepo na furaha katika kula chakula; ni Maulana tu ndio ambao wangkuwa wanakula chakula na sisi wengine wala hatungejali hata kukikaribia.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliweka starehe katika chakula ambacho ni hitaji la msingi la kuendeleza uwepo wa binadamu, na ili kuweza kupata starehe kwenye chakula Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka Ghariza ndani ya binadamu. Haja ya uwepo wa kudumisha umaumbile wa binadamu ni chakula ambapo haja

ya Ghariza ni starehe. Binadamu hula chakula kwa ajili ya starehe na starehe ni mfumo wa kibinagsi wa kuendelea kudumu alio-wekwa ndani ya binadamu. Inawezekana na inatokea kwamba Fitra ya binadamu hutiishwa, na ambapo bado hata mhusika hajabalehe lakini anakuwa nayo elementi ya starehe ndani ya Ghariza bado ataendelea kula kwa sababu tu anapata starehe katika kula chakula. Mtu ambaye amebalehe huwa hali chakula kwa sababu ya starehe, bali hula chakula kama kitu cha lazima kwa kuendelea kudumu kwake, lakini mtu ambaye hajabalehe hula chakula kwa ajili ya starehe.

Kitu kingine cha muhimu kwa binadamu ni kuendelea kudumu kwa jamii ya kibinadamu ambayo hufanyika kupitia kuzaliana. Kama starehe haingewekwa katika kuzaliana kupitia uhusiano wa kingono, basi hakuna mtu ambaye angeoa. Kama kuoingekuwa ni jambo la faradhi lakini bila kuwepo starehe ndani ya jambo hili basi ni Maulana wachache tu ndiyo wangeoa. Sasa basi pamoja na kwamba starehe imewekwa kwenye kitendo hiki bado baadhi ya watu hawaoi lakini wao hupata tu ile starehe iliyopo ndani ya kitendo hicho basi. Starehe ya ndoa ni dhamana ya kuendelea kudumu kwa jamii ya binadamu.

Pamoja na starehe hizi, pia Mwenyezi Mungu Mtukufu amem-pa binadamu akili ambayo ni uwezo wa roho na pia mwongozo wa kuziwekea mipaka starehe hizi, ili kwamba makusudio yote yanahifadhiwa; uwepo wa binadamu unahifadhiwa na mpango wa kuzaliana kwa binadamu pia unaendelea. Leo hii tumebakira na starehe tu lakini tumesahau falsafa yake; tunapata starehe kutoka vyanzo mbalimbali lakini mpango uliowekwa kwa ajili ya kuhifadhi jamii ya binadamu hautimizwi na sisi. Mtu anafikia umri wa miaka 35 lakini bado hajaoa; msichana anazidi kuwa na umri mkubwa lakini haolewi kwa sababu tu mwanamume wa kumuo hana kazi nzuri,

hajamaliza masomo, hana nyumba nzuri ya makazi yake na sababu zote za kimaumbile kama hizo.

Mvulana huyohuyo anapohisi njaa kwa nini mama yake hamwambii kwamba bado hajafanya shahada yake ya Uzamili, amalize shahada yake ya MBA kwanza hapo ndipo ampe chakula. Na anapo hitaji maji ya kunywa asimpe maji, ye ye aseme kwamba kwanza apate shahada, apate kazi nzuri, na nyumba nzuri ya makazi yake hapo ndipo ampe maji. Ni vema mtu kusoma na kupata shahada kwani hayo ni mahitaji ya mtu, lakini sio kukifanya chakula kiwe tegemezi kwa shahada za kisomi. Kama mtu hajala chakula basi hataweza kudumisha maisha yake na bila kula chakula mtu hataweza kusoma na kupata shahada pia.

Wakati wa kula chakula ukiwadia si vema kuwasilisha hoja za elimu; mtu ale chakula chake safi kilicho halali. Lakini inakuwaje kwenye suala la ndoa hoja za namna hii zinawasilishwa. Mara tu mvulana au msichana akishabalehe wazazi wanatakiwa kutambua haja ya watoto wao kuoa au kuolewa. Kama zikitolewa hoja za kwamba ngoja kwanza amalize masomo, apate nyumba nzuri, gari ya kutembelea na kadhalika basi atakuwa hana utiifu kwa wazazi wake na kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtoto huyu asipopewa chakula ataiba kutoka mahali pengine. Kwa hakika atakula kwa sababu chakula ni haja ya Tabiyat yake na Ghariza inamshawishi kula.

Wale wanaodai kwamba mtoto wake ana umri wa miaka 35 lakini wala hafikirii kuoa wapo sahihi, kwa sababu mtoto wake anakula Pizza mahali pengine. Mtoto ambaye hafikirii suala la ndoa ni kwa sababu ya uzembe wa mzazi wake, lakini mtoto huyo anatimiza starehe yake mahali pengine. Inawezekana kwamba anapata starehe kwa kutumia macho, kwa fikira au kupitia filamu, majarida, na mtandao. Na zipo njia nyingi kama hizo leo hii ambamo mtu

anaweza kupata starehe. Kama ambavyo nimekwishasema mapema kwamba utamaduni wa kimagharibi una nusu ya viwanda ambavyo huzalisha vitu vya kuamsha ashiki na nusu nyininge huzalisha vitu vya kutuliza matamanio hayo.

Ufisadi huu ambao umeenea kila mahali na mamia ya idhaa za runinga ambazo zimeingia hadi kwenye vyumba vya kulala na vyumba vya shughuli za watu, kama hautaguswa na mtoto na je hatat-umia chakula hiki? Mtoto mchanga ambaye anaomba maziwa; kama hakupewa maziwa atalia, na kupiga makelele na kufanya maisha yasiwe na raha.

Mtu mmoja alikuwa anasema kwamba mtoto wake mwenye umri wa miaka miwili ni mtulivu sana hivyo kwamba mara tu anapoo-na picha chafu kwenye runinga mtoto huyu hugeuza uso wake na kutazama upande mwengine. Mtu huyo aliulizwa kama mtoto wake hunywa maziwa lakini hapendi kula chokoleti. Lakini umri wake wa chokoleti utakapofika basi mwache ageuze uso wake. Mtoto huyu hugeuza uso wake kwa ajili yenu ninyi wazazi wake, lakini ngoja umri ufike. Mwenyezi Mungu Mtukufu naawalinde watoto wenu wote lakini kama tukibaki kuwa wazembe basi hili halitatokea. Hadithi ya Mtukufu Mtume inasema:

“Kila mtoto huzaliwa akiwa Muislamu; lakini wazazi wao huwa-geuza kuwa Wayahudi na Wakristo.” Maneno Wayahudi na Wakristo yamenukuliwa tu kama mfano. Ni wazazi wao ambao ndiyo huwfanya watoto wao kuwa kila kitu; wanawafanya watoto wao kuwa malofa, wahuni, hawana nidhamu na kila kitu. Hadithi isemayo “Pepo ipo chini ya miguu ya mama” haina maana kwamba ubusu miguu ya mama. Ni sahihi kwa sababu hadithi hii inarejelea kwenye utiifu kwa wazazi ambalo ni jambo la faradhi hata katika zama hizi za digitali, bila kujali kama mama ni mtu wa kawaida na mbumbumbu na mtoto akawa amesoma. Mtoto anatakiwa kumheshimu

mama kwa sababu mama ni onesho la mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini hadithi hii inayo maana nyingine pia; ambayo ni methali.

Kama vile mtu fulani anahitaji kitu fulani na anakitafuta, na mtu mwingine anakuwa na kitu hicho, na anasema kitu hicho kipo mkononi mwake. Katika lugha ya Kiarabu methali kama hiyo hutumiwa. Pale ambapo kipo katika udhibiti wa mtu kwa uhakika; anasema kitu hicho kipo chini ya miguu yake. Hii maana yake ni kwamba mama anaweza kufanya vyovyyote atakavyo. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa mama hadhi ya juu kwa sababu wajibu wake ni mkubwa. Wape watoto elimu lakini sio kwa ajili ya kupata kazi, bali iwe kwa sababu ya maono ya elimu. Ni wajibu wa wazazi kuwapa watoto wao chakula, na isije ikatokea kwamba mtoto anakwenda kupata chakula mahali pengine. Leo hii baadhi ya wazazi husema kwamba mwanae hali chochote; lakini hawajui anakula uchafu gani huko nje.

Wapo mama wengine hutamka kwa namna ya kujinadi kwamba mtoto wake wala hafikirii suala la ndoa. Mtoto huyo atafikiriaje suala la ndoa wakati yeye ameshiba? Wanawaweka wasichana wao bila kuolewa kwa kungojea mvulana mwenye fahari amuoe! Mzazi anatakiwa kumuoza mwanae kufuatana na viwango vya kidini. Ni kitu kinachoumiza sana kwamba wapo wazazi wanaooza watoto wao wa kike kwa familia zisizo za kidini, halafu upinzani hutoke. Hii ni kwa sababu msimamo wa mvulana unatofautiana na ule wa msichana, kila mmojawao anayo namana yake ya kufikiri kwa hiyo hutoke upinzani na baadaye kutalikiana.

Wazazi wa pande zote mbili wanaweza kuwa wanapendana lakini hawaangalii tabia ya mpenzi wa mtoto wao. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba uwekevu umewekwa katika ndoa al-muradi ndoa inafungwa kufuatana na viwango vya kidini. Funguo

za uwekevu zimewekwa kwenye vitu kama hivyo, lakini na huwa tunashangaa tunaposikia hivyo kwa sababu kwanza tunataka kupata kila kitu kutoka duniani na halafu ndio tuo. Mtu mmoja alimwendea Imam Sadiq ؓ na akasema; “Mimi nina njaa sina chakula.” Imam Sadiq ؓ akamwambia unatakiwa uoe. Mtu huyo alistaajabu na akapatwa na ghadhabu, na akasema kwamba wakati mimi mwenyewe nikiwa peke yangu sina chakula na sasa wewe unanidhihaki kwamba nimpate mtu mwagine tuwe wawili. Maimamu huwa hawana dhihaka wakati wa kutoa mwongozo. Imam Sadiq ؓ alikuwa anamuonesha mtu huyo sehemu ya hazina ya Riziki lakini si kutoka kwa kila umuonaye. Tathimini kikamilifu juu ya viwango vinavyofaa na halafu uoe.

Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka starehe katika Ghariza. Starehe imewekwa ndani ya chakula kwa ajili ya kudumisha maumbile na starehe katika ngono na ndoa kwa ajili ya kudumisha jamii. Lakini kama Ghariza ikiitawala Fitra basi makusudio husahauliwa na kitu kinachobaki ni starehe. Tazama makusudio na falsafa ya chakula ambayo Imam Ali ؓ anasema katika *Dua-e-Kumail*: “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! iimarishe miguu yangu kwa ajili ya kukutumikia Wewe.” Imam Ali ؓ anasema kwamba anataka apate nguvu ili aweze kutumikia dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ili aweze kumwabudu Yeye. Falsafa ya ndoa imetamkwa na Nabii Ibrahim ؓ aliposema: “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Nipe dhuria wema na watakatifu na ukabidhi Uimamu (Uongozi) katika dhuria hao ili waweze kutumikia dini Yako.”

### **Tofauti baina ya Hidayat-e-Takwini na Ghariza.**

Suala linalojitokeza ni juu ya tofauti baina ya mwongozo wa kundelea nao, au mwongozo uliotengenezwa (*Hidayat-e-Takwini*) na

Ghariza. Vitu hivi viwili haviko sawa kwa ajili ya binadamu. *Hideyat-e-Takwini* ni kwa ajili ya wanyama. Mojawapo ya hoja ambayo Nabii Musa ﷺ alimwambia Firauni alipokutana naye kwa kumjibu pale alipomuuliza kuhusu Mola Wake katika Surat-Taha.

قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى

**“Akasema: Mola Wetu ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza.” (Twaha; 20:50)**

Kama tukiwatazama wanyama na tumtafakari binadamu kwa upande wa unyama tu, basi Ghariza ni mwongozo *Takwini*. Kama vile mchwa, nyuki, kasa wote hawa wanao mwongozo *Takwini*. Vivyo hivyo ndani ya binadamu maelekezo yake ya njaa, kiu yote hayo ni mwongozo *Takwini* na ndani ya Fitra pia yapo maelekezo fulani kama vile utambuzi na kadhalika ni mwongozo *Takwini*. To-fauti baina ya mwongozo *Takwini* ndani ya binadamu na wanyama ni kwamba ndani ya wanyama mwongozo huu umewekewa mipaka juu ya Tabiyat na Ghariza yao ambapo ndani ya binadamu pia Fitra ina kiasi fulani cha elementi za mwongozo *Takwini*. Ndani ya binadamu ipo tofauti baina ya Ghariza na mwongozo. Ghariza ni silika na sio mwongozo *Takwini*.

Wakati Fitra inapotiishwa na kuhinikizwa chini ya vifusi vya Tabiyat na Ghariza basi hapo haiwezi kusikiliza mwongozo. Ni kama vile panapotokea tetemeko la ardhi na watu hufunikwa chini ya vifusi; jinsi muda unavyozidi kupita na watu wakiwa bado wamefunikwa chini ya vifusi ndivyo ambavyo itakuwa vigumu wao kusikia sauti za nje. Ni kitu cha namna hiyohiyo ambacho huitokea Fitra pale ambapo Fitra hutiishwa kwa kiwango kiasi kwamba muda hufika ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu husema kwamba umepigwa mhuri kwenye nyoyo zao, na maana yake ni kwamba wahusika hawawezi

kusikia sauti yoyote ya mwongozo; hii maana yake ni kwamba watu wamehnikiza Fitra zao kwa kiwango hicho.

Kama vile ambavyo binadamu ametoa ahadi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuchukua dhamana Yake katika safari hii kama atakavyo binadamu, mnamo siku ya hukumu Mwenyezi Mungu Mtukufu atawauliza binadamu kwamba je wanakumbuka ahadi yao? Haitakuwa rahisi binadamu kukumbuka ahadi hiyo, kwa sababu ahadi hiyo ilifanywa na Fitra ambayo wakati huo imetiishwa na kuhinikizwa. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba asijichoshe katika kuwaongoza baadhi ya watu kwa sababu watu hao ndio wale ambaeo wamewekewa vifusi vingi sana vya Tabiyat na Ghariza kwenye Fitra zao hivyo kwamba hawatasikia mwongozo wowote. Kwa hiyo hakuna haja ya kuwaongoza watu hao. Hii ni sehemu ya chini sana ya Fitra kwa hiyo ni ipi sehemu ya juu zaidi ya Fitra?

Mkengeuko hutokea kwa sababu ya Tabiyat na Ghariza. Ghariza hiyohiyo ambayo ni njia ya Fitra hujielimisha pale ambapo huvuka mipaka na kuponyoka kwenye udhibiti ndipo huitiisha Fitra. Tunapaswa kukumbuka kwamba Tabiyat ni uwanja ambamo Ghariza imepandikizwa. Kama vile matamanio na hasira, vyote hivyo ni Ghariza, na kama vitu hivyo vinabaki chini ya udhibiti wa Fitra huipatia uwezo wa kujielimisha, lakini kama vitu hivyo vikiishinda Fitra humwangamiza binadamu.

Watu huuliza swalii hili kuhusu mipaka ya ukamilifu wa Fitra. Hakuna mipaka kuhusu ukamilifu wa Fitra ambapo tunawenza kusema kwamba Fitra imefika kwenye kituo chake na hakuna haja kuendelea mbele. Hii ndio sababu binadamu ni adhimu zaidi kuliiko Malaika kwa sababu pale ambapo Malaika hufika hatua fulani husema yeye hawezi kuendelea zaidi ya hapo; anasema akienda mbele hata inchi moja tu atajiunguza mwenyewe. Pale anapoishia

Malaika ndipo utu wa binadamu unapoanza. Hakuna mpaka kwa binadamu.

Wakati binadamu anapokuwa roho iliyotosheka;

الْقَسْنُ الْمُطْمَئِنُ

“Nafsi iliyotua” (Sura al-Fajr 89:27)

Basi wito wa Mwenyezi Mungu Mtukufu huja;

أرْجِعِي إِلَى رَبِّكِ رَاضِيَةً مَرْضِيَةً

“Rejea kwa Mola wako hali ya kuwa radhi umeridhiwa”  
(Sura al-Fajr 89:22)

Sasa rudi; Mola wako ameridhika na wewe.

Sisi hufikiri labda Mwenyezi Mungu Mtukufu yupo kama mtoto mdogo ambaye huridhika kwa chokoleti. Kama mtu akitoa sadaka ya mkate uliooza, nguo za mitumba katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hataridhika naye. Mwenyezi Mungu Mtukufu huridhika kwa kuangalia kile kitu cha thamani alichomkabidhi binadamu. Kama binadamu atakuwa amekitunza vizuri kitu kile cha thamani Fitra, basi ataridhika naye, lakini kama binadamu hakijali kitu hi-cho basi hawezi kuwa radhi na mhusika. Mwenyezi Mungu Mtukufu anauliza iko wapi Fitra ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Umekuja kwangu na mtawanyiko huu wa Tabiyat. Mwenyezi Mungu Mtukufu hufurahi kama Fitra huibuka mshindi. Lakini kama ikishindwa binadamu huwa mbaya zaidi ya hayawani. Shimr alikuwa mbaya kuzidi sana hayawani. Qur’ani Tukufu inasema: “Wanakuwa wabaya zaidi sana kuzidi hayawani.” Ni udhalili wa aina gani? Mnyama kamwe hangekunywa maji halafu akaziba njia ili wanyama wengine wasinywe maji. Mnyama atakunywa maji halafu atatoa nafasi ili wany-

ama wengine wanywe pia. Lakini pale ambapo binadamu hushuka hadhi huzuia maji ya kunywa kwa wale ambao ndio njia ya rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu (rejelea tukio la Ashura).

### **Fitra ya mwanamume na mwanamke:**

Fitra (Hali ya kimaumbile), Tabiyat (mambo ya mwili) na Ghariza ni vitu vitatu ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameviweka ndani ya wanadamu. Mojawapo ya vitu hivyo ni mahsus kwa wanadamu; kingine kipo kwa wanadamu na wanyama na kingine kipo ndani ya wanadamu, wanyama na viumbe vingine vyote. Vipo vipengele vitatu katika uumbwaji wa binadamu. Binadamu anao mwili kama viumbe vingine na kwa kuwa mwili huu una mahitaji yake; unahitaji uwepo wa Ghariza na zaidi ya hivi vipengele viwili kwa ajili ya binadamu kupata upendeleo kuliko viumbe vingine, kwa hiyo kilihitajika kitu kingine zaidi cha thamani ambacho ni Fitra.

Roho ni uhalsia wa mwanadamu na mahitaji yake yote, sifa zake bainifu na maelekezo huitwa Fitra. Lakini roho inaweza kufika kwenye ukamilifu wake pale ambapo Tabiyat na Ghariza hufanya kazi ya kuihudumia Fitra na kuwa na manufaa kwa roho. Tabiyat ni kama uwanja na Ghariza ni njia iliyopo mikononi mwa Fitra ambayo itatumika katika kupata lengo la uumbwaji. Tabiyat na Ghariza zimetengenezwa na kuwekwa ndani ya binadamu; vitu hivi havihitaji kukamilishwa. Binadamu anapaswa kukubali chochote ambacho mwili umepewa na pia Ghariza haihitaji kuumbwa au binadamu kuipata Ghariza; vitu vyote hivi viwili viro ndani ya binadamu na binadamu mwanamume na mwanamke huzaliwa navyo.

Fitra ni uhalsia wa mwanadamu ambaye uhalsia wake ni roho, kwa sababu roho inaihitaji Fitra. Kanuni za Tabiyat hazitumiki kwa roho; Ghariza ina kanuni zake yenye na Fitra ina kanuni zake

yenye. Wanamume na wanawake wametenganishwa katika msingi wa Tabiyat na msingi wa Fitra. Ile sehemu ya binadamu ijulikanyayo kama Tabiyat imeumbwa na kuwekwa ndani ya mwanamume na mwanamke. Roho ya binadamu sio ya kiume au ya kike, roho ya binadamu ni ya binadamu tu. Fitra ni moja tu na binadamu mwanamume aliumbwaa chini ya Fitra hiyo nayo Fitra hiyohiyo akapewa binadamu mwanamke. Hii ndio sababu ilikwishatamkwa kabla kwamba Madhehebu ya Imamia ni mazuri sana. Kama mtu akichunguza madhehebu haya basi madhehebu mengine yote ya dunia hujis-alimisha mbele ya madhehebu haya. Leo hii watu wanapiga ngoma kuhusu nafasi ya mwanamke, haki za mwanamke na jinsia ya kike. Ni wao hao ambao humfikiria mwanamke kama kifaa cha kukidhi ashiki. Hii ni kwa sababu wanamume wao wamejiruhusu kutawaliwa na Tabiyat. Wao wanaichukulia Tabiyat kuwa ndio uhalisia wa binadamu mwanamume na mwanamke. Mbele yao, jinsia ya kike ni muhimu zaidi kuliko utu, na muhimu zaidi kuliko utu ni elimu ya binadamu inayohusu binadamu kwanza na mahitaji yake kuliko misingi ya dini.

Hadi hapo ambapo uhalisia wa binadamu haujafafanuliwa hatuwezi kuzungumzia haki za binadamu. Kwanza tunatakiwa kutambua kwamba ni nani tunayemzungumzia? Haki za mwanamke zinaweza kuzungumziwa tu pale ambapo tunajua kwanza mwanamke ni nani? Kama tukiiliza dini mwanamume ni nani na mwanamke ni nani na tuiulize Qur`ani Tukufu. Qur`ani Tukufu inasema kwamba uhalisia wa mwanamume na mwanamke ni Fitra na hakuna tofauti baina ya Fitra ya hizi jinsia mbili. Lakini pamoja na Fitra, uhusiano wa Tabiyat na Ghariza unatofautiana. Mwanamume na mwanamke wanayo maumbile tofauti ya kimwili lakini hiyo sio utu wao. Utu wao hautegemei juu ya umbile la kimwili, ni kwamba utu wao hutegemea kwenye Fitra, na hali hiyo haitofautiani kwa jinsia zote mbili. Lakini

unapofika wakati wa wajibu na kazi hapo ndipo hutokeza tofauti. Zipo tofauti zinazoonekana katika kanuni za kivitendo za Fikihi (*Fiqh*) na hii imefanywa kama msingi wa hoja kwamba Uislamu hu-wadhalilisha wanawake.

Majukumu na kazi hutolewa kwa kuangalia picha kamili ya mwanadamu. Majukumu na kazi hulazimishwa kwa roho lakini roho haiwezi kufanya lolote katika dunia hii bila ya mwili. Kila kitu inachokihitaji roho wakati ipo hapa duniani kitafanyika kupitia mwili. Maumivu, furaha, starehe, huzuni hufika rohoni kupitia mwili tu. Roho huchukua na kutoa kila kitu kupitia mwili. Roho inapaswa kusema na kusikiliza lakini inahitaji ulimi na masikio ya mwili. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiumba roho kwa namna hii tu.

Mwanamume na mwanamke watatofautiana hadi hapo mwili na roho vitakapotengena, na hii pia ilitakiwa kwa sababu ya mwende-lezo wa jamii ya binadamu. Ilikuwa muhimu kuumba jinsia mbili katika wanadamu. Jinsia ya kiume na jinsia ya kike, ili jamii hii ya binadamu iweze kuendelea kuwepo. Ubinadamu haukutofautishwa, isipokuwa kwa ajili ya kuuendeleza ubinadamu huo viumbwe vya aina mbili vilumbwa. Jinsia hizi mbili zote zina dini moja, uhalisia mmoja, Tawhiid moja, Imani moja. Lakini inapokuja kwenye majukumu, baadhi ya majukumu yalilazimu kuwa mahsus kwa mwanamume na baadhi ya majukumu yalilazimu kuwa mahsus kwa mwanamke.

Lakini haiwezekani kutathimini uhalisia wa mtu fulani kupitia majukumu. Kwa mfano mwanamke hawezi kuwa mtawala au Imamu wa nchi ya Kiislamu (Walii Mkuu); hawezi kuwa Nabii au Mtume na inaonekana kwamba Maimamu, Mitume na watawala wote walikuwa wanamume katika nchi ya Kiislamu. Jamii ya majaji, Marjaa ni majukumu ambayo walipewa manamume tu. Hii haimaanishi kwamba mwanamke ni dhalili katika utu na Fitra. Kama majukumu

ya kisheria yamegawanywa hii haina maana kwamba hata uadilifu pia umegawanywa.

Kwa mfano wapo watu wengi wenye vipaji na mabingwa ambao wapo kila mahali. Na katika taifa hilo moja yapo majukumu mengi ambayo yamegawanywa mionganoni mwa wanamume. Katika nchi fulani watu wengine hupewa madaraka ya kuendesha taifa. Hiyo haina maana kwamba hakuna mtu au watu wengine ambao wanawenza kumudu majukumu hayo ya kuendesha nchi vizuri zaidi ya wale waliopewa madaraka hayo. Inawezekana kwamba wapo watu wengi zaidi ambao ni waadilifu kuzidi hao walioko kwenye madaraka, lakini hata hivyo hawajapewa majukumu yoyote. Vigezo vya uadilifu vinatofautiana na vile vya majukumu. Inawezekana kwamba watu wengi wanawenza kuwa waadilifu lakini mionganoni mwao wachache ndio watakaopewa majukumu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amegawanya majukumu, na zile kazi ambazo zinafanyika kwa shida zilikabidhiwa kwa wanamume, na zile ambazo hazifanyiki kwa shida walikabidhiwa wanawake. Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoumba Tabiyat ya wanadamu, alimuumba mwanamume na Tabiyat ngumu na akamuumba mwanamke na Tabiyat laini. Yule aliyeumbwa laini alipewa majukumu yanayolingana na hali yake laini. Yule aliyeumbwa mgumu na imara alikabidhiwa majukumu ambayo yanaendana na vile alivyoumbwa. Ni kinyume na uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba amkabidhi majukumu magumu yule aliyeumbwa laini na kinyume chake. Ukitazama kanuni za Tabiyat na mbali na wanadamu kama ukivitazama viumbe vingine, kwa hakika unaweza kuona mabadi-liko katika Tabiyat.

Katika dunia ya Tabiyat zipo aina mbili za wanyama hai, aina moja ni ile ya wale ambao ni imara sana na wakubwa na wengine ni laini. Kama vile Farasi anayo Tabiyat mahsusini na kufuatana na

Tabiyat yake pia amekabidhiwa kazi ambazo zinaendana na Tabiyat (mambo ya mwili) yake. Unapaswa kupanda farasi katika mashindano ya mbio za farasi, kupanda farasi katika mapigano ya kivita. Pamoja na kwamba punda anaweza kubeba mzigo mkubwa kuliko farasi lakini hawezi kuhimili miondoko ya uwanja wa vita. Hii ni kwa sababu sifa bainifu fulani ziliwekwa ndani ya farasi ambazo ndizo zinasababisha farasi astahili kutumika katika uwanja wa vita.

Kama vile ambavyo ngamia ameumbwa kwa ajili ya maisha ya majangwani. Jinsi umbile lake lilivyo ndivyo na majukumu yake yalivyo. Dunia ya wanyama hawa inastaajabisha kama ukitafakari juu ya Tabiyat na tabia zao. Vivyo hivyo kwa upande wa mimea pia kila kitu kiliumbwaa katika Tabiyat mahsus, na mazingira yali-umbwa kufuatana na Tabiyat zao.

Kama majukumu fulani hayakukabidhiwa kwa wanawake hiyo haina maana kwamba wao wanayo mapungufu katika kuumbwa kwoo. Mwanamke hakupewa jukumu la kuwa Mtume au Imam. Kwa nini? Utume na Uimamu ni jukumu sio uadilifu. Ni hali am-bayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakabidhi baadhi ya watu wali-opendelewa na kuheshimiwa. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu anapokabidhi jukumu, hakabidhi hivihivi tu, vipo vigezo fulani vi-navyotakiwa kutimizwa.

Jukumu na uadilifu ni vitu vinavyotengana. Jukumu hupewa mtu mwenye uadilifu. Uadilifu maana yake ni ukamilifu na jukumu ni wajibu ambao umekabidhiwa kwa mtu ambaye amefikia kwenye ukamilifu huu. Uimamu sio ukamilifu wa uadilifu, badala yake ni wajibu ambao umepokelewa baada ya kufika kwenye ukamilifu. Utume sio ukamilifu lakini ni wajibu uliopokelewa baada kupata ukamilifu. Sheria ya kimungu ni kwamba atapewa majukumu na mamlaka yule ambaye amefika kwenye ukamilifu.

Baadhi ya watu hawaelewi jambo hili na huzungumza vitu vya kupotosha kutokana na hisia zao. Kama vile kuthibitisha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, huzungumza vitu ambavyo hatima yake hukanusha vitu vingi. Kama vile wasemavyo kwamba kazi ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakabidhi Mitume ipo pia kwenye uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambapo angeweza kumkabidhi mtu mwingine yejote pia. Na baadhi yao wamekwenda hadi kwenye kiwango hiki, Mungu apishe mbali, cha kusema kwamba kazi ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakabidhi Mitume ali-kuwa na uwezo wa kuwakabidhi kazi hiyohiyo mbu na inzi. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ni:

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu”**  
**(Sura al-Baqarah 2:20)**

Mulla Sadri anasema kwamba baadhi ya watu wana jicho moja. Mwenyezi Mungu Mtukufu amekabidhi macho mawili ili mtu aweze kuona picha kamili; kama ukitazama kitu kwa kutumia jicho moja utaona nusu ya picha. Baadhi ya watu hutazama dini na Tawhiid pia kwa kutumia jicho moja. Wanapoona kwa kutumia jicho moja wanaweza kuona uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini hawawezi kuona Hekima ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Walisema kwamba uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu unathibitisha kwamba Yeye anaweza kukabidhi kazi yoyote kwa kiumbe chochote. Hii inaonesha kwamba hawajaelewa Tawhiid; Utume na Uimamu.

Ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anao uwezo juu ya kila kitu; kama tu ukizingatia fungu hili la maneno. Kukabidhi kazi ya Mitume kwa mbu na inzi si uwezo juu ya vitu. Hivi si vitu ambavyo vinaweza kuchukua uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu

fu, vitu hivi havimo katika mzingo wa vitu vyenye uwezo wa kuchukua uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ili viwe viongozi wa wanadamu. Ni vitu gani ambavyo havipo katika mipaka ya vitu? Vitu ambavyo haiwezekani kutokea havifikiriwi kama vitu. Swali: hivi Mwenyezi Mungu Mtukufu anao uwezo wa kumuumba mwenza wake Mwenyewe? Watasema nini? Kama anaweza kuumba basi hiyo ni kuvuruga Tawhiid na kama hawezi basi hawezi kundelea kuwa mwenye uwezo (*Qadr*). Kwa hiyo tutapataje ufumbuzi wa suala hili? Kuna jibu gani kwa suala hili?

Jibu lake ni kwamba swalı lenyewe haliko sahihi. Mwenza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hawezi kuumbwa, lakini usilize kama Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweza kuumba hiki au hapana. Uliza kama mwenza wa Mwenyezi Mungu Mutukufu anastahiki kuumbwa? Haiwezekani kuumba wenza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na asili yoyote isiyo na uwepo. Kitu chochote ambacho hakiwezekani hakiwezi kukubali uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ili kuweza kukubali uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kitu hicho kinapaswa kuwa katika mzingo wa uwezekano. Vivyo hivyo asili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hukabidhi kazi ya uongozi wa wanadamu si kwa mwengine isipokuwa Mtume au Imam. Haiwezekani kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu akabidhi kazi ya kuongoza wanadamu kwa mtu ambaye hana uwezo. Ngoja niseme hili kwa mfano.

Unao walimu na maprofesa wazuri sana wa mifumo mizuri ya masomo, na yupo mtoto mchanga wa umri wa miezi sita. Unamchukua mtoto huyu na kumpeleka kwa profesa na unamwambia kwamba kwa sababu amewafanya watu wengi sana wafuzu kiwango cha shahada na PHD, kwa hiyo unataka Profesa amfundishe mtoto wako pia. Profesa huyo atakataa kumsomesha mtoto huyo mwenye umri wa miezi sita kwa sababu haiwezekani. Profesa huyu hawezi

kulaumiwa kwa sababu ya kukataa kumuelimisha mtoto mchanga wa miezi sita pamoja na kwamba amesikika kuelimisha watu wengi mashuhuri.

Sasa ni kitu gani kitakuwa kimetokea kwa kipaji chake? Profesa huyo atajibu kwa kusema kwamba kipaji chake bado kipo imara; kwa sababu kuelimisha kwa kutegemea kipaji cha mwalimu tu haitoshi kwani uwezo wa mwanafunzi unahitajika pia. Mtoto huyu hana uwezo wa kupokea elimu na hali hii haiathiri kipaji cha profesa.

Kama ukimpa bingwa wa fani ya seremala mti wa mgomba, na mgomba una mashina laini sana na ngozi yenye maji ndani yake. Sasa wewe unamwambia atengeneze fenicha kutokana na mti huo wa mgomba. Seremala huyo atakujibu kwamba hataweza kufanya kazi hiyo. Hutakiwi kuwa na shaka na ueledi wake wa kazi hiyo na uanze kumuuliza kuhusu utaalamu wake wa kazi hiyo. Seremala huyo atakujibu kwamba kipaji chake na utaalamu wake hauna shaka kabisa, lakini ili aweze kuonesha kipaji na utaalamu wake katika fani ya useremala anahitaji aina ya ubao ambao unaweza kuhimili uwezo wa taaluma yake.

Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye uwezo usiowezwa anasema kwamba kama Yeye angeteremsha Qur'ani Tukufu hii juu ya mlima, mlima huo ungepasuka na kuteketea. Mlima ulikuwa hauna uwezo wa kuhimili uzito wa mwongozo. Kuhimili mzigo wa cheo cha Utume unahitajika ukamilifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu hampatii mtu cheo cha Utume au Uimamu hadi awe amekamilika kimaadili. Jina la ukamilifu ni *Wilayat* na jina la cheo ni Unabii (*Nabuwat*), Uimamu (*Imamat*). Mtu mwenye kukamilika kimaadili amepata Wilayat. Mara tu mtu anapokuwa *Awliya-Allah* na anafika kwenye hadhi ya Wilayat, basi hapo ni uamuzi wake Mwenyezi Mungu Mtukufu kumpa mtu huyo Uimamu au hapana.

Ukamilifu unahitajika kwa ajili ya cheo na mamlaka lakini wote wale ambao ni wakamilifu inawezekana wasipate cheo. Katika nchi yetu wapo watu wengi ambao wamesoma na baadhi yao pia wana vyo vyeo lakini wapo wengi ambao hawakupewa cheo au hawa jachukua cheo chochote. Ukamilifu kimaadili ni elimu sio cheo. Kama ukimuona mkuu wa chuo katika chuo, ye ye kuwa mkuu wa chuo sio uadilifu, ni elimu yake ndiyo maadili. Inawezekana awepo profesa mwingine hapo chuoni ambaye anayo maadili kama hayo lakini hakupewa cheo cha ukuu wa chuo.

Mwenyezi Mungu Mtukufu hajamuweka mwanamke chini ya mwanamume katika ukamilifu wa kimaadili. Katika uwanja wa ukamilifu wa maadili uwezekano wote uliopo kwa mwanamume pia upo kwa mwanamke. Kama una shaka iulize Qur'an Tukufu kwamba uadilifu huohuo alioupata mwanamume, mwanamke aliupata pia? Lakini cheo na mamlaka alikabidhiwa mwanamume tu kwa sababu mabsusi. Katika Qur'an Tukufu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema nimemteua Mariamu na nimempa ubora juu ya wanawake wote ulimwenguni. Si kwamba Mariamu ﷺ alipewa cheo cha ubora hivihivi tu lakini uadilifu huu ulioneshwa na Mariamu. Mmojawapo wa wema wa asili wa Mariamu ni kwamba Malaika alikuwa akishuka kwake. Ili Malaika ashuke hakuna haja ya uwanja wa kutua badala yake ni moyo safi ndio unaohitajika. Katika *Jamia Kabeer* huwa tunatongoa ‘Amani iwe kwenu ambao Malaika walishuka kwenu mara kwa mara’.

Malaika hawashuki juu ya Milima, wao hushuka juu ya nyoyo safi ambazo husafishwa kwa kupata sifa bainifu zilizo kamili. Ufunuo (*Wahy*) haushushwi kwenye milima hushuka kwenye moyo safi wa Mtukufu Mtume ﷺ. Sasa kama ukiwaliza hawa watu kumi na moja ambao wamefika kwenye hadhi ya Wilayat wanasema kwamba katika hadhi ya Wilayat hakuna anayeweza kulinganishwa na mama

yetu Bibi Fatma Zahra ﷺ. Yeye hakupata cheo chochote cha Uimamu au Utume lakini alikuwa kwenye hadhi ya Wilayat na alikuwa na sifa zote za maadili kamilifu. Hii ni kwa sababu unapokuja kwenye nafasi hizi upo mtambuko wa mawasiliano ya kijinsia.

Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliondoa majukumu yote kuto ka kwa wanawake ambayo kwayo cheo na mamlaka vilihitajika, na pia aliondoa majukumu yote ambamo cheo na mamlaka vilikuwa vitu vya lazima. Majukumu yote ambayo mwanamke angekutana na wanamume, kuzunguka mionganoni mwa (*Nan Mahram*) ajinabi, yaani mtu ambaye unaweza kufunga naye ndoa yaliondolewa kwa mwanamke kwa sababu kazi ya mwanamke ni laini sana. Mwanamke alipewa kazi ambayo mahsusni ni laini. Matunzo na malezi ya Fitra ya binadamu, kuanzia utotonii, alipewa mwanamke na kazi ngumu, inayofanyika kwa nguvu ya msuli alipewa mwanamume.

Utume si uadilifu, uadilifu ni Wilayat. Mtu akifika kwenye hadhi ya Wilayat anapewa cheo cha Utume. Na kazi ya Utume ni kupokea ufunuo (*Wahy*) kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwasilisha kwa wanadamu kwa ajili ya mwongozo. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumpa Utume mwanamke yejote kwa sababu mionganoni mwa wale waliopotoka, wanamume ndio wengi kuliko wanawake. Firauni, Nimrod, Shadad, mionganoni mwa Bani Umayyah watu waliokatili, wengi wao walikuwa wanamume. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa cheo hiki mwanaumume lakini katika matendo mema hadhi ileile ambayo amepewa mwanamume na mwanamke amepewa pia.

Bibi Fatima ﷺ ni *Ismat-e-Kubra* na mwanae Bibi Zainabu ﷺ ni *Ismat-e-Sughra* ambapo yeye hakupewa Umaasumu wowe na Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini alifika kwenye hadhi ya Umaasumu kwa kuutafuta yeye mwenywewe. Imamu Maasumu ﷺ

anasema kwamba “Ewe shangazi yangu wewe ni msomi bila mwali-mu (*Aalima Gair e Muallima*).

Kwa sababu tu ya vyeo vingine vya utawala, mahakama na Mar-jat hazistahili kupewa wanawake tunasema kwamba Fitra ya mwanamume na mwanamke ni tofauti? Sasa katika hotuba ya Imam Ali رض ambamo amezungumzia kuhusu mapungufu ya mwanamke in-gesababisha usumbufu kwa wasomaji. Imam Ali رض anasema wanawake wanayo mapungufu katika Imani, akili na urithi. Hotuba hii ilikuwa inahusu muktadha wa mazingira ya vita vya Jamal. Baadhi ya watu wakawa waathirika wa kutokuelewana na kuchukua manu-faa kutoka kwa mtu.

Rejea hii kwamba wanawake wanayo mapungufu ilikuwa mah-susi kwa ajili ya tukio hilo, kwa sababu Imam Ali رض alikuwa na mwanamke (mkewe) ndani ya makazi yake kwa hiyo asingeweza kutoa hitimisho la jumla. Imam Ali رض hakuwa anarejelea kwenye Fitra ya mwanamke; ambayo ipo sawa kwa mwanamume na mwanamke, na mwelekeo wa Fitra ya mwanamume na mwanamke ni sawa isipokuwa ipo tofauti ya Tabiyat katika maelekezo na uelekeo.

Fitra haina tofauti baina ya mwanamume na mwanamke, na maelekezo yake na uso wake ni kwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ndio maana inasemekana kwamba watoto wote wachanga hu-zaliwa juu ya Fitra ambayo huelekea kwa mintarafu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama wamwabuduo Mwenyezi Mungu Mtukufu lakin wazazi wao huwachukua na kuwapeleka mbali na Fitra na hu-wapeleka kwa mintarafu ya dini nyingine.

## Hivi Uislamu Haujapitwa na Wakati Baada ya Kuwepo kwa Miaka 1400?

Haya ni machafuko mengine ambayo yapo mionganoni mwa baadhi ya watu kwamba inawezekanaje dini ambayo umri wake sasa ni miaka 1400 kuwa ilani ya wanadamu. Hii ni dunia ya teknolojia na sayansi, mlinganishe tu mtu wa miaka 1400 iliyopita na mtu wa zama za sasa na unaweza kuona tofauti kubwa. Kwa hiyo inakuwaje una-wasilisha dini hii yenye umri wa mika 1400 kama ndiyo suluhisho la matatizo ya binadamu wa zama za sasa. Kama dini ni suluhisho basi iwe ni dini ya zama za sasa na si dini yenye umri wa miaka elfu na zaidi.

Katika zama za sasa binadamu amebadilika na hili si jambo la kukanushwa. Baadhi ya wazee hawakubaliani na jambo hili na wao wanajaribu kulazimisha mazoea yale yaliyopitwa na wakati kwa watto. Wazee wanataka mjukuu avae nguo kama zile walizovaa wao wakati wa utoto wao. Hoja hizi zipo kwenye makazi ya watu, na watto wanasema kwamba zama zimebadilika. Ni kweli kwamba mahitaji yamebadilika lakini ni mahitaji gani hayo? Mahitaji ya Tabiyat yamebadilika lakini si mahitaji ya Fitra. Mahitaji ya mwili huendelea kubadilika kila wakati lakini mahitaji ya Fitra hayabadiliki kamwe.

Hivyo basi pale Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoleta dini, ali-fanya kwa kuigawa dini katika sehemu mbili; sehemu moja ilikuwa ile isiyokuwa na mabadiliko. Yaani yale yaliyo halalishwa (*Halal*) ya Muhammad ﷺ yatabakia kuwa halali hadi Siku ya Hukumu na yale ambayo Mtukufu Mtume ﷺ ametangaza kuwa ni Haramu (Yaliyoharamishwa) yatabakia kuwa haramu hadi Siku ya Hukumu. Wakati zama zimebadilika dini ingepaswa kubadilika kwa sababu binadamu anabadilika. Lakini dini haibadiliki na haitabadilika hadi hadi Siku ya Hukumu.

Hii ni kwa sababu dini ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameianzisha ni kwa ajili ya mwongozo wa Fitra ya binadamu. Jinsi Mwenyezi Mungu Mtukufu ambavyo ameitengeneza dini isiwe na mabadiliko ni kwa sababu dini imepelekwa kwa Fitra ambayo kamwe haitabadilika na kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema;

لَا تَبْدِيلَ لِخُلُقِ اللَّهِۚ

**Hakuna mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.**  
**(Sura ar-Rum 30:30)**

Fitra haibadiliki kamwe na itakuwa hivyo daima milele. Tumeona kwamba Shariah nyingi zimekuja, na Shariah mpya zimekuja, kwa hiyo sasa kwa upande wa Uislamu Sharia hazibadiliki hata kama mahitaji ya kimwili yamebadilika?

Hii ni kwa sababu dini imekamilika na ni nzuri sana. Sasa hata Shariah ya dini haitabadilika, lakini kwa ajili ya kuhudumia mwili Tabiyat ya binadamu, mfumo wa Ijtihad (jitihada ya utafiti) umewekwa ndani ya dini. Ijtihad haimaanishi “kuzungumzia mambo ya kale katika zama za leo,” haina maana ya kusema kwa ulimi wako kitu kile ambacho kilikwishatamkwa zamani. Utafiti (Ijtihad) maana yake ni kwamba kila kizazi kinapozaliwa huzaliwa na mahitaji yake mapya na mahsusni kwa ajili ya Tabiyat, lakini Fitra itabakia hivyo bila mabadiliko.

Mabadiliko haya yanayofuatana na Tabiyat ambayo huwa yanakuja katika kila kizazi na huwa yanahitaji Mujtahid kwa kila kizazi. Mujtahid huyu anapaswa kuelewa mahitaji ya kizazi na kukirekebisha kizazi kufuatana na vipengele vya msingi vya dini na wakati huohuo akiwa anarekebisha vipengele vifuatavyo.

Dini ni kwa ajili ya mwongozo wa kila kizazi lakini ili kuifanya dini iwe ya kivitendo mlango wa utafiti (Ijtihad) ni somo ambalo li-

nahitaji kupewa maelezo ya kina. Siku zote pamekuwepo na malalamiko kwamba nchini India na Pakistan hajajitokeza Mujtahid kama ilivyo nchini Irani, Iraq, Lebanon na Afghastan. Ni sawa kama vile unauliza swali kwamba kwa nini aina ya samaki Nyangumi haonekani ndani ya dimbwi lakini anaonekana baharini. Nyangumi ni aina ya samaki anayezaliwa baharini na sio kwenye madimbwi.

Siku ambapo taifa hili litaendeleza utamaduni, fikra, malengo ambayo ni mapana kama bahari, siku hiyo aina ya samaki aitwaye Nyangumi ataonekana ndani ya bahari hii. Endapo fikra zetu ni ndogo mno na mahitaji yetu ni madogo mno sasa kwa nini tunahitaji Mujtahid? Mujtahid anahitajiwa na jamii zile ambazo zinataka kufanya kitu kiulimwengu, wale amba wanataka kuondosha mifumo ya kishetani na kuweka mbadala wa mifumo ya kimungu.

Ili pawepo na mwendelezo na ulinganifu wa dini wakati ambapo Mitume na Maimamu hawapo ﷺ, mipango fulani inapaswa kufanya (kwa ajili ya uzembe wa Ummah). Mpango huo ni utafiti (Ijtihad). Tofauti baina ya Shi'ah na Sunni ni kwamba Shi'ah wannaamini kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alipoondoka duniani alifanya mpango wa uongozi wa Ummah. Kwa hiyo, kwa miaka 250 urithi wa uongozi ulikuwepo lakini uliondoka baada ya Imamu wa 12 ku-chukuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa katika maficho (kwa sababu ya uzembe wa Ummah).

Kwa hiyo sasa labda Imamu (a.t.f.s.) huyu aliondoka na kwenda mafichoni bila ya kufanya mpango wowote kwa ajili ya Ummah? Hivi inawezekana kwamba Imam (a.t.f.s.) alipoondoka alikabidhi Ummah kwa nchi yao au kwa Bani Umayyah, Bani Abbas au wadhalimu fulani? Jibu ni kwamba Mtukufu Mtume ﷺ hakupewa ruhusa ya kuuacha Ummah ujiendeshe wenyewe baada ya yeye kuondoka duniani, na wala Imam Maasumu (a.s.) hakupewa ruhusa ya kuua-

cha Ummah ujiendeshe wenyewe. Ilikuwa muhimu kwao kufanya mipango kwa ajili ya Ummah.

Katika mjadala mchungaji wa kondoo mmoja ambaye alikuwa anakanusha Uimamu; Imamu ﷺ alimpa hoja hii mchungaji huyo. “Wewe ni mchungaji ambaye huwapeleka kondoo malishoni?” Mchungaji akajibu “ndiyo,” Imamu ﷺ akamuuliza “ni kondoo wangapi ambao huwa unawapeleka malishoni?” mchungaji akasema “takribani kondoo mia moja.” Imamu ﷺ akamuuliza mchungaji “kama dharura isiyotegemewa inatokea na unatakiwa kuondoka kwenye konde la malisho na urudi nyumbani hivi utawaacha kondoo wako waendelee kujichunga wenyewe au utamkabidhi mtu aendelee kuwachunga?” Mchungaji wa kondoo akauliza “kwa nini? Hapa jangwani wapo mbwamwitu watawashambulia kondoo.” Imamu ﷺ alimjibu; “hivi thamani ya kondoo wako inazidi thamani ya Ummah wa Waislamu; hivyo kwamba huwezi kuwakabidhi kondoo wako kwa mbwamwitu lakini unaweza kuukabidhi Ummah wa Waislamu kwa madhalimu na mbwamwitu!?”

Mfumo wa utafiti Ijtihad ni kwa ajili ya lengo hili tu kwamba dini ya Fitra inasonga mbele kufuatana na Fitra na mabadiliko yatafanya-ka kufuatana na mabadiliko ya Tabiyat. Hisia kama hizi hazitakiwi kuendekezwa, kwamba dini hii imezeeka kwa hiyo inahitajika dini mpya. Fitra ya mtu wa kwanza kuumbwa duniani itabakia kuwa ileile hata kwa mtu wa mwisho kuzaliwa hapa duniani. Fitra itabakia kuwa ileile kwa wana wa Adamu. Dini itabakia ileile lakini Shariah itabadilika. Katika msamiati wa Kiarabu, Shariah maana yake ni ukingo wa mto ambapo maji hutekwa.

Imetamkwa katika hadithi kwamba dini ni kama mto, na kwenye mto huu kingo nyingi zimetengenezwa katika vipindi vyavizazi vingi lakini maji yanayotiririka kwenye mto huo hayabadi-liku. Mitume wote walikuwa na mafundisho yanayofanana kwa

ajili ya Fitra na kwa hiyo ni muhimu kwa kila Mtume kumthibitisha Mtume aliyemtangulia na kutoa habari njema kwa Mtume anayemfuata yeye. Hii ni kwa sababu ni mfuatano uleule. Pale ambapo Mtume anamthibitisha Mtume aliyemtangulia na kutoa habari njema kuhusu Mtume anayekuja baada yake, ni kwamba anawasilisha haki ya Utume wake. Vivyo hivyo pale ambapo Imamu Maasumu anakwenda mafichoni, kwa kutangaza mpango baada yake anawasilisha haki ya Uimamu huu. Kama Imamu hafanyi hivi basi Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema; ‘Ewe Mtume kama hukutangaza hili basi ni sawa na kwamba hukufikisha ujumbe wowote.’

Jamii hizo zenyе viongozi waliopo sasa haziwezi kuangukia mikononi mwa madhalimu na hakuna ye yeyote anayeweza kufanya lolote kwa jamii hizo. Viongozi, watetezi, mwongozo wa Fitra hulinda dini.

Tabiyat huendelea kubadilika kila mara lakini Fitra haibadiliki, pamoja na kwamba ama inaweza kudhoofika au kuwa na uwezo mkubwa. Fitra huwa na hali ya kupanda na kushuka. Wakati mwingine Fitra hudhoofika sana hivyo kwamba hudhibitiwa na Tabiyat na inapokuwa na nguvu huitawala Tabiyat hiyo.

Katika Surah Shams, Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa ahadi 11 za vitu 11 kutoka kwenye dunia ya Tabiyat. Baada ya kutoa ahadi 11 Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kwamba alitoa ahadi kwa roho na malezi yake, aliweka vitu viwili ndani ya uenyewe huu; Takua (*Taqwa*) na *Fujuur*. Tumeweka Fitra na Ghariza ndani mwake. Na mwenye kufanikiwa ni yule aliyeelimisha na kuing`arisha Fitra yake na yule ambaye ameihinikiza Fitra yake chini ya Tabiyat ameangamia.

Wakati Tabiyat inapoanza kuwa na mamlaka, na Ghariza inapoanza kutawala; wakati Ghariza ya kujipenda mwenyewe, utajiri,

ulafi, ashiki vikiamshwa, basi adui wa uenyewe na adui wa utu hunufaika na hali hiyo. Adui huonesha moto kwenye cheche hii ya Ghariza ilioamshwa, na binadamu hugeuka na kuwa muuaji wa Husein ﷺ.

Zipo Ghariza mbili kuu ndani ya binadamu; mojawapo ni ile ya matamanio (*ishtaha*) na nyingine ni chuki (*Ghadhab*). Kama Ghariza hizi mbili zikielimishwa na kuwa chini ya udhibiti wa Fitra basi hutakasika. Jukumu la *Ishtaha* ni kupendezesha ambapo jukumu la *Ghadhab* ni kuzuia. Ghariza hizi mbili zisipodhibitiwa basi hii Ghariza ya matamanio hugeuka na kuwa ashiki na Ghariza ya chuki hugeuka na kuwa uovu. Endapo hizi Ghariza mbili zikielimishwa na kuwa chini ya udhibiti wa Fitra hugeuka na kuwa uso mzuri ndani ya binadamu. Mojawapo hugeuka na kuwa *Tawallah* (kuwapenda marafiki wa Mwenyezi Mungu Mtukufu) na nyingine hugeuka na kuwa *Tabarah* (hujitenga na maadui wa Mwenyezi Mungu Mtukufu). Wakati Tawalla na Tabarahs zinaingia kwenye uwanja wa kivitendo mojawapo inakuwa *Amr Bil Maroof* na nyingine inakuwa *Nahi Anal Munkar*.

Lakini Tawallah na Tabarah zikiwa chini ya udhibiti wa Tabiyat na Ghariza inakuwa na mamlaka basi kwa sababu tu ya ugavana wa jiji la Ray, inamgeuza Umar ibn Saad kuwa muuaji wa roho takatifu sana ya Husein ؓ. Ghariza humgeuza mtu kuwa Shimr lakini kama Fitra inatakaswa mtu kama Hurr anakuwa Shahidi wa Karbala.

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION**

---

1. i) Qur'an Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili  
ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina - 'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatoo
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqlain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vyta kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vyta kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vyta furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vyta wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlis za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha— Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitoa Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukossoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo  
(Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi